

3000f

**MAUDHUI YA UKIMWI KATIKA *UA LA FARAJA NA*
*KALA TUFAHA***

NA

KINARA GLADYS

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI
NA LUGHA ZA KIAFRIKA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA
KENYATTA.**

JUNI, 2012

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kinara, Gladys
 Maudhui ya ukimwi
 katika ua la faraja



2012/399640

UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU ASILI NA HAIJAPATA KUWASILISHWA
KWA MADHUMUNI YA SHAHADA YOYOTE KATIKA CHUO KIKUU
KINGINE.

JINA: KINARA GLADYS

SAHIHI: 

TAREHE: 12-06-2012

WASIMAMIZI: TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA IDHINI YETU KAMA
WASIMAMIZI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

JINA: DKT. EDWIN MASINDE

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI: 

TAREHE: 12-06-2012

JINA: DKT. PAMELA, M. Y. NGUGI

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI: 

TAREHE: 13-06-2012

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa binti zangu wapendwa Patience Ariri na Prudence Mwende.
Uvumilivu, subira na nguvu mliyonipa ilinipa ari ya kukamilisha kazi hii.

SHUKRANI

Shukrani jazila zimwendee Mwenyezi Mungu kwa kunijalia baraka zake hadi kutimia kwa kazi hii. Ni kwa uwezo na neema yake tu ambapo kazi hii ilikamilika. Atukuzwe milele.

Napenda kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Pamela, M. Y. Ngugi kwa kila hatua ya kazi hii. Msaada wenu wa maoni, fikra, maarifa, mapendekezo na mwongozo wa kila aina, ulinisaidia katika kufikia kiwango hiki, wala hauwezi kusahaulika. Ahsante sana kwa kuvumilia kutoka mwanzo hadi mwisho.

Shukrani ziwaendee wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika. Nilipata maarifa mengi kutoka kwao, ahsanteni sana. Shukrani za kipekee zimwendee Dkt. Richard Wafula kwa miongozo ya nadharia ambayo ilifanya kazi hii kupata mwelekeo. Nasema ahsante sana.

Shukrani za dhati zimwendee Pius Nyakundi katika uhariri wa kazi hii. Wanafunzi wenzangu tuliokuwa nao darasani wanastahili shukrani nyingi. Tulisaidiana kindugu na kuhimizana katika kukamilisha kazi hii. Umoja na upendo tuliokuwa nao ulifaa na sitawasahau. Shukrani za kipekee ziwaendee Priscah Chebet, Fredrick Mayore, Naomi Kuvuna, Atina Nyabokeye na Winie Wachira. Walinifaa sana kwa hali na mali na Mungu awabariki.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wazazi wangu Bw. Naftali Moruri Kinara na Bi. Agnes Kemuma Moruri kwa kunitia ari ya kuendeleza masomo. Uvumilivu wenu pamoja na subira umefanya kazi hii kutimia.

Nawashukuru ndugu zangu Catherine Kerubo, Dennis Kinara, Jane Moraa, Charles Mogusu Debrah Kwamboka, Jackline Nyaboke, Shadrack Kinara na Harriet Nyambeka kwa kunipa moyo na kwa maombi yenu pamoja na msaada wa fedha ulioniwezesha kufaulu.

Mume wangu na rafiki mpendwa Japheth Peter Muindu isingekuwa mawaidha yake ya kunihimiza kuendeleza masomo pamoja na imani yake kwangu, nisingekuwa hapa nilipo. Amenitendea mengi. Sitamsahau Lester Mwetu Peter kwenu nyote nasema ahsante sana.

Mwisho nawashukuru rafiki zangu walionifaa kwa njia mbalimbali. Willy Kipchirchir Toroitich, Jackline Moraa Mabeya, Josphine Injehu Mbira, Ann Kiigi na John Waweru wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Annastasia Njeri Njoroge na Samson Marisa Ogembo wa maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mchango wao katika kazi hii haukadiriki. Kwa wote nasema Mungu awabariki.

MAELEZO YA ISTILAHU

Matini: Kifungu cha maandishi au usemi wa lugha au kitu kinachoweza kujisimamia katika kueleza dhana fulani.

Usemi: Mjadala wa kitaalamu wa kimaandishi au kimazungumzo unaohusu mada fulani ya kisiasa, kidini au hata kifasihi.

Riwaya ya Kileo: Riwaya ya kipindi kilichopo na iliyo chini ya mfumo wa kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kisiasa uliopo. Katika kazi hii tunarejelea riwaya zilizoandikwa kati ya mwaka wa 2000 na 2007.

Matendo ya Usemi: Nadharia inayotumiwa kuhakiki usemi kwa kuonyesha kuwa lugha ina uwezo wa kutenda. Baadhi ya matendo yanayoweza kufanywa kwa kutumia lugha ni kama: kuonya, kutoa amri, kuahidi, kutisha, kufariji kati ya mengine. Katika muktadha huu nadharia hii itachukuliwa kuchunguza jinsi riwaya hizi za *Ua la Faraja* (2005) Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) Omar, B. zilivyo na uwezo wa kuonya na kuhimiza walioathiriwa na UKIMWI kwa kuwapa matumaini.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza jinsi riwaya za: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) zilivyosawiri usemi unaokusudia kuwapa tumaini walioathiriwa na maradhi ya UKIMWI na kuonya wasio na maradhi haya dhidi ya mienendo inayoweza kuwafanya kuambukizwa. Katika kuchunguza jinsi riwaya hizi zilivyosawiri suala la UKIMWI, utafiti huu umechunguza usemi unaotumiwa kuusawiri UKIMWI, athari ya maradhi haya kwa wahusika katika riwaya husika, na kuonyesha nafasi ya riwaya hizi katika kukabiliana na suala zima la UKIMWI pamoja na changamoto zinazotokea. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Naratolojia pamoja na ya Matendo ya Usemi. Kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia zilizotumiwa, mtafiti alihakiki riwaya zilizoteuliwa ili kupata data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti. Data iliyopatikana imerekodiwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia. Data imewasilishwa kwa maelezo katika utaratibu huu: Sura ya kwanza ya utafiti imetanguliza mada, maswali yanayoongoza utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu ya kuchagua mada na misingi ya nadharia. Sura ya pili imechunguza usemi uliotumiwa kusawiri UKIMWI katika riwaya husika. Sura ya tatu imechunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Sura ya nne imechunguza nafasi ya masimulizi haya katika kukabiliana na suala la UKIMWI na changamoto zake. Utafiti huu pia umedengua maana zilizohusishwa na maradhi ya UKIMWI na kuwapa matumaini wanaougua na walioathiriwa. Tumehitimisha utafiti wetu na kutoa mapendekezo kwa tafiti zijazo katika sura ya tano. Utafiti huu umekusudiwa kuwafaa wasomi, watafiti, taaluma ya udaktari, Mashirika Yasiyo ya

Kiserikali yanayoshughulika na kukabiliana na suala la UKIMWI na wanajamii kwa jumla.

YALIYOMO

Mada	(i)
Ungamo.....	(ii)
Tabaruku	(iii)
Shukrani	(iv)
Maelezo ya istilahi.....	(vi)
Ikisiri.....	(vii)
Yaliyomo	(ix)

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada	1
1.1 Suala la Utafiti	5
1.2 Maswali ya Utafiti	6
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.4 Sababu za Kuchagua Mada	6
1.5 Upeo na Mipaka	9
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	10
1.7 Misingi ya Nadharia	18
1.7.1 Naratolojia	18
1.7.2 Matendo ya Usemi	25
1.8.0 Mbinu za Utafiti	27
1.8.1 Ukusanyaji wa data.....	28

1.8.2 Uteuzi wa Sampuli	28
1.8.3 Uchanganuzi wa Data	29
1.8.4 Uwasilishaji wa Data	29

SURA YA PILI: USEMI MBALIMBALI WA MARADHI YA UKIMWI

2.0 Utangulizi.....	31
2.1 UKIMWI ni Uchawi	36
2.2 UKIMWI ni Laana	39
2.3 UKIMWI ni Ugonjwa Mpya	42
2.4 UKIMWI ni Kifo	43
2.5 UKIMWI ni Mdudu	47
2.6 UKIMWI ni Janga	51
2.7 UKIMWI ni Mwiba.....	54
2.8 UKIMWI ni Kudura.....	57
2.9 Mwamko Mpya wa Jamii Kuhusu Maradhi ya UKIMWI.....	58
2.10 Hitimisho	59

SURA YA TATU: ATHARI YA MARADHI YA UKIMWI KWA WAHUSIKA

3.0 Utangulizi	60
3.1 Unyanyapaa	61
3.2 Uyatima	66
3.3 Utamaushi	70

3.4 Ubadilishaji wa Mienendo ya Wahusika	73
3.5 Uadilifu wa Kifasihi	76
3.6 Ujasiri	80
3.7 Udhaifu wa Wanajamii	81
3.9 Hitimisho	84

**SURA YA NNE: MATUMIZI YA RIWAYA ZA *Ua la Faraja na Kala Tufaha*
KATIKA KUKABILIANA NA MARADHI YA UKIMWI NA CHANGAMOTO
ZAKE**

4.0 Utangulizi	85
4.1 Matumizi ya Mipira ya Kondomu.....	86
4.2 Kuacha Uasherati	91
4.3 Uaminifu Katika Ndoa	95
4.4 Ubabe-dume	98
4.5 Vipingamizi vya Kijamii	100
4.6 Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi.....	102
4.7 Kupiga Vita Unyanyapaa na Kuwapa Waathiriwa Matumaini.....	106
4.8 Kupima Damu Kabla ya Ndoa.....	109
4.9 Hitimisho	111

SURA YA TANO: HITIMISHO

5.0 Utangulizi	114
5.1 Muhtasari wa Utafiti	114
5.2 Matokeo ya Utafiti	117
5.3 Mchango wa Utafiti	120
5.4 Mapendekezo	121
Marejeleo	123

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 USULI WA MADA

Tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI katika miaka ya 1980 humu nchini Kenya, jamii imeendelea kuhamasishwa kuhusu jinsi ya kukabiliana na maradhi haya. Baadhi ya makundi yaliyojishughulisha ni kama vile Mashirika ya Kibinafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, wanahabari, wanamuziki, viongozi wa kisiasa, asasi za kidini na wasomi. Waandishi wameshughulikia mada ya UKIMWI kupitia tanzu mbalimbali. Kwa mfano, Mutembei (2009), ameshughulikia ushairi kama utanzu uliojadili suala la UKIMWI hadharani.

Nchi ya Kenya kwa mfano imepata kiwango cha juu cha uhamasisho tangu mwaka wa 1984 wakati maradhi haya yalipogunduliwa. Hata hivyo, uhamasisho huu haujaenda sambamba na kupunguza mienendo ya kingono inayofanya maradhi haya kuenea. Japo matumizi ya mipira ya kondomu yameonekana kuwa njia bora ya kuzuia kuambukizwa na kuenea kwa maradhi haya, mielekeo ya kidini na ya kijamii imezidi kupinga mbinu hii.

Mambo mengine ambayo yamezidi kutatiza vita dhidi ya UKIMWI ni ukosefu wa usawa katika jamii unaoendelezwa na jamii inayotawaliwa na mfumo wa kuumeni, taasubi ya kiume na ubabe-dume, hali ambayo inatiliwa nguvu na ujinga, ukosefu wa usawa wa

kiuchumi pamoja na kufumukana kwa utamaduni uliowaweka wanajamii pamoja (Kebasso na wengine, 2005).

UKIMWI ni suala nyeti lililogubikwa katika siri, unyamavu na unyanyapaa. Kwa sababu hiyo, UKIMWI umekuwa tatizo lililojikita katika utamaduni wa jamii. Kulingana na Muiruri (2010), utafiti uliofanywa na 'Action Aid International (Kenya)' na 'Women Fighting AIDS in Kenya' ulionyesha kuwa idadi kubwa ya wanaougua wanakufa kutokana na unyanyapaa, licha ya rasilmali iliyotumika kuielimisha jamii kuhusu maradhi haya. Vilevile Muiruri anasema kwamba, watu saba kati ya kumi wanaamini kuwa wale wenye maradhi ya UKIMWI wanapata adhabu kutokana na uzinzi. Asilimia hamsini na tano ya watu katika jamii hawawezi kula pamoja na wanaougua, na mmoja kati ya kila watu wawili hawezi kumsalimu kwa mkono anayeugua. Wengi wa walioathiriwa wanaishi katika hali ya makataa. Aidha, utafiti wenyewe ulionyesha kuwa kiasi cha unyanyapaa na ubaguzi kati ya wanawake na watoto walioathiriwa na maradhi haya ni wa hali ya juu. Takwimu zilizopatikana kutokana na utafiti wa vikundi hivi zinaonyesha kuwa asilimia sitini na sita ya walioambukizwa maradhi ya UKIMWI hawafichui hali yao kwa yeyote. Wataalam wa Masuala ya UKIMWI kama madaktari wanasema kuwa kukataa kufichua hali yao ya UKIMWI kwa yeyote kunasababisha unyanyapaa wa kibinafsi. Ama wanapofichua hali yao au jamii inapotambua hilo, husababisha unyanyapaa wa kijamii.

Fasihi ni kati ya njia zinazotumiwa kama jukwaa la kuhamasisha jamii kuhusu masuala yanayowazingira watu. Ni kutokana na kugundua umuhimu wa fasihi katika jamii ndipo Taasisi ya Elimu Nchini Kenya imependekeza kuwa mada kuhusu maswala ibuka yakiwemo UKIMWI yazingatiwe katika Fasihi kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Vilevile ni somo la lazima kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa chuo kikuu. UKIMWI unajitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi kama vile ushairi, riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Kwa mfano kuna hadithi fupi zilizo na visa vya UKIMWI kama vile *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Likizo ya Mauti na Hadithi nyingine* (2007), *Alidhani Kapata na Hadithi nyingine* (2007) miongoni mwa nyingine. Mutembezi (2009) anasema kuwa kuna mashairi mengi ambayo yamechapishwa katika vitabu na magazeti yanayohusu suala la UKIMWI yakiwa na lengo la kuhamasisha jamii na kuionya dhidi ya maradhi hatari ya UKIMWI yasiyo na tiba. Kwa hiyo, mashairi yalionekana kuwa na nafasi kubwa katika kushughulikia suala la UKIMWI. Kama vile ushairi, utanzu wa riwaya una dhima kubwa katika jamii kama vile kukosoa, kuelimisha, kufafanua utamaduni, kuonya, kufichua hali zinazozingira jamii, kufariji na kuburudisha.

Jamii imeibua masimulizi mengi kuhusu maradhi haya ya UKIMWI. Masimulizi haya yananuia kuifanya jamii kuelewa na kupata maana zaidi kutokana na yale yanayowazingira watu. Masimulizi haya vilevile yanajaribu kurekebisha na kurejesha maana halisi hasa pale inapokumbwa na tishio. Kila siku binadamu husukumwa na haja ya kuchunguza na kuumba upya masimulizi yao ya kibinafsi ili kujitambulisha. Kama anavyosema Mark (1987:171-172):

Hatujazaliwa katika mifumo changamano ya masimulizi ya kijamii pekee bali pia tunapata tajriba, uelewa na kuratibu maisha yetu kutokana na masimulizi yanayotuzingira.

UKIMWI ni miongoni mwa masuala ibuka yanayoathiri jamii ya sasa na umeshughulikiwa sio tu na wataalam mbalimbali bali pia na wanajamii wenyewe. Watu mbalimbali wameshughulikia UKIMWI kwa njia tofauti. Lugha teule hutumiwa kama chombo cha kuwasilisha ujumbe na kuhamasisha jamii kuhusu UKIMWI. Kwa mfano, Gachara (2005), amechunguza jinsi lugha inayotumiwa hufanikisha kampeni dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Naye Kimani (2006) anaelezea kuwa kuna uhusiano wa picha na matini katika mabango ya matangazo ya UKIMWI. Kobia (2008) amehakiki sitiari za diskosi ya UKIMWI miongoni mwa wazungumzaji wa Oluluyia wa Magharibi mwa Kenya.

Kutokana na udurusu wa mtafiti, kulikuwa na haja ya kuchunguza jinsi fasihi, hususan, riwaya ya Kiswahili ilivyoshughulikia suala la UKIMWI. Kwa hivyo, mtafiti alidhamiria kuchunguza jinsi ujumbe na taswira za UKIMWI zilivyowasilishwa katika masimulizi ili kuona jinsi yanavyoweza kutumiwa kuonya wale ambao hawajapata maradhi haya kuambaa mienendo inayoweza kuwaingiza katika janga lenyewe na kuwahamasisha na kuwahimiza kwa kuwapa matumaini wale walioathiriwa. Katika kufanya hivyo, utafiti ulikusudia kudengua mitazamo pamoja na maana iliyotokana na utamaduni wa wanajamii inayoendelea kukoleza makali ya UKIMWI. Utafiti ulilenga kupendekeza njia chanya za kukabiliana na UKIMWI.

1.1 SUALA LA UTAFITI

Miongoni mwa majukumu ya riwaya ni kuonya, kukashifu, kuhamasisha, kuelekeza kati ya mengine. Waandishi wa kisasa wamezingatia masuala ya UKIMWI katika kazi zao na wamefanya hivyo kwa kutumia mashairi, hadithi, tamthilia wakiwa na lengo la kuelimisha, kuonya, kuhimiza walio na maradhi ya UKIMWI kuendelea kuishi kwa kuwapa tumaini na wasio nayo kujaribu kujiepusha. UKIMWI umetambulishwa na unyanyapaa, hofu, kifo, uasherati na soni kati ya mengine. Maradhi haya yanaiathiri jamii kwa namna mbalimbali. Masimulizi haya ya UKIMWI yamechochewa na maoni ya umma kama vile: hisia, visasili wala si suala la elimu viumbe. Katika muktadha huu, kuna haja ya kudengua mitazamo hii na kuipa maana tofauti na mbinu anuwai za kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Kwa hivyo, utafiti huu umekusudia kuwa fasihi itaipaa jamii jukwaa muhimu la kukabiliana na maradhi haya.

Utafiti huu umechunguza masimulizi katika *Ua la Faraja* (2005). Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) Omar, B. ili kubainisha namna suala la UKIMWI lilivyosawiriwa kama usemi unaokusudia kuonya wale ambao hawajapata UKIMWI na kuwatia moyo walioathiriwa kwa kuwapa matumaini. Utafiti ulinua kuchunguza usemi unaotumiwa kusawiri suala la UKIMWI, kuonyesha athari ya maradhi haya kwa wahusika na kubainisha nafasi ya masimulizi haya katika kukabiliana na suala zima la UKIMWI na changamoto zake. Katika kufanya hivyo, utafiti umeonyesha namna ujumbe na taswira za UKIMWI zilivyowekwa katika masimulizi ili kuonya jamii dhidi ya mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili.

1.2 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Ni usemi upi umetumiwa kusawiri suala la UKIMWI katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*?
- b) Maradhi ya UKIMWI yanaathiri vipi wahusika katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*?
- c) Riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha* zina nafasi gani katika kukabiliana na suala zima la UKIMWI na zina changamoto gani?

1.3 MALENGO YA UTAFITI

Utafiti umetimiza malengo yafuatayo:

- a) Kuchunguza usemi uliotumiwa kusawiri suala la UKIMWI katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*.
- b) Kuchunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika katika riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*.
- c) Kubainisha nafasi ya riwaya za *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha* katika kukabiliana na suala la UKIMWI na changamoto zake.

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Mshawasha wa kuchagua mada hii ulitokana na sababu kwamba UKIMWI ni suala nyeti katika jamii ya sasa. Kuna waathiriwa na wahasiriwa wengi. Kulingana na UNAIDS (2011), takriban watu milioni 22.9 wanaugua maradhi ya UKIMWI barani Afrika.

UNAIDS wanasema kwamba, idadi hii imekuwa ikiongezeka kila kukicha. Kumekuwa na mielekeo hasi kuhusu walioambukizwa; jambo ambalo limehusisha maradhi haya na unyanyapaa. Kulingana na Nation Correspondent (2006), Kasisi wa Katoliki nchini Kenya Benjamin Nzimbi alisikitika kuwa msimamo wa kanisa la Kikatoliki awali ulishikilia kuwa wanaougua maradhi ya UKIMWI walipata laana kutoka kwa Mungu kutokana na dhambi zao. Jambo hili linaendeleza unyanyapaa kwa wanaougua hivyo kulikuwa na haja ya kuwa na mielekeo bora ambayo itaipa jamii njia chanya za kukabiliana na maradhi haya ili kuwapa wanajamii matumaini.

Pili, kuna haja ya kuwa na mwingiliano wa kitaaluma kati ya somo la Fasihi na taaluma ya udaktari katika kukabiliana na UKIMWI. Uhakiki wa kifasihi unaohusu UKIMWI unatupa uelewa wa kina kuhusu maradhi haya ambayo yametibua maisha ya mwathiriwa (mhusika). Muundo wa masimulizi katika matini unaonyesha tajriba ya wahusika: uchungu, majuto, mapenzi, huzuni na huruma kwa walioathiriwa na unaibua hisia za huruma kwa msomaji. Ili kumtuliza mwathiriwa kwa njia ya kimaadili, daktari anahitaji kujiweka katika tajriba yake, awazie maisha ya baadaye ya mgonjwa, aweke fikra na hisia zake pamoja na mgonjwa, waanze kuandika sura mpya ya maisha ambayo msuko wake umetibuliwa na maradhi ya UKIMWI. Hii ni kwa sababu UKIMWI unaathiri wahusika kutoka katika hali yao ya afya, unawakengeusha, unawadhoofisha na maisha yao yanabadilika. Kwa hivyo, kuna haja ya kutathmini uhusiano huu mpya ili kuwawezesha wahusika kukabiliana na ukweli huu ili kutafuta masimulizi mengine mapya yatakayowawezesha kukabiliana na hali hii ya ramani iliyovurugika. Madaktari na

wauguzi basi wanafaa kujua kuwa waathiriwa sio tu wagonjwa wa kupewa dawa wakiwa na matumaini ya kupona bali ni muhimu wagundue hawa ni wahusika ambao wapo katika hali ya kukadiria thamani ya maisha, mipango ya maisha, mirathi pamoja na kujua kuwa hawa ni wahusika ambao wapo katika upeo wa mgogoro wa nafsi, mwili na akili na hivyo kutafuta njia bora za kuwahudumia.

Tatu, kazi ya uhakiki katika jamii ni kuhamasisha na kuibua mitazamo mipya. Wahakiki wanatumia stadi zao za uhakiki kuelewa jamii ya mwandishi, thamani, falsafa na kuwasilisha kwa hadhira ya mwandishi. Ni muhimu basi kuhakiki na kutathmini masimulizi yanayohusu UKIMWI jinsi yalivyo katika riwaya ya Kiswahili kwa kuwa utaongeze ufahamu wa masuala ya UKIMWI na kuwapatia wanajamii nafasi nzuri ya kufikiria na kuyawazia maradhi haya ambayo yana uwezo wa kuangamiza jamii. Kwa hivyo, uhakiki wa riwaya zinazozungumzia UKIMWI unahitajika kwa sababu utapendekeza njia mwafaka za kukabiliana na UKIMWI na kupendekeza njia bora za masuala ya ngono, kuondoa unyanyapaa na kuchangia kuwapa tumaini walioathirika na walioambukizwa.

Sababu nyingine ni kuwa utanzu wa riwaya unaendelea kuwa kipengele muhimu cha somo la fasihi katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Ni dhahiri kwa hivyo kuwa utanzu huu una sehemu mahsusi na muhimu katika dhima ya fasihi ya kukosoa, kuhamasisha, kutahadharisha, kufundisha, kuelimisha na kufafanua utamaduni wa jamii. Ili kupa utanzu huu dhima yake inayostahili uhakiki umekusudia kuonyesha jinsi

masimulizi haya kuhusu UKIMWI yanavyoweza kuwa usemi wenye kusudi la kuionya jamii dhidi ya mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili na kuwapa moyo walioathiriwa.

Utafiti huu unanua kuwa na umihimu mkubwa kwa wale ambao hawajaathiriwa na maradhi ya UKIMWI na wale walioathirika kwa kuibua njia chanya za kukabiliana na maradhi haya.

1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umeshughulikia riwaya mbili ambazo ni *Ua la Faraja* (2005) ya Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) ya Omar, B. Riwaya hizi ni za kisasa kwa kuwa zimeandikwa katika kipindi tulichomo na pia zimeakisi vyema masuala yanayoathiri jamii katika mfumo wa kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kisiasa uliopo. Aidha, zinashughulikia suala la UKIMWI linaloathiri jamii ya sasa pakubwa.

Japo kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu usawiri wa wahusika katika tanzu mbalimbali za fasihi, utafiti huu umeegemea zaidi upande wa usawiri wa suala la UKIMWI katika riwaya mbili za: *Ua la Faraja* (2005) ya Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) ya Omar, B. kwa sababu UKIMWI unaelekea kuathiri jamii kwa kiasi kikubwa, hasa katika mataifa yanayoendelea. Katika kushughulikia mada hiyo utafiti huu ulichunguza jinsi masimulizi yanavyoweza kusawiriwa kama usemi unaokusudia kuonya wale ambao hawajapata maradhi haya ili kuambaa mienendo inayoweza kuwatia katika

janga hili. Vilevile, utahamasisha walioathiriwa na maradhi haya kwa kuwapa matumaini pamoja na kudengua mitazamo hasi na kuibua mitazamo chanya ya kukabiliana na maradhi haya.

Utafiti huu uliangalia usemi unaotumiwa kusawiri suala la UKIMWI. Aidha ulichunguza jinsi wahusika wanavyoathiriwa na UKIMWI pamoja na kuchunguza nafasi ya riwaya hizi: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) katika kukabiliana na suala la UKIMWI na changamoto zinazotokea.

Uteuzi wa riwaya hizi ulionekana kufaa madhumuni ya utafiti huu kwa vile zilielekea kuwa na upekee fulani: zilikuwa na data ambayo mtafiti angependa kushughulikia. Zinazungumzia suala la UKIMWI kwa kuwamulika wahusika walioathiriwa moja kwa moja na jamii zao. Uhakiki wa riwaya hizi utatupa uelewa mpana wa jamii katika kukabiliana na suala la UKIMWI kwa kuwa waandishi wa fasihi hutoa malighafi yao kwenye mazingira yao.

1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kuna wahakiki wengi ambao wameshughulikia suala la UKIMWI. Mutembei (2009) alifanya utafiti kuhusu UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wake ulisukumwa na hoja kuwa UKIMWI unaegemea zaidi katika tabia ya mtu. Utafiti wake ulilenga kuchunguza mchango wa mashairi katika kuishughulikia tabia ya mwanadamu. Alitumia nadharia ya Mimetiki iliyoangalia mawazo au fikra za mwanadamu kama zenye nguvu na

uwezo wa pekee. Kulingana na nadharia hiyo, fikra ni viumbe hai. Hutungwa, huzaliwa hukua na kufa. Fikra nyingine huwa na muda mfupi wa maisha na kwa hiyo hazidumu na nyingine maisha yake huwa marefu. Fikra hizi hulelewa katika hatua mbalimbali za kukua kwake na huweza kuwaathiri watu. Husambaa na kuenea kutoka sehemu moja hadi nyingine, zikipingwa au kukubalika, zikipunguzwa au kuongezwa kimo.

Kulingana na utafiti wake, fasihi ni matokeo ya fikra hizi ambazo huwamo vichwani mwa wanadamu. Fikra humwathiri binadamu na binadamu huziathiri fikra. Na jinsi adumvyo katika maisha ya mapambano, ndivyo fikra zake zibadilikavyo kuakisi ukweli wa wakati, nazo pengine huwa na umri mkubwa hata kumzidi mwanadamu ambaye akifa, fikra zake huendelea kuwepo zikienea na kuwaathiri wengine. Kwa kuongozwa na nadharia ya Mimetiki, aliangalia fikra za washairi wa Kiswahili kama zinazojirudufu. Fikra hizo zinatokana na ufahamu wa kisayansi na utafiti wa sayansi ya tiba na hasa kuhusu janga la UKIMWI, zinaingia katika mawazo ya washairi wa Kiswahili na zinajidurufu. Kutokea hapo, kila mshairi huathiriwa na vipengele mbalimbali vya maisha yanayomzunguka na kuzitoa kwa njia ya ushairi, kwanza akirudufu zile fikra za awali na kuziongezea na zile zake. Matokeo ya kuathiriana huku ni kupata ushairi wenye nguvu ambao nao una uwezo wa kuathiri wale wanaousoma au kuusikia. Aliona kuwa yaliyojadiliwa yalikuwa na lengo la kutueleza kuhusu tabia, ama kuirekebisha au kuiendeleza, basi kuathiriana huko hakutakoma, kutakuwa ni kama kuambukizana.

Kulingana na utafiti huo, ndani ya vichwa vya wasomaji au wasikilizaji, meme zinapokea fikra za washairi hawa, na zinajirudufu zikiongeza taarifa nyingine ambazo wasomaji au wasikilizaji wanakuwa nazo kuhusiana na janga la UKIMWI. Kwa hiyo, mwitikio unakuwa umepita katika mchakato huo muhimu wa maambukizo. Mchakato huo ndani ya vichwa unaweza kutumiwa kwa faida ya jamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Utafiti wake ulilenga kuchunguza mashairi ya Kiswahili yanavyoweza kutumiwa kubadili tabia ya mwanadamu kuhusiana na suala zima la UKIMWI. Utafiti huu ulichunguza riwaya za *Ua la Faraja* (2007) Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) Omar, B. ili kuchunguza namna zinaweza kukabiliana na UKIMWI kwa lengo la kutahadharisha wasio na maradhi haya kuepukana na mienendo inayoweza kuwafanya kuyapata na kuwafariji walio nao kwa kuwapa matumaini. Nadharia iliyotumika vilevile ni tofauti kwa kuwa utafiti huo ulitumia nadharia ya Mimetiki iliyolenga kuchunguza jinsi fikra za mwanadamu zilivyo na nguvu na uwezo wa pekee. Nao huu ulitumia nadharia ya Naratolojia pamoja na Matendo ya Usemi. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa kulingana na Mutembei (2009), ushairi ndio utanzu wa kwanza katika fasihi kulijadili janga la UKIMWI hadharani kabla ya tanzu nyingine. Kwa hivyo, mtafiti alionyesha yale yaliyofikiriwa na jamii kuhusu UKIMWI katika miaka ya mwanzo ulipotokea. Mkabala wake wa kihistoria na kiulinganishi ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwani ulijenga msingi wa utafiti huu.

Mutembei (2011), alifanya utafiti katika fasihi linganishi uliolenga kuchunguza tamthilia zilizoshughulikia suala la UKIMWI katika mabara mawili tofauti. Alihakiki tamthilia

katika nchi ya Tanzania na Marekani. Utafiti wake ulilenga kuchunguza namna nchi hizo mbili zenye tamaduni tofauti zilivyosawiri maradhi ya UKIMWI, namna zilivyoyaelewa maradhi haya punde tu yalipoanza kuwaathiri wanajamii na nafasi ya kazi hizo za kisanaa katika kuwaelimisha wananchi kuhusu maradhi ya UKIMWI. Kulingana na mtafiti, japo nchi hizo mbili hazingeweza kulinganishwa kiuchumi, kiteknolojia na katika maendeleo ya kisayansi, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti ili kugundua namna maradhi ya UKIMWI yalivyosawiriwa hasa katika nyakati za utandawazi. Vipengele vya kitamaduni vya utandawazi vilimsaidia mtafiti katika kufikia lengo lake. Utafiti uliongozwa na nadharia ya kisemiotiki ya kitamaduni katika ubia wa mawazo. Mtafiti aliona kuwa, tamthilia zilizoshughulikia maswala ya UKIMWI zilifaa kuangaliwa kama ishara katika muktadha maalum wa mawasiliano. Kulingana naye, maradhi ya UKIMWI ni msimbo unaohitaji ujuzi katika utamaduni halisi ili kuuelewa. Utafiti huo ulionyesha kuwa japo nchi hizo ni tofauti na pia zinatoka katika mabara tofauti, waandishi wa kazi za kisanaa walielekea kuwa na mielekeo sawa hasa kuhusu maradhi ya UKIMWI. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulijikita katika riwaya za Kiswahili: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Nadharia zilizotumiwa pia ni tofauti kwa kuwa utafiti huu ulitumia nadharia ya Naratolojia pamoja na Matendo ya Usemi. Hata hivyo, utafiti wa Mutembei ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa tamthilia kama ilivyo riwaya ni jukwaa muhimu la kuwasilisha ujumbe kuhusu maradhi ya UKIMWI.

Kobia (2008), alichunguza sitiari zinazotumiwa kuzungumzia diskosi ya UKIMWI miongoni mwa wazungumzaji wa Oluluyia wa Magharibi mwa Kenya. Utafiti wake

ulijikita katika lahaja za Oluluyia. Data ilikusanywa katika matatu, sherehe za matanga, mikahawa, baa, vyuoni na miktadha mingine ya kijamii katika eneo la Magharibi mwa Kenya. Utafiti wake ulichanganua maana ya usemi unaotumiwa na wanajamii hawa kuashiria maradhi ya UKIMWI. Utafiti wake ulionyesha kuwa ni vibaya kuzungumzia suala la UKIMWI miongoni mwa jamii hii hivyo basi, jamii ilizua sitiari ambazo zingewawezesha kulizungumzia kwa uwazi bila woga. Sitiari hizi zilitokana na lugha ya kawaida ambayo ingewezesha wanajamii kuelewa ulimwengu wa UKIMWI. Sitiari hizi zilionekana kuumba ukweli wa UKIMWI katika eneo la Magharibi mwa Kenya. Pia, zilionekana kuwa muhimu kwa kuwa ziliwezesha wanajamii kupata ujumbe kuhusu UKIMWI ambao ungekuwa vigumu hasa ikizingatiwa kuwa ni mwiko kuzungumzia UKIMWI kwa lugha ya kawaida na hivyo kuathiri mtazamo wa jamii kuhusu suala hili. Utafiti huo uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi na ile ya Uchanganuzi Sitiari. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulijikita katika riwaya za Kiswahili: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Nadharia zilizotumiwa pia ni tofauti kwa kuwa utafiti huu ulitumia nadharia ya Naratolojia pamoja na Matendo ya Usemi. Hata hivyo, utafiti wa Kobia ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa diskosi zinazotumiwa kusawiri UKIMWI zinatokana na sitiari zinazotumia lugha ya kawaida ili jamii iweze kuelewa dhana hii ya UKIMWI.

Vilevile katika mwaka wa 2004, Muriungi alihakiki miili ya wahusika. Kulingana na utafiti wake wahusika wenye afya ndio wanaofaulu katika shughuli za mahaba ikilinganishwa na wanaougua. Wahusika wanaougua maradhi ya UKIMWI

waliwasilishwa kama wanaoharibu utaratibu wa jamii ilhali wenye siha walionekana kutetea utaratibu wa jamii kwa kuendeleza jamii safi na taifa lenye afya. Utafiti ulipendekeza kuwa uhusiano wa mahaba ulitumiwa na waandishi kama njia ya kuiweka jamii katika matabaka. Mawazo haya yalionekana kama njia ya kuingilia njia za kitamaduni za mahaba ambazo zimekuja kutambulishwa kama njia za kudhibiti na kuenea kwa maradhi ya UKIMWI na kuwaadhibu wanajamii na kuwawekea mipaka ya kingono na kijinsia. Utafiti huu ulikuwa na mchango kwa kazi hii kwa kuwa ulichunguza athari ya maradhi haya kwa wahusika. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulilenga kuchunguza jinsi masimulizi yalivyosawiriwa kama usemi unaolenga kuonya na kufariji walioathiriwa na maradhi ya UKIMWI.

Muriungi (2006), alichunguza tabia za wanajamii zilivyoathiriwa na maradhi ya UKIMWI katika kazi za kubuni. Mabadiliko katika uhusiano wa kijinsia na utamaduni ulionyeshwa kuathiriwa na suala la UKIMWI. Wanaume na wanawake nchini Kenya walikabiliwa na haja ya kubadili mienendo yao ya kujamiiiana. Nguvu na mamlaka yanayotokana na taasuba ya kiume, utamaduni, imani, ilionekana kuathiriwa kwa kiasi kikubwa. Utafiti wake ulionyesha kuwa jamii ilipata mapinduzi makubwa kutokana na athari ya maradhi ya UKIMWI. Utafiti wenyewe ulilenga pia kuchunguza jinsi diskosi pendwa zilivyotumiwa ili kuwazia upya tabia za kijamii kuhusu ujinsia kama njia ya kudhibiti kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Utafiti ulionyesha kuwa diskosi pendwa inaweza kuwasilisha ukweli uliofichika kuhusu jinsia, ujinsia, mahaba na masuala ya kiuana kwa namna ambayo njia nyingine za mawasiliano hazingeweza kuwasilisha

ujumbe huu. Utafiti wake ulijikita katika riwaya pendwa na ulilenga muktadha wa UKIMWI ili kuumba upya na kuibua maana mpya na mienendo ya kijinsia ya jamii ya Kenya. Utafiti wake ulikuwa na mchango mkubwa kwa kazi hii kwa kuwa ulionyesha jinsi jamii ilivyoathiriwa kutokana na maradhi haya na kuonyesha haja ya kubadili mahusiano ya kijamii ili kukabiliana na maradhi haya. Pia haja ya kuumba upya na kuibua maana na mienendo ya kijamii upya ulikuwa mchango mkubwa. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa huu ulijikita hasa katika riwaya za: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Pili, kazi hii iliongozwa na nadharia ya Naratoljia na Matendo ya Usemi na tofauti na utafiti wake uliotumia nadharia ya ki-Foucault.

Kimani (2006) alichanganua uhusiano kati ya picha na matini katika mabango ya matangazo ya UKIMWI. Utafiti huo ulizingatia zaidi mchango wa picha katika mabango ya matangazo ya UKIMWI. Mtafiti alizingatia fasiri tofauti za maana na ujumbe katika mabango kwa kuchunguza wapokezi. Utafiti huu ulionyesha kwamba mabango ya matangazo ya UKIMWI yamekusudiwa kufikisha ujumbe kwa wapokezi kila wanapoyatalii wapitiapo mahali yalipoangikwa. Utafiti huo ulionyesha hakuna fasiri inayoweza kusemwa ni ya mwisho. Usawiri wa picha anuwai ni juhudi za kuwasilisha maana na kufikia hadhira kubwa. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulijikita katika riwaya na nadharia zinazotumika pia ni tofauti. Utafiti wake ulitumia nadharia ya Semiotiki na huu ulitumia ile ya Naratoljia pamoja na Matendo ya Usemi.

Gachara (2005) alishughulikia lugha ambayo imetumiwa katika kampeni za kuhamasisha umma kuhusu ugonjwa sugu wa UKIMWI. Alilinganisha na kulinganua utoshelevu wa matini zilizoandikwa na zile za kiusemi katika uwasilishaji wa ujumbe kwa umma. Katika utafiti wake, aligundua kuwa matini zilizoandikwa zilikuwa toshelevu zaidi ya zile zilizokuwa katika hali ya usemi. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa ulijikita katika jamii moja ya Wakikuyu na kutathmini zaidi matangazo yaliyotolewa kwa lugha ya Kikuyu hasa nyimbo na matangazo katika redio na televisheni. Isitoshe, utafiti wake ulikuwa jumulifu katika kuelezea utoshelevu wa matini zote zilizoandikwa bila kutujulisha ni gani iliyo toshelevu zaidi na kwa sababu gani na zile ambazo si toshelevu ni nini hasa kinachofaa kufanywa ili pia ziwe toshelevu. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulijikita katika fasihi na hasa katika riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007).

Sontag (1989), alichunguza lugha na fasiri inayozingira suala la UKIMWI katika *Illness as Metaphor and AIDS and its Metaphors*. Katika utafiti wake, alionyesha dhiki inayowakumba wanaougua maradhi ya UKIMWI kutokana na sitiari mbaya zilizotumiwa kuyaashiria. Kutokana na uchunguzi wake aligundua athari iliyotokana na sitiari hizi ziliwafanya wanaougua kukosa kutafuta matibabu yanayostahili. Aidha, sitiari hizi zilichangia katika kuleta unyanyapaa. UKIMWI ulionekana kama tauni na hukumu kwa mwathiriwa. Licha ya kuwa maradhi haya yanawakumba walimwengu wote na watu wa jinsia zote, ulihushwa na uozo na kupotoka kwa maadili. Utafiti wake ni tofauti na utafiti

huu kwa kuwa ulijikita katika riwaya mahususi. Hata hivyo utafiti wake ulikuwa muhimu katika kuweka msingi wa kazi hii.

Tofauti na tafiti hizo zilizotajwa, utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi masimulizi katika *Ua la Faraja* (2005). Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) Omar, B. ili kubainisha namna suala la UKIMWI lilivyosawiriwa kama usemi unaokusudia kuonya wale ambao hawajapata UKIMWI na kuwatia moyo walioathiriwa.

1.7.0 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu ulitumia nadharia changamano kwa kuwa suala la UKIMWI linaweza kuangaliwa kwa mikabala mbalimbali. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ile ya Naratolojia ambayo ilichunguza usemi mbalimbali uliotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI, wahusika na mtazamo wa msimulizi katika kuandika masimulizi haya. Kwa kuwa nadharia hii ilikuwa pungufu, kulikuwa na haja ya kuongeza nadharia ya Matendo ya Usemi ili ichunguze usemi tofauti uliotumiwa katika riwaya hizi pamoja na kuchunguza namna masimulizi haya yanaweza kutumiwa kuonya jamii dhidi ya mienendo mibaya inayoweza kuifanya kuambukizwa maradhi haya na kuwafaraji waathiriwa kwa kuwapa matumaini.

1.7.1 NADHARIA YA NARATOLOJIA

Naratolojia ni nadharia ya uchunguzi wa hadithi au simulizi. Nadharia hii hutoa vipengele vinavyoweza kutumiwa katika kuzihakiki simulizi (hadithi). Inachunguza sifa

za undani za umuundo wa hadithi, usimulizi wake, mtazamo unaotokea, wahusika na wakati.

Nadharia ya naratolojia ilianza mwaka wa 1966 kule Ufaransa. Hii ilitokana na nadharia ya umuundo iliyochanganua muundo wa simulizi. Neno “naratolojia” lilibuniwa miaka mitatu baadaye na Tzvetan Todorov (1969). Naratolojia basi ilijihusisha na kuchunguza muundo wa masimulizi kwa kugawa vipengele vya simulizi kisha kuzingatia uamilifu na uhusiano. Kimsingi nadharia hii ilitofautisha kati ya kile kinachosimuliwa (hadithi) na vipi kilivyosimuliwa (diskosi).

Wafuasi wengine wa nadharia hii ni kama vile; Prince (1973), Barthes (1975), Genette (1980), na Chatman (1990). Wataalamu wengine ni kama Lord Raglan na Vladimir Propp (1968). Hata hivyo, Kwa mujibu wa Wamitila (2002), nadharia hii iliwekewa msingi wa mawazo na mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato katika andiko lake *Republic*. Utanzu wa fasihi ambao unahusishwa sana na nadharia hii ni wa riwaya.

Suala kuu katika nadharia hii ni simulizi na usimulizi. Hii ina maana kwamba ni sharti kuwe na kitendo cha kusimulia hadithi au simulizi fulani. Kwa mfano, hadithi inaweza kusimuliwa kwa matumizi ya nathari au ushairi, ikawa andishi au simulizi. Kwa hivyo inamjuzu mwana-Naratolojia kuchunguza kilichosimuliwa, matukio yaliyosimuliwa na usimuliaji wenyewe na njia iliyotumiwa pamoja na ufanisi wake.

Usimulizi ni njia ya mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji na kati ya msimulizi na yule anayesimuliwa. Simulizi nayo ni maelezo kuhusu matukio ya kihalisia au ya kubuni ambayo msimulizi huchukulia kuwa ya kuisimua na tena yenye kuwa na umuhimu. Masimulizi huundwa kwa njia ya kuonyesha usimulizi wa mfuatano wa matukio yenye mahusiano. Matukio katika usimulizi yanaweza kuwasilishwa kwa jinsi mbalimbali. Kama anavyosema Genette (1980), kuna mambo matatu muhimu ya kuzingatia katika simulizi:

- (i) Kauli ya kisimulizi au kimaandishi iliyodhamiria kulieleza tukio au matukio fulani.
- (ii) Mfuatano wa matukio halisi au ya kibunilizi ambayo ni kiini au yanalenga usemi fulani.
- (iii) Tendo lenyewe la kusimuliwa au kisimulizi.

Kutokana na maelezo ya Genette (ibid) mambo yanayodhihiriki ni: Simulizi, Hadithi na Usimuliaji. Kwa hivyo, katika simulizi lazima kuwe na utambwaji wa hadithi kwa njia mbalimbali. Aidha, mfuatano wa matukio katika simulizi huweza kuwasilishwa kwa njia mbalimbali. Jinsi kuu ni ile ya uelezaji na uonyeshaji. Plato anatumia dhana ya “daigesia” kwa maaana ya uelezaji na “mimesia” kwa maana ya uonyeshaji. Utafiti ulitumikiza mhimili huu wa kisimulizi au kimaandishi inayodhamiria kulielezea tukio au matukio fulani kuchunguza masimulizi yanayozingira suala la UKIMWI katika riwaya zilizoteuliwa.

Kipengele kingine muhimu katika nadharia hii ni wakati. Wahakiki wa Naratolojia kama vile Genette (1980) na Rimmon-Kenan (1983), wanabainisha kati ya wakati-hadithi na wakati-matini. Wakati-hadithi imechukuliwa kuonyesha wakati ule unaotumika katika hadithi kutokea mwanzo hadi mwisho ambapo yaweza kuwa baina ya siku moja na miaka mingi kiasi cha kuhusisha vizazi vingi. Wakati-matini huchukuliwa kuwa wakati inayochukua matini fulani kusomwa. Kipengele cha wakati huweza pia kuangaliwa kwa kuvichunguza vigezo vingine kama mpangilio, muda na idadi marudio. Vipengele hivi vinakuwa muhimu katika uhakiki unaolenga kuchunguza mfuatano wa kiwakati au kwa kutofungamana nao. Ikiwa yatasimuliwa kiwakati, msuko wa hadithi huwa na mpangilio sawa. Muda nao huurejelea uhusiano katika hadithi. Tukio linaweza kuchukua kipindi kirefu au kifupi. Idadi marudio nayo hurejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi. Inamjuzu mwana-Naratolojia basi kujua kile anachohakiki ili kuweza kutumikiza hoja ya wakati.

Uhakiki wa ki-Naratolojia huangalia wahusika kama kipengele muhimu cha matini ya kifasihi. Manfred (2005) anasema kuwa, kuna mambo kadhaa mhakiki anaweza kuangazia anapochunguza wahusika. Wahusika huchunguzwa kutokana na viashirii mbalimbali. Mhakiki anaweza kuzibainisha njia mbili kuu za kuwatambulisha wahusika katika matini. Kuna uelezaji wa moja kwa moja unaohusu kutolewa kwa maelezo ya waziwazi kumhusu mhusika fulani. Kisha kuna uwasilishaji usio wa moja kwa moja unaohusisha matendo ya wahusika, maneno yao, sura zao, mazingira, mandhari na hali yao kati ya mengine.

Mhakiki anaweza kuchunguza jinsi wahusika wanavyowasilishwa kupitia matendo yao, maneno yao na mazingira yao.

Tunapohakiki hadithi ni vizuri pia tuwe na uhakiki wa kindani na wa kijuujuu. Uhakiki wa kijuujuu humfanya msomaji kusoma kazi ya fasihi kama yenye lengo la kuburudisha. Uhakiki wa kindani nao unachunguza kazi ya fasihi kama yenye kubeba ujumbe wa kina bali na kuburudisha. Katika masimulizi tunaweza kuchunguza yanayosemwa na mhusika mkuu, mhusika mjenzi, msimulizi iwapo ni mmoja kati ya wahusika ambao wamo kwenye hadithi, au iwapo ni msimulizi bila kuhusika katika hadithi.

Kipengele kingine muhimu ni kile cha hali ya msimulizi, sauti ya msimulizi na mazaji. Genette (ibid). Sauti ya msimulizi inajenga mawasiliano na anayesimuliwa. Yeye ndiye anayetoa mtazamo wa masimulizi, mfuatano, na kuchagua ni nini cha kuwacha katika masimulizi na pia kutoa dhamira. Pia kuna mazaji ambayo yaweza kuwa ya kukubali, kuonyesha furaha, huzuni ambayo pia inachangia hali ya masimulizi.

Mtazamo wa msimulizi pia ni muhimu. Msimulizi kwa wakati wote huwa na dhamira au mwelekeo fulani ambao anakusudia msikilizaji au msomaji wake kujishirikisha nao. Genette (1980) anasema katika uhakiki wa matini ni vyema kuweza kutambua: ni nani anaona? “Nani anayewakilisha mtazamo wa msimulizi? Nani anayezungumza”. UKIMWI. Mtazamo wa msimulizi ulituwezesha kuchunguza kusudi la masimulizi haya jinsi yanavyoweza kutumiwa kuonya wale hawajapata maradhi haya kuambaa mienendo

inayoweza kuwaingiza katika janga hili na kuwafariji walioathiriwa kwa kuwapa matumaini pamoja na kuchunguza ujumbe, taswira na maana zinazoweza kutokana na suala zima la UKIMWI.

Maswala mengine muhimu katika uhakiki wa ki-Naratolojia ni usemi. Usemi wa masimulizi ni yale yaliyosemwa au matini inayotokana na tendo la usimulizi. Kama anavyosema Dolozel (1973), matini yoyote ya kisimulizi ni ufungamano wa usemi wa msimulizi na usemi wa wahusika. Hii ina maana kwamba usemi waweza kuwa wa msimulizi unaojumlisha matukio yanayosimuliwa na maoni ya msimulizi na usemi wa wahusika unaojumlisha masimulizi ya vitendo na. Kimsingi simulizi inaweza ikawekwa katika sehemu mbili: usemi wa msimulizi unaojumlisha matukio yanayosimuliwa na maoni ya msimulizi na usemi wa wahusika unaojumlisha masimulizi ya vitendo na maneno. Mhimili huu ulituwezesha kuchunguza kile kinachosemwa na msimulizi, wahusika na maoni yao kuhusiana na suala zima la UKIMWI

Kwa jumla Genette anadokeza dhana zifuatazo kuwa za umuhimu mkubwa katika nadharia hii; mpangilio, wakati, hali, mazaji, dhamira, uhusika, mtazamo, simulizi, mandhari kati ya mengine.

Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulilenga kuchunguza jinsi suala la UKIMWI lilivyoshughulikiwa kama usemi unaokusudia kuonya wale ambao hawajapata maradhi

haya na kuwapa tumaini walioathiriwa. Tafiti hizo zilitoa mchango mkubwa katika kuweka msingi wa kazi hii.

MIHIMILI ILIYOTUMIWA KATIKA KAZI HII:

i) Kauli ya kisimulizi au kimaandishi inayodhamiria kulieleza tukio au matukio fulani ilituwezesha kuchunguza yanayosemwa kuhusu suala la UKIMWI katika riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) ili kuona jinsi suala la UKIMWI lilivyoelezwa katika riwaya hizi.

ii) Kipengele kingine muhimu ni usemi. Usemi wa masimulizi ni yale yaliyosemwa au matini inayotokana na tendo la usimulizi. Hii ilituwezesha kuchunguza kile kinachosemwa na msimulizi na wahusika na maono yao kuhusiana na suala zima la UKIMWI.

iii) Uhakiki wa wahusika ulituwezesha kuchunguza jinsi maradhi ya UKIMWI yanavyoathiri wahusika. Tulichunguza yale yanayosemwa kuwahusu, matendo yao, wanayoyasema, mazingira yao ili kuhakiki athari ya maradhi haya katika jamii.

iv) Mtazamo wa msimulizi ulituwezesha kuchunguza kusudi la masimulizi haya jinsi yanavyoweza kutumiwa kuonya wale hawajapata maradhi haya kuambaa mienendo inayoweza kuwaingiza katika janga hili na kuwafaraji walioathiriwa kwa kuwapa

matumaini pamoja na kuchunguza ujumbe, taswira na maana zinazoweza kutokana na suala zima la UKIMWI.

Ijapokuwa nadharia hii ya Naratolojia inachunguza simulizi, haingetosha kufanikisha utafiti huu. Kulikuwa na haja ya kujumuisha nadharia ya Matendo ya Usemi ili kutuwezesha kuchunguza namna masimulizi haya yalivyosawiriwa kama usemi wenye kusudi la kuonya na kuwahimiza walioathiriwa kwa kuwapa tumaini.

1.7.2 NADHARIA YA MATENDO YA USEMI

Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa J. L. Austin katika miaka ya 1930 na akaiendeleza katika mihadhara ya William James katika Chuo Kikuu cha Havard katika mwaka wa 1955. Mihadhara hii ilichapishwa baadaye katika kitabu maarufu cha *How To Do Things With Words* mwaka wa 1962. Austin aliona nadharia hii kama ya maana lakini Searle ambaye aliendeleza katika mwaka wa 1969 na 1979 aliiona kama nadharia ya usemi.

Kulingana na nadharia hii ya Matendo ya Usemi, lugha hutumiwa kutenda. Baadhi ya matendo tunayofanya kwa kutumia lugha ni pamoja na kuahidi, kufariji, kuonya, kukosoa, kutisha kati ya mengine. Wanaoshikilia mtazamo huu wanasema msemaji anapotaja sentensi au usemi huwa anafanya matendo matatu yafuatayo:

Tendo la usemi. Hili ni tendo la kutamka neno au sentensi ikiwa na maana fulani. Maana inaweza kuwa kutahadharisha, kuagiza, kutoa amri, kuhimiza, kutisha kati ya mengine.

Tendo la kusudio. Hili ni tendo la kunuia au kudhamiria kwamba usemi uliotolewa (neno au sentensi) ufasiriwe au ueleweke kwa namna fulani na msikilizaji. Usemi unaweza kufasiriwa kama tendo la kusifu mtu, kuonya, kukashifu, kufariji, kuhimiza kutokana na maneno unayoyasema.

Tendo la mwikio. Hili ni tendo la msikilizaji kuitikia au kujibu kwa kufanya jambo fulani baada ya kuelewa au kufasiri kusudi la usemi uliosema na msemaji. Kwa mfano, mwikio waweza kuwa kukimbia, kulia, kucheka mradi unatenda jambo ambalo unakusudia linaafiki usemi uliotolewa. Iwapo usemi utafasiriwa kulingana na kusudi la msemaji na kuitikia jinsi anavyoambiwa tendo la usemi litakuwa limetimiza masharti kulingana na muktadha unaohusika.

Kulingana na mtazamo huu wa matendo ya usemi, maana ya neno, sentensi au usemi huelezwa kwa kurejelea masharti ya muktadha wa matumizi yanayofaa. Yaani neno au usemi au sentensi inaweza kueleweka inapotolewa katika muktadha unaofaa. Masharti ya kimuktadha yanayotimizwa wakati neno au sentensi au usemi unapotajwa ndiyo maana yake. Neno au sentensi au usemi unapotajwa katika muktadha wa matumizi yasiyofaa haitakuwa na maana na hivyo basi msikilizaji hataweza kujua maana yake na kuelewa kusudi la usemi.

MIHIMILI ILIYOTUMIWA KATIKA KAZI HII:

- i) Tendo la usemi ambalo ni tendo la kutamka neno au sentensi likiwa na maana fulani ambayo yaweza kuwa kuonya, kuagiza, kuhimiza. Utafiti huu ulilenga kutumia mhimili huu ili kuchunguza namna riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) zilivyosawiriwa kama usemi wenye maana fulani. Maana hii ikiwa ni kuwaonya wale hawajapata maradhi haya dhidi ya mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili la UKIMWI na kuwapa matumaini walioathiriwa.

- ii) Tendo la kusudio ambalo ni tendo la kunuia au kudhamiria kuwa usemi uliotolewa ufasiriwe kwa namna fulani na msikilizaji. Usemi unaweza kufasiriwa kama wenye lengo la kusifu mtu, kuonya, kuhimiza, kukashifu miongoni mwa mengine. Mhimili huu ulituwezesha kufasiri masimulizi haya kama yenye lengo la kuonya wale hawajapata maradhi haya kuambaa mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili na kuwafariji walioathirika kwa kuwapa matumaini.

1.8.0 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Mbinu hii ilitumika ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti na mihimilii ya nadharia teule. Maandishi mbalimbali yalipitiwa maktabani ikiwa ni pamoja na majarida, vitabu, makala, mtandao wa mawasiliano ili kupata data faafu kwa mada ya utafiti. Aidha vitabu vya fasihi vilivyoteuliwa kwa minajili ya mada hii: *Ua la Faraja* (2005) Mkufya, W. E. na *Kala Tufaha* (2007) ya Omar, B. vilichanganuliwa kwa kina ili kupata data iliyofaa utafiti. Maandishi mengine

jumulifu ya fasihi yalisomwa ili kumwongoza mtafiti katika kuiweka kazi hii katika mkabala unaofaa.

Vitabu na makala katika mtandao yanayoendeleza nadharia ya Naratolojia na Matendo ya Usemi vilisomwa ili kujenga ufahamu wa mtafiti na kuhusishwa katika utafiti. Mihimili ya nadharia hizi ilibainishwa na kutumiwa katika kuongoza kutafuta na kuchanganua data ya utafiti. Tafiti za awali zinazohusiana na mada hii zilichunguzwa kwa nia ya kupata data na pia mbinu za kuchanganua data.

1.8.1 UKUSANYAJI WA DATA

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka katika riwaya mbili za Kiswahili za: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Mtafiti alisoma vitabu hivi kwa kina na kuyatenga kwa kuyaandika mambo yote yaliyo muhimu kwa utafiti huu katika daftari ili kumwezesha kukamilisha utafiti kwa kupata data iliyotosheleza mahitaji ya utafiti. Mambo yaliyotengwa ni pamoja na usemi uliotumiwa kuusawiri UKIMWI, athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika na nafasi ya riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI na changamoto. Maana zinazotokana na UKIMWI zilidondolewa na kuandikwa kando kama sehemu ya data ya utafiti.

1.8.2 UTEUZI WA SAMPULI

Uteuzi wa sampuli ni wa kimaksudi. Kazi teule za fasihi andishi ya Kiswahili zimeteuliwa kwa sababu kutokana na uchunguzi awali wa mtafiti vimeshughulikia suala

la UKIMWI. Kazi hizi ni: riwaya mbili: *Ua la Faraja* (2005) ya Mkufya na *Kala Tufaha* (2007) ya Omar, B. Kwa kuongozwa na malengo ya utafiti ambayo yalilenga kuchunguza usemi mbalimbali unaotumiwa kusawiri maradhi ya UKIMWI, kuchunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika na kuchunguza namna riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) zinavyoweza kukabiliana na suala zima la UKIMWI na changamoto zinazopatikana. Mihimili ya nadharia ya Naratolojia na Matendo ya Usemi vilevile iliongoza mtafiti katika kupata data inayohusiana na malengo ya utafiti. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulifaa utafiti huu katika kuonyesha jinsi waandishi hawa walivyosawiri suala la UKIMWI. Mbinu hii ilisaidia kuteua hadithi ambazo zimekuwa na mchango mkubwa kwa malengo ya utafiti huu.

1.8.3 UCHANGANUZI WA DATA

Data iliyokusanywa kwa kunukuu kwenye daftari ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti alichanganua usemi uliotumiwa kusawiri suala la UKIMWI, athari za maradhi ya UKIMWI kwa wahusika na nafasi ya masimulizi haya katika kukabiliana na suala la UKIMWI na changamoto zinazotokea. Aidha, uchanganuzi huu uliongozwa na mihimili ya nadharia zilizohusika: Naratolojia na Matendo ya Usemi.

1.8.4 UWASILISHAJI WA DATA

Data iliyokusanywa imewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalizingatia usemi unaotumiwa kusawiri suala la UKIMWI, athari za maradhi ya UKIMWI kwa wahusika na nafasi ya masimulizi haya katika kukabiliana na suala la UKIMWI na

SURA YA PILI

USEMI MBALIMBALI WA MARADHI YA UKIMWI

2.0 UTANGULIZI

Sura ya kwanza ilijumlisha mada ya utafiti, usuli, swala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu ya kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya utafiti. Pia ilishughulikia udurusu wa maandishi yanayohusiana na mada, nadharia zitakazoongoza utafiti na mbinu za utafiti. Katika sura hii tutashughulikia usemi uliotumiwa katika riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Mhimili wa nadharia ya Naratolojia utakaomwezesha mtafiti kutimiza lengo hili ni ule wa usemi. Kulingana na nadharia ya naratolojia, usemi wa masimulizi ni yale yaliyosemwa au matini inayotokana na tendo la usimulizi. Dolozel (1973:4) anasema kwamba matini yoyote ya kisimulizi ni ufungamano wa usemi wa msimulizi na usemi wa wahusika. Hii ina maana kwamba usemi waweza kuwa wa msimulizi unaojumlisha matukio yanayosimuliwa na maoni ya msimulizi na usemi wa wahusika unaojumlisha masimulizi ya vitendo na maneno. Ni kutokana na ufungamano huu ndipo tunapata usemi tofauti unaotumiwa katika riwaya hizi kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Kauli za wahusika hawa na maoni yao yanachangia pakubwa katika kuonyesha jinsi wahusika katika riwaya hizi wanavyoyaona maradhi haya.

Maradhi ya UKIMWI yalitambulika Afrika Mashariki miaka ya 1980. Uvumbuzi wa maradhi haya uliwafanya wanajamii kupitia katika hatua mbalimbali ya kuyumbayumba

kabla ya kupata uelewa kuhusu maradhi haya. Mwanzoni maradhi haya yalijulikana kwa majina mengi ambayo yalitoka kule Marekani ambako ndiko ulikoanzia. Baadhi ya majina haya ni kama; “*Gay Cancer*”, *Wrath of God Syndrome* (WOGS) na *Gay-Related Immunodeficiency Disease* (GRID) na hasa kiini chake kikibadilishwa majina mengi kabla ya kutulia na kukubaliana kuwa ujulikane kama Human Immunodeficiency Virus (HIV) (Schoepf, 2004). Humu nchini maradhi haya yalijulikana kama UKIMWI ikiwa na maana ya Upungufu wa Kinga Mwilini na katika hali hiyo mwili unapoteza kinga ya magonjwa na kusababisha kushambuliwa na magonjwa nyemelezi (Mutembei, 2009). Usemi kuhusu UKIMWI hauwezi kutengwa na historia ya maradhi hasa kwa kuwa tangu kugunduliwa kwake jamii ilizua visasili tofauti kuhusu hadi pale maana yake ilipokubalika na wanajamii kuwa uitwe UKIMWI.

Katika nchi za Afrika Mashariki kwa mfano UKIMWI ulitambulika kwa mara ya kwanza kati ya mwaka wa 1982 nchini Uganda, 1983 nchini Tanzania na 1984 nchini Kenya (Serwadda, 1985) Mwanzoni maradhi haya yalitambuliwa miongoni mwa wanajamii maskini ambao waliishi vijijini na waliojishugulisha na uvuvi na biashara (Lyons, 2004). Utambuzi huu uliwapa wanajamii nafasi ya kuyabatiza majina tofauti kama maradhi ya wafanyabiashara, makahaba na madereva wa masafa marefu ambao walikuwa wakifanya biashara ya usafarishaji bidhaa kati ya nchi ya Kenya, Uganda na Tanzania na jioni wakijipumzisha katika miji midogomidogo iliyochipuka kwenye barabara kuu inayounganisha nchi hizi. Usemi huu ambao ulilenga kuyatambua maradhi haya kama ya

wanajamii fulani uliwafanya wanajamii wengi kutowajibika na hivyo kuendelea kujihusisha na tabia hatari ambazo zilifanya maradhi haya kuenea zaidi.

Mitazamo kuhusu maradhi haya iliwatatiza wanajamii kabla ya kupokelewa na kudhibitiwa. Mitazamo hii uliwafanya wanajamii kuibua majina tofauti ili kuyaashiria. Kuna sitiari kadha zilizotumiwa na wanajamii ili kuwafanya kuelewa maradhi haya kadri yalivyoenea katika jamii. Kwa mfano Kobia (2008) alichunguza semi tofauti katika jamii ya Luyha na akaona kuwa walitumia sitiari tofauti kuashiria maradhi haya. Baadhi ya sitiari hizi ni kama vile “kudungwa na mwiba”, “UKIMWI uliletwa na wazungu”, “mnyama hatari”, “funza” kati ya mengine. Ngoyani (2006) anasema sitiari huwapa wanajamii mhimili wa kuwaza au mche ambao kwa kuupitia ujumbe na matukio yanaonekana. Ujumbe unawafikia hadhira kwa njia yenye nguvu na ya kuvutia mno kupitia kwa sitiari kuliko kutumia lugha ya kawaida. Sitiari kama usemi wa mawasiliano unaibua taswira zenye nguvu ambazo zinaweza kubadili maoni ya umma, mielekeo na ufasiri wa jambo Fulani. Ni kutokana na sitiari hizi ambapo mtafiti analenga kuchunguza usemi mbalimbali uliotumiwa na wanafasihi hususan riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) kuchunguza namna jamii inavyochukulia maradhi ya UKIMWI.

Matumizi ya sitiari hizi ni muhimu katika kuleta taswira kamili na kuonyesha athari ya maradhi haya. Sitiari hizi zinaonekana kama njia ya kuelewa kitu kwa njia ya kitu kingine. Cienki (2005) anasema, sitiari hizi zinazotumiwa katika masimulizi haya zinasaidia kufanya mambo magumu na yenye utata kueleweka katika umma. Matumizi

ya sitari hizi zaweza pia kudengua visasili na kufichua ukweli kwa njia inayokubaliwa bila kumkasirisha yeyote katika jamii (Todoli, 2007). Usemi tofauti uliotumiwa katika riwaya hizi unaibua taswira yenye nguvu na yenye uwezo wa kubadilisha maoni ya jamii, uelewa na ufasiri wa mambo yanayohusu maradhi ya UKIMWI. Taswira hizi zina uwezo wa kutahadharisha wahusika na kuwafanya kuwa makini katika maswala yanayohusu ngono.

Mbali na sayansi, fasihi ni njia mojawapo muhimu ambayo ujumbe kuhusu UKIMWI umekuwa ukipitishwa. Kazi ya fasihi kama vile mashairi, nyimbo, maonyesho na hadithi zimetumiwa na wanajamii kama jukwaa la kutoa ujumbe kuhusu maradhi haya hatari ya UKIMWI. Katika riwaya hizi zilizoteuliwa, UKIMWI umepewa majina mbalimbali. Kutokana na majina hayo wanajamii wanapata uelewa wa kina kuhusu maradhi haya ambayo yameitatiza jamii kwa karibu miongo mitatu.

Kulingana na Cuddon (1997) usemi ni mjadala wa kitaalam wa kimaandishi au kimazungumzo unaohusu mada fulani ya kisiasa, kidini au hata kifasihi. Naye Harmon na Holman (2006), wanasema usemi ni namna ya kuzungumza unaowekewa mipaka na itikadi, utaalamu, utamaduni au jumuiya zenye usosiolojia. Kwa upande mwingine Fairclough (1992) anaona usemi kama matini au matamshi yenye mazoea ya kutangatanga, kubuniwa, kuenezwa, kuzungushwa na kutumiwa na jamii. Hii ina maana kuwa usemi unatokea katika muktadha halisi wa muundo wa jamii. Kwa hivyo katika muktadha huu usemi unachukuliwa kama wenye kubuniwa na jamii na wenye mazoea ya

kubadilika. Tukirejelea matamshi kuhusu UKIMWI usemi huu unabuniwa na wanajamii na kuenezwa na kisha kutumiwa na wanajamii wenyewe. Uchanganuzi wa usemi tofauti ni muhimu katika kuangalia taswira, sitiari na usemi tofauti unaotumiwa katika riwaya za: *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007) ili kuchunguza jinsi jamii imechukulia maradhi ya UKIMWI. Usemi huu unaotumiwa na wanajamii kuhusu suala la UKIMWI umetokana na mazingira yao ya kila siku na unaweza kuathiri fikra zetu na utambuzi kuhusu jambo fulani na kuumba tabia za wahusika hasa kuhusu maradhi ya UKIMWI. Lugha ya tamathali tofauti na lugha ya kawaida inaweza kuvutia na kuwekwa kwenye kumbukumbu ya wasikilizaji na wasomaji kwa hivyo waandishi hawa wametumia usemi tofauti kuyaashiria maradhi ya UKIMWI kutoka kwenye mazingira yanayowazunguka.

Usemi unaotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI unaonekana kubadilika katika fasihi. Kuna usemi tofauti unaotumiwa kama vile UKIMWI ni janga, kifo, laana, uchawi kati ya mengine. Matumizi ya usemi huu, unayanyanyapaisha maradhi haya na kuyafanya kutisha. Kulingana na nadharia ya Matendo ya Usemi (Austin, 1962), lugha hutumiwa kutenda. Jamii inapotumia usemi mbalimbali kuyaashiria maradhi haya inanua kutenda mambo kama vile kuitisha ili kuwafanya kuambaa na kuiogofya dhidi ya mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili. Hili ndilo linajitokeza kutokana na usemi tofauti unaotumiwa.

Tumeshughulikia riwaya ya *Kala Tufaha* na *Ua la Faraja*. Riwaya ya *Kala Tufaha* imeandikwa na Omar Babu na kuchapishwa na Phoenix mwaka wa 2007. Riwaya hii

inazungumzia mhusika Fumbwe ambaye alikuwa mumewe Hatima. Fumbwe anampachika mimba yaya wake aitwaye Kibibi na kukataa kuwajibika katika kulea kitoto hicho (Kala). Hatima naye anafumaniwa na mumewe wakiwa na rafiki yake Chongea. Mwishowe ndoa kati ya Fumbwe na Hatima inavunjika na Fumbwe anajiingiza katika anasa. Hatimaye Fumbwe anapata maradhi ya UKIMWI ambayo yanamuua.

Riwaya nyingine ni ile ya *Ua la Faraja* iliyoandikwa na William Mkufya na kuchapishwa na Longhorn mwaka wa 2005. Riwaya hii inaangazia maisha ya mhusika Ngoma ambaye ana mke anayeitwa Tabu na watoto watano: Juma, Aisha, Abu, Rahma na Nuru. Ngoma ni mfanyabiashara mwenye mali lakini anaitolekeza familia yake na kushiriki katika anasa na Queen na Asha. Mwishowe anapata UKIMWI na kumuambukiza mke wake Tabu. Queen anaamua kujiua, Ngoma anakufa na mwishowe Tabu anakufa na kuwaacha watoto wao mayatima chini ya ulinzi wa Grace ambaye alikuwa dadake Tabu. Sehemu ifuatayo itachunguza semi mbalimbali katika riwaya zilizoteuliwa.

2.1 UKIMWI NI UCHAWI

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007) UKIMWI unachukuliwa kama uchawi. Fumbwe alipoanza kuugua hakujua chanzo cha maradhi yale. Alitafuta matibabu katika hospitali mbalimbali bila mafanikio kwa hiyo alianza kufikiria ni nini hasa kilichosababisha hali hiyo kama inavyojidhihirisha katika nafsi yake:

Alivuta nadhari kukumbuka aliyoyapitia. Watu walisema kwamba maradhi yale kajitakia kwa jinsi alivyoishi. Kwake yeye akiamini kaletewa

na mtu. Ama kachomekwa mzizi au laana. Alihisi kuwa laana yenyewe ni kiumbe ambacho aliwahi kukibughudhi. Kiumbe ambacho hakikuwa na hatia (Omar, 2007:174).

Fumbwe alijaribu kukumbuka ni nani aliyemletea maradhi yale bila mafanikio yoyote. Huenda alidhania ni mkewe Hatima kwa kuwa yeye pia hakuwa mwaminifu katika ndoa lakini hata hivyo Fumbwe alikuwa na wapenzi wengi kwa hiyo hangeweza kutambua chanzo chake. Alipokosa kujua kilichosababisha maradhi yale alianza kukumbuka mambo ambayo alikuwa ametenda. Alikumbuka alivyomnaji Kibibi na kumpachika mimba na kisha kukataa kuwajibika. Ndipo mawazo yakamjia akafikiri kuwa huenda Kibibi alimchomeka mzizi baada ya yote aliyomtendea. Fumbwe alienda katika hospitali mbalimbali bila mafanikio yoyote na alipokosa matibabu aliamua kwenda kwa waganga kama mwandishi anavyosema :

Alikuja huku baada ya kwisha hospitali pamoja na madaktari. Kawaenda waganga na waganguzi. Mizimu pia hakusaza (Omar, 2007:175)

Waganga nao hawakumtibu Fumbwe kwa kuwa haukuwa uchawi. Mwishowe alikufa kutokana na maradhi haya ambayo yaliitatiza jamii na kuifanya kutojua chanzo chake au jinsi ya kukabiliana nayo.

Imani kuhusu maradhi ya UKIMWI kama uchawi pia inashadidiwa na watafiti wengine. Nchini Kenya, kwa mfano katika jamii ya Waluo kuna imani ijulikanayo kama *chira*. Mwita (1993) anasema watu wengi katika jamii ya Waluo huuchukulia ugonjwa wa UKIMWI kama *chira*. Dhana hii imejikita katika imani kuwa kutokana na matendo maovu ya nyakati za nyuma na mtu kutozingatia miiko ya jamii, mtu huyo hulaaniwa, na

laana hii hujitokeza kupitia katika *chira*- ugonjwa wa ajabu wenye kujitokeza kama upele na mtu kukonda hatimaye kufa. Imani kuhusu *Chira* imejikita miongoni mwa jamii ya Waluo ambapo wengine huuona kama suala la uchawi linalofanywa dhidi ya mtu mmoja ambaye ametenda kosa fulani katika jamii (Scott Lee, 2003).

Katika jamii ya Abanyole wa Magharibi mwa Kenya, Alembi (2002) anasema kuwa maradhi yaliyomfanya mgonjwa kuugua na yaliyofanana na *chira* yaliitwa 'ebiila'. Maradhi haya yalitokana na kujamiiana na watu wenye ukoo mmoja na yalikoleza makali yake hasa pale mhusika aliposhiriki ngono na mama wa kambo. Nchini Uganda iliaminiwa kuwa hali ya kuugua kusikopona iliyowapata vijana ilitokana na uchawi (Isichei, 2004). Imani hii ilitokana na sababu kuwa huenda Watanzania waliwaroga Waganda kama adhabu kwa kuwaibia na kuwadhulumu wakati walipokuwa wakifanya biashara nao. Nchini Tanzania wananchi walidhani UKIMWI ni hali ya kiuchawi uliofanywa na Waganda labda kwa vile wafanyabiashara wa Tanzania walikuwa wamewadhulumu (Mutembei 2009 na Alembi 2002). Vilevile, kutokana na mtafaruku ulioikumba jamii kuhusu maradhi hayo na kutokuwa na habari kamili kuyahusu wengi walidhani ni uchawi (Mutembei 2011).

Usemi kuwa UKIMWI ni uchawi unatokana na udhaifu wa mwanadamu katika kupata jibu la tatizo linalomsibu. Wahusika waliougua waliposhindwa kupata matibabu hospitalini, waliekea kwa waganga. Hii bado ikiwa imani kuwa UKIMWI ni uchawi ulifanya maradhi haya kuenea. Shauku ya wananchi ya kutaka kujua maambukizi na

kuenea kwa ugonjwa haikuzimwa haraka. Ombwe lililojitokeza lilizibwa haraka na watu waliojiita waganga. Na watu hawa ambao ni zao la mfumo wa mahitaji ya jamii, huwa na majibu ya haraka kuhusu maswali magumu yanayowakabili wananchi (Schoepf 2004 na Mutembei 2009).

Waganga hawa ikumbukwe kuwa wengi ni wale ambao ujumbe kuhusu maradhi haya waliupata kwenye vyombo vya habari; nia yao ikiwa kupata pesa kutoka kwa wagonjwa bila kujua kuwa walichangia katika kueneza maradhi ya UKIMWI. Hii ndiyo ilikuwa imani ya jamii kabla utafiti wa kina kufanywa. Hata hivyo imani hii iliwafariji wanajamii kama vile Fumbwe wakati alipokuwa akiugua hasa ikizingatiwa kuwa wanajamii hupenda kulaumu wengine kuhusu chanzo cha matatizo yao. Hakuna anayetaka kuchukua wajibu na hivyo kuendelea kufanya ngono ya kiholela bila kujua ulikuwa ukienza zaidi.

2.2 UKIMWI NI LAANA

UKIMWI unachukuliwa kama laana katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007). Fumbwe alipougua hakujua kilichosababisha hali ile. Alienda katika hospitali tofauti kutafuta matibabu lakini hakufanikiwa. Aliposhindwa alianza kukumbuka iwapo kuna mtu ambaye alimkosea na kutokana na matendo yale akamlaani kama inavyojidhihirisha katika kifungu kifuatacho:

Fumbwe alivuta nadhari kukumbuka aliyoyapitia. Watu walisema kwamba maradhi yale kajitakia kwa jinsi alivyoishi. Kwake yeye akiamini kaletewa na mtu. Ama kachomekwa mzizi au laana. Alihisi kuwa laana yenyewe ni ya kiumbe ambacho aliwahi kukibugudhi. Kiumbe ambacho hakikuwa na

hatia. Alikumbuka jinsi kiumbe hicho kilivyomlilia kikitaka akinisuru, lakini yeye akajipa hamnazo akacheza alivyotaka.

Maneno fulani yalivuma kichwani mwake kama kwamba jana, kauli ambazo zimekuwa donda ndugu moyoni mwake. *“Malipo ni papa hapa duniani. Mimi sina uwezo wa kujitetea. Maskini hohehahe hapa nilipo!”* Mwenyewe kuyasema akitokwa na machozi. “Umenitoa kwa wazazi wangu bila hiari umenipa kuazirika! Insha Allah Rabbi akupe kama haya tu. Nyumba uliyojenga uihame kama nilivyohama mimi. ‘Ya Rabbii nimetubu. Hii ni laana ya ..., Fumbwe alikatiza hiyo fikra akapanda kitandani (Omar, 2007: 174 -175).

Fumbwe alipojaribu kuchunguza chanzo cha maradhi yale alimkumbuka Kibibi, mtoto wa Mwalimu Selemani, ambaye alikuwa ameenda kwake kwa ajili ya kulea kitoto chao. Fumbwe mwishowe alimnajisi na kumpachika mimba. Mtoto ambaye alikuwa bikira kwa kujiandalia maisha mema ya ndoa mwishowe alirudi kwao Mferejini. Mwalimu Selemani hangeweza kustahimili aibu ile kwa hiyo, alimfukuza. Kibibi alitaka kujitia kitanzi lakini akaopolewa na Ma’Asha. Baadaye alipojaribu kutafuta haki yake, Fumbwe alimdhulumu kwa kuwa maskini hana haki. Alihakikisha kuwa Kibibi hangemshtaki kwa kuwahonga mawakili wote na kuwatishia iwapo wangemsaidia Kibibi kumshtaki kwa kumbaka. Hilo ndilo lilimla Fumbwe na kumfanya kudhani kuwa kosa hilo ndilo lililosababisha maradhi yake bila kukubali kuwa ni vitendo vyake ndivyo vilivyomtia katika hali hiyo. Kwake yeye aliona ni adhabu ya kosa alilomfanyia Kibibi. Hata hivyo wanajamii wengine waliona kuwa huenda maradhi yale yalitokana na mienendo yake ya kisherati kwa kuwa walijua kuwa kulikuwa na maradhi yaliyoitwa UKIMWI ambayo yaliwaathiri watu kama alivyokuwa akiugua Fumbwe.

Imani kuwa UKIMWI ni laana ni usemi ambao umejisimika katika jamii na kuendelezwa na taasisi za kidini. Kwa mfano, kwenye Biblia katika kitabu cha Yereimia 29:18 Bwana asema “Nami nitawafuatia kwa upanga, na njaa, na tauni, nami nitawatoa watupwe huko na huko katika falme zote za dunia, wawe kitu cha kulaaniwa, na cha kushangaza, na cha kuzomewa, na cha kulaumiwa katika mataifa yote nilikowafukuza.” Katika kifungu hiki wasiomskiza Bwana wamelaaniwa kwa hivyo wanaopata maradhi haya wamelaaniwa kutokana na kutofuata sheria zake.

Usemi huu ambao unakaribiana na imani ya *chira* katika jamii ya Waluo nchini Kenya ambayo huchukulia kuwa kutokana na matendo maovu ya nyuma, na mtu kutozingatia miiko ya jamii, mtu huyo hulaaniwa, na laana hii hujitokeza kupitia katika *chira* ugonjwa wa ajabu wenye kujitokeza kama upele na mtu kukonda na hatimaye kufa ni imani inayorudisha jamii nyuma na kukataa kuwajibika (Mwita 1993 na Parkin 1978).

✓ Katika kushadidia haya, kanisa nalo halikuachwa nyuma katika kuongeza unyanyapaa. Wakimnukuu Benjamin Nzimbi, waandishi wa habari wa gazeti la *Taifa Leo* (2006) waliripoti msamaha ulioombwa naye Nzimbi kwa niaba ya kanisa akisema kuwa mbinu zao za awali za kuwatenga waliougua maradhi ya UKIMWI na kuendeleza unyanyapaa na ubaguzi ulitokana na kutojua. Hii ni kwa kuwa hapo awali kanisa lilidhani kuwa maradhi haya yalikusishwa na watenda dhambi na kwa hiyo ilikuwa laana kutoka kwa Mungu.

Udhaifu huu wa binadamu wa kuumba UKIMWI kama laana au adhabu unapotosha ukweli wa kisayansi hasa pale wanajamii wanapoambukizwa bila kupenda kwa mfano watoto wanaozaliwa na virusi vya UKIMWI pamoja na wale wanaowekewa damu iliyoambukizwa. Imani hii ya kuona maradhi haya kama laana yanamfanya binadamu kutokuwa na wajibu wowote hasa kuhusiana na maswala ya ngono.

2.3 UKIMWI NI UGONJWA MPYA

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) UKIMWI umesawiriwa kama ugonjwa mpya. Omolo ambaye alikuwa jirani ya Ngoma na rafikiye Queen alipokwenda Arusha alimpeleka mamake Queen kwenda kumuuguzwa Queen. Queen alikuwa rafiki yake Omolo ambaye walijuana katika shughuli za kazi na mwishowe wakafanya mapenzi naye. Kwa hiyo Queen alipoanza kuugua alimwomba Omolo kumleta mamake amuuguze baada ya Mamudi (mfanyakazi wake Queen) kumjulisha kuwa alitaka kuwacha kazi. Walipotoka Arusha alimwambia dereva wake ampeleke mamake Queen hadi kwa Queen ndipo alipomfikisha aliona mapokezi yale pamoja na siha ya Queen na aliporudi ofisini alimripotia bosi wake akisema:

Lakini Boss, tuseme kweli, Yule Queen si amekumbwa na *ugonjwa huu mpya* usiokuwa na tiba? “Dereva alimuuliza Omolo “yawezezana hakuna mwenye uhakika lakini dalili zinaonyesha”.

“Mimi naona ule ni UKIMWI tu. Hakuna swali, mtu ukonde namna ile! Tena basi anakohoa sana. Yaelekea ana TB Yule!” (Mkufya, 2005:153).

Dereva aliyaona maradhi haya kama ugonjwa mpya usio na tiba kwa kuwa waliougua walikufa hata baada ya matibabu. Vilevile afya ya waliougua ilisinyaa na kuwa mbaya ikilinganishwa na hapo awali kama vile Queen alivyobadilika. Kutokana na maneno ya

dereva inaonekana kuwa maradhi haya yalichukuliwa na wanajamii kama yasiyo na tiba na mapya kwa kuwa yaliingia katika jamii miaka ya 1980.

Mawazo haya yanashadidiwa na wanajamii wengine ambao wanayaona maradhi haya kama yaliyo na chanzo chake ughaibuni. Baadhi ya wanajamii mfano wazungumzaji wa lahaja ya Lukabras wa jamii ya Luyha wana usemi unaochukulia maradhi haya kama yaliyoletwa na wazungu (Kobia, 2008).

Huu ni mfano wa baadhi ya semi zilizotumiwa kuyaashiria maradhi haya katika jamii ambayo ilionekana kutokuwa na ufahamu mkubwa wa maradhi haya. Hata hivyo, usemi wenyewe unawafanya wanajamii kutowajibika. Katika hali ya kutafuta lawama, wengi waliamini hayakuwa maradhi asili na hivyo hawakutilia maanani athari ya maradhi haya. Badala yake waliendelea na mienendo hatari ya kingono ambayo iliyafanya maradhi haya kuenea kwa kasi. Hivyo basi usemi kuwa ni ugonjwa mpya na kujaribu kusema kuwa ulitoka ughaibuni ni usemi ulioyafanya kuenea.

2.4 UKIMWI NI KIFO

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) UKIMWI umesawiriwa kama kifo. Ngoma, mumewe Tabu alikuwa na urafiki na Queen ambaye alikuwa amepata maradhi nyemelezi ya UKIMWI. Majirani zake pale kijijini Tandika walikuwa wamepata fununu hii na kwa hiyo, Tabu katika pita pita zake akakumbana na ujumbe huu. Mumewe alipokuja usiku

wa manane kutoka *Malaika Bar* walizozana naye. Katika ugomvi ule Ngoma aliamka na kumfuata mke wake sebuleni, kama anavyosema mwandishi:

Kwa hasira, Tabu alinyanyuka akaenda kabatini na kuchomoa kisu kutoka kwenye sinia iliyokuwa na vyombo vya jikoni. Akamkabili Ngoma huku anatoa onyo Kali, "Ninasema usiniguse!"

"Sikugusi Ma'Juma. Nataka tujadiliane!"

"Tujadiliane nini? Umeniua halafu wataka tujadiliane!" "Nani kakwambia una UKIMWI? "Ngoma aliuliza kwa sauti ya kumbebeleza. Ulevi wote ulikwishamtoka.

'Kila siku nimekuonya: acha! Acha! Hukunisikia, ulijiona rijali sana kuvamia kila mzoga wa kike uliokuta. Sasa umeniletea gonjwa. Eti tujadiliane! Nijadiliane na mtu ambaye hata sasa ananuka harufu ya uasherati!

Sauti ya Tabu ikaanza kukoroma kwa uchungu. Akaendelea kusema huku akilia, "Ngoma! Ngoma! Kwa nini *umenihukumu kifo*? Nimekukosea nini? Sikukuzalia watoto? Sikuwatunza wanao? Sikukufulia marundo ya nguo? Sikukupokea kitandani hata ukiwa unanuka harufu mbaya za pombe, sigara na majasho ya kilevi? Niambie! Niambie hata siku moja ambayo nilikukosea mpaka sasa nikastahili hukumu hii ya *kifo*? Kwa yote niliyokutendea hukumu ni *kifo*? Watoto utawafanya mayatima. Jamani, jamani nani atawalea wanangu nikifa? Ndugu zako mwenyewe unazijua roho zao mbaya. Tutamkabidhi nani watoto tukifa? (Mkufya, 2005: 27-28).

Kutokana na kifungu hiki ni wazi kuwa maradhi haya yanachukuliwa kama kifo. Tabu aliposikia kuwa Queen rafiki ya mume wake alikuwa akiagua maradhi nyemelezi ya UKIMWI aliona kuwa hakukuwa na kitu kingine ila kifo. Hiyo ndiyo sababu anamuuliza Ngoma kwa nini amemhukumu kifo. Kwake maradhi ya UKIMWI yalimfanya aliyeugua kufa moja kwa moja.

Mhusika mwingine ambaye anaona maradhi haya kama kifo ni Grace ambaye alikuwa dadake Tabu. Grace alipoambiwa na dadake kuwa kaambukizwa UKIMWI alipoenda kumtembelea alipata mawazo mengi sana kama anavyosema mwandishi:

Grace alijipa moyo kumsahau Omolo na mambo yake binafsi. Saa zilipita huku akizidi kuwaza. Alipoingia chumbani kwake ilikuwa saa mbili. Sasa ilikuwa saa nne. Alijihisi mwili wake umekuwa mzito. Alikuwa na njaa lakini hakuwa na hamu ya kula. Akabaki kuwazia kifo cha dada yake mpenzi. Kwa nini kifo? Mara nyingi alipokwenda kusali kanisani mchungaji alitamka, “Mshahara wa dhambi ni mauti” na watu waliamini kauli hiyo. Ni kweli wenye dhambi hufa. Grace akajiuliza: dada yake katenda dhambi gani? Ngoma alistahili adhabu hiyo ya kifo. Dada yake, je? Na watoto walikosa nini kustahili kuadhibiwa uyatima? Siyo kweli! Mauti siyo mshahara wa dhambi. Wema pia hufa sawasawa na waovu (Mkufya, 2005: 94).

Kwake Grace alipoambiwa na dadake kuwa alikuwa akiugua maradhi ya UKIMWI aliona kuwa maradhi yale yalikuwa kifo. Hilo lilikolezwa na usemi wa dini ulioshikilia kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. Grace aliona Ngoma (shemejiye) alistahili adhabu ile kutokana na usherati wake na kuitelekeza jamii yake lakini dadake Tabu hakustahili kwa kuwa hakufanya usherati na aliachiwa mzigo wa kulea familia na mumewe.

Usemi huu kuwa mshahara wa dhambi ni mauti ni mzuri katika kuifanya jamii kuambaa mienendo ambayo kulingana na utamaduni wake inabainishwa kama dhambi. Hata hivyo unaongeza unyanyapaa kwa kuwa Tabu (mkewe Ngoma) alikuwa mwanamke mwenye maadili. Je, twaweza kusema kuwa kufa kwake kunatokana na dhambi zake? La, aliambukizwa maradhi haya! Usemi huu kwa hiyo hauna msingi kwa kuwa unawafanya wanadamu wengine kuhisi kuwa wao ni watakatifu na kuwalimbikizia lawama wengi ambao wamejikuta katika hali hii bila kujitakia.

Vilevile katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007) tunaona maradhi haya yakisawiriwa kama kifo. Fumbwe alipoanza kuugua alitafuta matibabu katika hospitali mbalimbali.

Aliwaendea pia waganga bila kupata matibabu. Mwishowe aliamua kwenda katika hospitali iliyokuwa karibu na nyumbani kama anavyosema mwandishi:

Angaa huku ni karibu na nyumbani watu wake walisema “Lolote likitokea jamaa zake tuko karibu”. Wasichosema ni kuwa walikusudia mauko. Kila uchao huamka na wasiwasi wakitaraji kulakiwa na tanzia ya akraba yao huyu; mtu mwenye ugonjwa ambao hauna cha dawa wala kafara (*Omar, 2007: 175*).

Jamii haikutarajia chochote ila kifo chake Fumbwe. Baada ya kupelekwa kwa waganga na hospitali zote walizozijua waligundua haikuwa uchawi, yalikuwa maradhi yasiyo na tiba.

Usemi kuwa UKIMWI ni kifo ulitokana na kutokuwa na habari tosha za kuambukizwa, kusambaa na kujitunza. Na kwa sababu maradhi ya UKIMWI yaliingia Afrika Mashariki miaka ya 1980 jamii haikujua muda wa kupevuka kwa maradhi haya. Wengi waliokuwa wameugua mwishoni mwa miaka ya themanini walianza kufa kwa mfululizo miaka ya tisini. Tafiti zilizotolewa nazo zikaonyesha kuwa maradhi haya hayakuwa na dawa, tiba wala chanjo dhidi ya virusi vya ugonjwa huu mbaya. Wanajamii walianza kuzungumza kuwa UKIMWI ni kifo. Hili sasa likawa moja kati ya usemi uliotumiwa na wanajamii kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Usemi ambao uliyanyanyapaisha maradhi haya na kuyafanya kutisha zaidi.

Hata hivyo, katika kuyahusisha maradhi haya na dhana iliyo katika mazingira ya kawaida inaweza kuleta mwitikio unaotarajiwa kutoka kwa wanajamii. Hasa ikizingatiwa kuwa

binadamu anaogopa kifo. Kwa kuyaita maradhi haya “kifo” kunaweza kuwafanya wanajamii kutahadhari ili kuyaepuka.

Usemi kuwa UKIMWI ni kifo unalenga kuyaumba maradhi ya UKIMWI ili kuyapa maana inayoweza kuwaingia watu, nao wawe na mwitikio unaotarajiwa. Lakini baada ya utafiti wa kina kufanywa, na watu kufahamishwa na kufundishwa imekuja kubainika kuwa mtu anaweza kuishi kwa miaka mingi ikiwa atajitunza vizuri kwa kuzingatia lishe bora pamoja na kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Kwa mfano katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) tunayaona haya:

Dkt. Hans alikuwa anaitikia maelezo ya Tabu.

‘Vizuri, kuna mengine. Ukipima ukajua mapema kama kuna virusi, utajitahidi kuutunza mwili wako ili uweze kuishi zaidi kama una virusi. Utatumia maelekezo yetu ya lishe, matibabu ya maradhi ya kawaida na kutumia dawa za kupunguza kasi ya kuongezeka kwa virusi. Ukizitumia dawa hizo vizuri zitaongeza muda wako wa kuishi (Mkufya, 2005:186).

Kutokana na maelezo haya ya Dkt. Hans ni wazi kuwa jamii ilipiga hatua katika kubadilisha mawazo ya kuona maradhi haya kama kifo na kuondoa unyanyapaa uliohusishwa na maradhi haya.

2.5 UKIMWI NI MDUDU

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007) UKIMWI umesawiriwa kama mdudu. Kibibi (Mfanyakazi wa Fumbwe na Hatima) alikuwa ameketi ukumbini akiwa anabadilisha vituo kutafuta kipindi kizuri. Hakuona cha kumridhisha, ndipo mwisho akaangukia kipindi cha vibonzo kama anavyosema mwandishi:

Mhusika mkuu alikuwa kijana mmoja aliyeitwa Kala. Kibibi aliondoka kumpenda Kala kwa ujasiri wake. Alikuwa kijana mdogo lakini mwenye ari kuu. Kipindi cha wiki hii Kala alikabiliana na dudu moja lilokuwa na sura ya kutisha lilodhulumu wanadamu. Dudu lenyewe kubwa na lenye macho makubwa na miguu mingi. Lilikuwa likiwaua wanadamu wala halikushughulika na wanyama wengine. Ajabu ni kwamba liliwalenga watu waliolikaibia au waliokuwa kwenye njia liipitayo. Kala alijitokeza, akawa akabiliana nalo. Alilidunga kwa mikuki na mishale yenye sumu.

Dudu linapodungwa lilizima kama kwamba limekufa. Baada ya muda lilizinduka likawa kali zaidi. Si Kala wala wenzake, hakuna aliyeweza kulidhibiti dudu hilo mbuai. Maiti zilizagaa kila mahali kwenye mapito yake. Kala hakukata tamaa ila aliendelea kukabiliana nalo huku akiwashauri watu kuliambaa sana. Mwisho Kala alijitokeza na ziaka yenye mishale ya sumu. Akalipiga lile dudu. Lilizimia na mara hii lilionekana kuwezwa. Hata hivyo ghafla lilitaga yai ambalo punde liliangukiwa dudu jingine lenyewe.

Ajabu ya hili dudu, Kibibi alimaka “liliandama wanadamu tu! Tena wote waliolikaibia. Ukiwa mbali halishughuliki nawe. Lakini iweje watu wanajipeleka kwenye mauti? Wanaonywa hawasikii. Siku zote binadamu hukimbilia alikokatazwa (Omar, 2007: 62-63).

Kama yalivyo maradhi ya UKIMWI dudu hili liliwalenga wanajamii waliolikaibia. Kwa hiyo iwapo wanajamii wangeambaa mienendo inayoweza kuwatia katika janga hili hawangeyapata maradhi haya. Kutokana na kifungu hiki tunaona taswira ya mdudu anayeitatiza jamii kama yalivyo maradhi ya UKIMWI. Wanajamii walijaribu kutafuta suluhu la tatizo hili bila mafanikio. Hii inatokana na taswira ya mdudu ambaye alikuwa akidungwa badala ya kufa anabadilika na kuibuka kwa njia nyingine.

Vilevile pale hospitlini alikolazwa Fumbwe, kulikuwa na picha iliyoangikwa katika ukuta yenye mdudu aliyekuwa akila tufaha kama inavyojidhihirisha katika kifungu hiki:

Ukutani mlitundikwa karatasi na mabango yenye ujumbe tofauti tofauti kuhusu afya. Moja lilisema ‘Kinga yashinda tiba’; jingine likanadi

'Uvutaji Sigara Wadhuru afya yako'. Kubwa ya yote ni hilo bango kubwa lililonadi kwa wino mwekundu: "JIHADHARI!" lilikuwa na picha ya tufaha kubwa lililoiva kweli kweli. Lilionekana kama mtu kaliama upande mmoja. Tufaha lenyewe lilikuwa na mdudu aliyefanana na kiwavi amejitokeza katika sehemu iliyong'atwa. Dudu lenye macho makubwa, sura ya kutisha lakini limetabasamu. Kando ya picha ya tufaha pamechorwa picha za watu wawili. Mwanaume wa umri wa makamo. Wote wamelikodolea macho tufaha, walionekana kulimezea mate. Kando yao pamechorwa jichwa linalotisha likiwa limetoa macho na ulimi. Jichwa lenyewe si la Binadamu si la mnyama chini yake hayo maandishi "JIHADHARI!"(Omar, 2007: 181).

Taswira hii ya mdudu kulila tunda na hasa tufaha ni nzuri katika kuisisitizia jamii kuwa maradhi haya yalishika sehemu ambayo binadamu ameshindwa kujinasua nayo; sehemu ya ngono. Hata hivyo, tahadhari kuwa tufaha limeliwa na mdudu inaweka woga kwa wanajamii ili wajihadhari wakijua kuwa kitu chaweza kuonekana kizuri kama lilivyo tufaha na kumbe kimeliwa na mdudu: mtu anaweza kuwa na afya nzuri lakini ana virusi vya UKIMWI. Zaidi ya hayo picha za watu wa jinsia zote ni njia chanya katika kuonyesha jamii kuwa maradhi haya si ya kina mama hasa makahaba pekee kama ilivyokuwa imani ya awali bali ni maradhi yanayoambukizwa kwa jinsia zote.

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) UKIMWI pia umesawiriwa kama mdudu. Omolo jirani yake Ngoma alikuwa ametoka safarini. Usiku huo alikuwa amechoka sana kwa hiyo, akaona ataelekea *Malaika* kwa chakula chake cha jioni. Kama anavyosema mwandishi:

Usiku ulikwisha ingia. Kelele za watu na redio zilizofunguliwa kwa sauti kubwa zilisikika kutoka katika kila nyumba. Vicheko, mayowe ya watu wakifurahia maisha na wakati mwingine vilio vya watoto wakidai mahitaji mbalimbali ya kitoto; vyote viliupa mji uhai. Kila mmoja alijua la kwake, lakini kwa ujumla ikawa shamra-shamra za mji zilizomfanya mwenye

kutazama juujuu asione *mdudu* mbaya aliyekuwa anaila jamii ile polepole (Mkufya, 2005:154).

Tunaona jinsi wanajamii walivyoshughulika na maisha yao na kusahau kuwa kulikuwa na maradhi yaliyokuwa yanawaangamiza. Maradhi ambayo yalikuwa yamejificha na kuzidi kuwaangamiza kila siku kwa kuwa jamii iliendelea na mienendo iliyowafanya kuyapata. Taswira ya UKIMWI sawa na mdudu katika jamii huenda ilileta maana zaidi. Jina hili linakaribiana zaidi na ukweli wa kisayansi kuhusu virusi vya UKIMWI ikilinganishwa na usemi mwingine kama vile uchawi, laana au ugonjwa mpya.

Kwa kuwa dhana ya HIV kisayansi ilizungumzia “wadudu” wadogo sana walio katika jamii ya virusi, ni rahisi lugha ya kawaida kuongelea mdudu. Huenda usemi kuwa UKIMWI ni mdudu uliibuliwa na jamii ili kuleta taswira ya vile maradhi ya UKIMWI yanaila jamii polepole bila kujua. Kama vile funza au minyoo wanavyoweza kuingia kwenye mwili wa binadamu na kumwathiri polepole, ndivyo maradhi haya yalivyo. Kwa njia hii ilikuwa hatua kubwa katika kumwelimisha mwanajamii wa kawaida (Mutembei, 2009).

Kuumba UKIMWI kama mdudu kuliwawezesha wanajamii kupata taswira ya maradhi haya na kuyaona kama yanatokana na mdudu. Katika kufanya hivyo jina linapokelewa na jamii na watu wengi huelewa lisemwalo na kuwa na maitikio yanayotarajiwa.

2.6 UKIMWI NI JANGA

Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), janga ni tukio la hatari lisababishalo taabu na maafa. UKIMWI kuwa janga ni usemi unaotokana na athari ya maradhi ya UKIMWI kwa mgonjwa, familia, jamii na hata serikali. Athari hizi ni kama vile uyatima, umaskini, ukosefu wa fedha za kugharamia wanaougua kati ya mengine. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) kuna wahusika wengi wanaoyachukulia maradhi ya UKIMWI kama janga. Mamake Queen aliyeletwa na Omolo kuja kumuugua mwanawe Queen, alipofika kwake Queen walikuwa na mengi ya kuzungumza na mtoto wake kama inavyobainika:

Queen hakupenda kumweleza mama yake waziwazi kuhusu maradhi yaliyomsibu. Waliendelea tu kusalimiana, Queen akiuliza habari za ndugu zake huko Arusha na habari za marafiki alioachana nao zamani. Mara aambiwa fulani hayupo, kahamia mji fulani, mara aambiwa mwingine kaolewa, mara nyingine aliambiwa fulani na fulani wamekwisha kufa. Baadhi ya vifo hivyo vilitokana na UKIMWI. Lakini, pamoja na yote hayo, donda kuu lilikuwa linamla moyoni ni maradhi gani aliyokuwa anaugua mwanawe? Nafsi yake ilikataa na iliogopa kukisia ugonjwa aliokuwa nao binti yake mzuri. Kila alipokumbuka vifo vya vijana wa kiume na wa kike wa rika la Queen, ambavyo vilitokea kijijini kwao, hofu kuu ilimwingia kwani kuugua kwao kulifanana sana na kuugua kwa Queen (Mkufya, 2005: 165-166).

Vifo vingi vilivyotokea kule vijijini vilisababishwa na maradhi ya UKIMWI na kumfanya mamake Queen kumhofia mtoto wake kwa kuwa afya yake ilikuwa imesinyaa. Wahusika katika riwaya hii wanaokufa kutokana na maradhi ya UKIMWI ni kama vile: Queen, Ngoma, Asha, Tabu na Chiku (japo hatuambiwi kama alikufa kuna habari kuwa kapata maradhi ya UKIMWI na mwishowe alipelekwa nyumbani kwao). Hii ndiyo ilikuwa athari ya maradhi haya. Maradhi haya mwanzoni yalidhaniwa kuwa ya makundi

fulani lakini sasa mawazo hayo yalifutiliwa mbali na athari yake. UKIMWI uliingia kila mahali. Kwenye ndoa, mfano kati ya Ngoma na Tabu, rafikiye Asha ambaye alikuwa akiendesha gari la masafa marefu pia aliyapata kutoka kwake Asha na kumpelekea mkewe ambaye pia japo hatukuambiwa lazima alikufa.

Athari nyingine iliyoyafanya maradhi haya kuitwa janga ni idadi kubwa ya mayatima walioachwa baada ya wazazi wao kufa kama inavyoonekana katika kifungu hiki:

“Nasikia kaka yake marehemu pia ameshafariki?” Omolo aliuliza “Ndiyo UKIMWI huo huo, na mke wake akamfuata, wakaacha mtoto huyo Dadii. Kwenye familia alikuwa amebaki Queen tu, na mama yake alimtegemea sana. (Mkufya, 2005: 182)

Dadii, mpwa wake Queen, pia alibaki yatima baada ya wazazi wake kufa. Wengine ni kama wanawe Ngoma na Tabu na watoto wake Msafiri. Huu ulionekana kuwa mzigo mkubwa katika jamii hasa ikizingatiwa kuwa watoto hawa ni wachanga na wanahitaji chakula, mavazi, malazi na masomo.

Katika kushadidia maoni haya, UKIMWI ulitangazwa kuwa janga na rais Daniel Arap Moi wa taifa la Kenya mwaka wa 1999. Hii ilitokana na idadi ya vifo, uyatima, gharama kubwa kwa serikali ya kutibu waliogua. Maradhi ambayo mwanzoni yalizungumziwa kwa sauti ya chini sasa yakaanza kutangazwa hata watoto wakayajua na kuogopa athari zake. Kwa mfano:

Juma hakupenda kabisa kuamini kwamba janga lile alizoea kusikia hatari zake kama hadithi redioni, kwenye magazeti, televisheni, sasa limepiga hodi katika familia yao, aliyelileta ni baba! Kamletea mama yao mpenzi maradhi hayo yasiyo na tiba (Mkufya, 2005:16).

Juma, mwanawe Tabu na Ngoma, aliyajua maradhi haya kwenye vyombo vya habari kama janga lakini sasa janga lenyewe lilikuwa limeingia katika familia yao.

Mwanzoni wanajamii hawakujua yalikuwa maradhi yapi wala yalienea vipi. Hivyo basi jamii ilikuwa ikiendelea na desturi na tamaduni zilizokuwepo kama vile kuwarithi wajane, kutumia sindano hospitalini bila makini yoyote na kufanya ngono za kiholela. Vyombo vya habari vilichukua nafasi kubwa katika kuuhamasisha umma kuhusu maradhi ya UKIMWI ambayo yalikuwa janga.

Kuyaona maradhi ya UKIMWI kama janga ni usemi “unaoeleweka” na imechukua nafasi ya saratani ambayo awali ndiyo maradhi yaliyotisha. Sontag (1989) anasema jambo moja muhimu kuhusu “janga” ni kuwa limetoka mahali tofauti. Kulingana naye UKIMWI ulitoka barani Afrika na ukaenea katika mabara ya Magharibi. Kwa kuwa maradhi haya yanaambukizwa kupitia kwa ngono, uwiano kutoka kwa janga na adhabu unapatikana kwa urahisi.

Mawazo haya ya Sontag yanaonyesha jinsi wanajamii wanavyojaribu kulaumiana. Wengine wakisema ulianza Afrika nao wengine ulianza Magharibi hata hivyo janga lenyewe limeathiri jamii kwa jumla. Kwa hiyo, usemi kuwa ni janga au baa unaafiki ukweli wa maradhi ya UKIMWI. Nchini Kenya kwa mfano baada ya miaka kumi, vifo vingi vilikuwa vimetokea katika maeneo ambayo UKIMWI ulichukuliwa kuwa uchawi

na baadhi ya wanajamii kufikiri kuwa ni ugonjwa wa watu maalum. Nyumba zilifungwa na mayatima kuachwa chini ya ulinzi wa ndugu na jamaa.

2.7 UKIMWI NI MWIBA

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) UKIMWI umesawiriwa kama mwiba. Ngoma alipofika nyumbani kutoka *Mwangaza Bar* ugomvi ulizuka baina yake na Tabu. Tabu alikuwa amekwisha pata fununu kuwa mume wake walikuwa marafiki na Queen na baada ya utafiti aliofanya ilikuwa wazi kuwa Ngoma kamletea UKIMWI. Ngoma alipofika nyumbani alipata Tabu amefunga mizigo yake tayari kurudi kwao. Jambo hili lilimtia mawazo mengi kama tunavyoambiwa na mwandishi:

UKIMWI! Kila alipofikiria neno hili, kitu kama mshale kilimchoma tumboni kwa nguvu. Alikwishawahi kusoma magazeti, vijitabu na vijarida vinavyoeleza habari za UKIMWI, Lakini wakati huo alizielewa habari hizo kama hadithi tu. Aliziona habari hizo kama zisizomhusu sana. Queen alikuwa mwanamke mzuri, msomi, mwenye afya, tena alikuwa anafanya kazi kwenye ofisi yenye hadhi kubwa. Wazo kwamba hata yeye angekuwa na UKIMWI lilikuwa mbali sana na fikra zake. Hata gharama na mifarakano iliyosababishwa na kumpata Queen alistahamili kwa sababu ya dhana yake kwamba alikuwa mwanamke adimu, wa kipekee, ambaye hangeweza kuhatarisha uhai wake kwa kuhusiana na wanaume wenye UKIMWI. Alijipa kichwa kwamba, ingawaje yeye hakuwa wa kwanza kumpata, lakini bila shaka hao wengine wote waliomtangulia hawakuwa na virusi vya UKIMWI. Sasa *mwiba* alioudharau ulikuwa umeanza kumwotesha tende, tende lisiloponyeka, tende la aibu, chungu, lililojaa lawama (Mkufya, 2005:33).

Ngoma alionekana kupuuzwa mawazo kuwa maradhi haya pia yaliweza kuwapata wanawake warembo hasa ikizingatiwa kuwa Queen alikuwa msomi na kumpata ilichukua gharama kubwa. Kulingana na Ngoma, maradhi haya sasa yamekuwa mwiba kwa sababu yatamfanya kuugua kwa aibu, uchungu na lawama kutoka kwa familia yake. Jambo

ambalo mke wake alimkanya lakini yeye akaona kuwa starehe yake ilikuwa kujifurahisha hata kama angemkasirisha mke wake kama inavyoonekana katika mfano:

Hoja hii ilimwandama Ngoma. Zamani alipopata pesa alidhani furaha ya maisha iko kwenye anasa hata kama akimkirihi mke wake. Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba. Kila alipogusa akakuta panachoma, alilala akiwaza, na usingizi ulimjia muda mrefu baada ya mke wake kulala. (Mkufya, 2005: 138).

Ngoma kupata UKIMWI, kunamfanya kuuona kwa jicho tofauti na kudengua mitazamo ya kijadi kuwa UKIMWI ni ugonjwa wa malaya. Hapa hata wanandoa ambao wana mienendo hatari wanaupata. Kuyaona maradhi ya UKIMWI kama ya kikundi fulani cha watu mfano malaya ni imani potovu hasa kutoka kwa mhusika Ngoma. Imani hii ambayo ilikuwa miongoni mwa wanajamii wakati maradhi ya UKIMWI yaligunduliwa ilifanya maradhi haya kuenea kwa kuwa wengi hawakutaka kuwajibika.

Omolo pia anayaona maradhi haya kama mwiba. Omolo alikuwa jirani yake Ngoma lakini walikuwa wanajuana na Queen kutokana na shughuli za kikazi. Omolo kama vile Ngoma alikuwa na wasiwasi mkubwa kwa kuwa alikuwa amefanya mapenzi na Queen na alihofia kuwa huenda alikuwa ameambukizwa kama anavyosema mwandishi:

Huu ulikuwa msimamo wake toka zamani. Aliutibua kwa kujenga uhusiano na Queen, akateleza, akakwama miguuni kwake, jambo lililozua wasiwasi katika nafsi yake. Wazo kwamba kugusana kwake na Queen kwaweza kuwa kumemwambukiza UKIMWI, lilikuwa doa kubwa na zito katika nafsi yake. Hakutaka kugusana na mwanamke na alipogusana na Queen kwa bahati akachomwa na mwiba wake. Sasa tena huyu Grace anazidi kumsogelea na mbinu zake zilikuwa ngumu mno kuzikwepa (Mkufya, 2005:152).

Omolo alikuwa na msimamo mkali tangu kukosewa na Mima. Mima alikuwa mwanafunzi mwenzake chuoni. Siku moja alienda kwenye chumba chake na kumfungua uchi wake akitaka kujua iwapo Omolo alikuwa amepashwa tohara. Tangu siku hiyo Omolo aliamua kutojijusisha na wanawake. Alipokuwa kazini walikutana na Queen ambaye alimhadaa na mwishowe wakafanya mapenzi naye. Japo walitumia mipira ya kondomu, mara ya pili mipira ulichanika na kumtia wasiwasi mkubwa akifikiri kuwa huenda aliambukizwa UKIMWI. Udhaifu wa Omolo ni kuona kuwa huu ulikuwa ni mwiba wa Queen. Jambo ambalo linatuonyesha kuwa wanaume wanayaona kama maradhi ya wanawake.

Hii inaonyesha ubaguzi na dhuluma dhidi ya wanawake kwa kuwa maradhi haya hayabagui jinsia yoyote ndiyo maana hata mataifa yaliyoendelea yanakabiliwa na maradhi haya. Kulingana na Omolo wanawake ndio mwiba wa kutahadhari. Dhana ambayo inaendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke.

Katika kushadidia haya, jamii nyingi Afrika zinatawaliwa na mfumo wa kuumeni. Chochote kibaya kinakuwa ni kwa ajili ya mwanamke. Hii ndiyo imani iliyotawala jamii tangu jadi ambayo pia inathibitishwa na tafiti za kisayansi. Utafiti uliofanywa na NACC (2005) ulionyesha kuwa, kutegemea jinsia, wanawake ndio walioathirika sana na maradhi ya UKIMWI. Huenda hii ndiyo sababu katika baadhi ya wanajamii kwa mfano Wamarama kutoka Magharibi mwa Kenya wana usemi kuwa UKIMWI ni maradhi ya wanawake (Kobia, 2008).

2.8 UKIMWI NI KUDURA

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) UKIMWI umesawiriwa kama kudra. Kulingana na TUKI (2004), neno kudura linatumika kidini kuonyesha nguvu au uwezo wa mwenyezi Mungu. Grace anaona kuwa dadake amepeta maradhi yale kutokana na nguvu za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, hakuna lolote ambalo wangetenda kuzuia nguvu hizo. Grace alipotoka kwa dada yake Tabu baada ya kumsimulia kisa kuwa alikuwa ameambukizwa UKIMWI na Ngoma, Grace alikuwa na mengi ya kujiuliza kama inavyodhihirika:

Kwa nini Mungu hakumwadhibu na kumzuia kabla ya kumdhuru dada yake? Kwa nini dada yake hakupata ishara ya kujiepusha naye? Uhalali gani wa *kudra* ile iliyomwangukia dada yake, kudra ambayo ndiyo maangamio yake? Lakini akaona kwamba maswali yake hayakusaidia lolote. Madhara yamekwishatokea. UKIMWI hauponyeki wala haupozwi kwa mtenda dhara kusema samahani (Mkufya, 2005:93)

Kulingana na Grace, huenda ilikuwa kudura. Kwake, dadake hakustahili kwa kuwa alikuwa amepata shida nyingi katika ndoa hasa ikizingatiwa kuwa mume wake alikuwa amemwachia jukumu lote la kulea watoto. Haya ni mawazo ya kukatisha tamaa kama wanavyoshikilia wanafalsafa wa Kidhanaishi. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), wadhanaishi wanasema kwamba kukata tamaa na mauti ni baadhi ya maudhui wanayoshikilia. Wao wanaamini kwamba mwisho wa mwanadamu ni kifo. Hivyo ndivyo Grace anavyofikiri kuhusu kuambukizwa kwa dadake: yeye anaona kupata maradhi ya UKIMWI ni kifo.

2.9 MWAMKO MPYA WA JAMII KUHUSU MARADHI YA UKIMWI

Baada ya muda wa miaka minne katika wakati hadithi, mawazo ya wanajamii yanabadilika kuhusu maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) tunaona mhusika Queen akizungumzia wazi maradhi ya UKIMWI pale anapomweleza Omolo kuhusu magonjwa nyemelezi ya UKIMWI kama inavyoonekana katika mfano huu:

Omolo alihisi harufu mbaya ya kwapa iliyochanganyika na lile jeraha.

“Umeumia na nini? “Alimuuliza na kuonyesha mshtuko usoni.

“Sijaumia. Hujawahi kuuona?”

“Kuona nini?”

“*Mkanda wa jeshi*,” Queen alisema na kumtazama Omolo usoni.

Queen akakohoa kidogo. Kikohozi chake kilikuwa kikavu sana. Akasaidia kumweleza Omolo, “Huu ni *mkanda wa jeshi*, ndivyo wanavyouta mitaani. Kitaalamu unaitwa *Shingles au Herpes Zoster*. Siku hizi unawapata watu wengi wanapoanza kuugua magonjwa nyemelezi ya UKIMWI (*Ua la Faraja*, 2005:63).

Queen anamwambia wazi Omolo kuwa anaugua maradhi ya UKIMWI. Kujitangaza wazi kwa umma kama vile mhusika Queen anavyosema ni maendeleo ya kiwango cha juu. Waathirika wanaposimama wa kutangaza hali yao wenyewe kunaondoa unyanyapaa. Ushupavu huu kwa kiasi kikubwa unaondoa imani potovu kuwa UKIMWI ni uchawi au laana kama ilivyochukuliwa awali na kupiga vita unyanyapaa. Katika kuyapa maradhi haya majina yasiyosheheneza hukumu, jamii inaonekana kujitengenezea njia ya kuanza kuyakubali maradhi ya UKIMWI na athari zake. Pia katika kuutania na kusema ni mwiba ni hatua kubwa ya kuyakubali japo pia inawafanya wanajamii wengine kutowajibika.

2.10 HITIMISHO

Sura hii ililenga kuchunguza usemi mbalimbali uliotumiwa na wanajamii kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI jamii imeibua usemi mbalimbali kama maradhi ya vikundi fulani ikiwemo malaya, madereva wa masafa marefu, askari na mabasha. Hata hivyo kuenea kwake pamoja na idadi ya vifo vilivyotokana na maradhi haya kulionyesha kuwa hayakuwa ya vikundi hivi pekee. Wanajamii nao walianza kuathirika. Usemi mbalimbali ulichipuka kuwa UKIMWI ni uchawi, laana baadaye jamii ilianza kuunyanyapaisha na kuyapa majina ambayo yanatisha na kuipa jamii mwendikio tofauti kama vile UKIMWI ni kifo na pia ni janga. Kwa wale ambao hawakuelewa maana ya usemi kuwa UKIMWI ni mdudu, ugonjwa mpya ulitumiwa kuyaashiria. Lakini, baada ya maradhi haya kuenea kutoka kwenye vikundi maalum na kuiathiri jamii nzima wanajamii walizua usemi wa kuyatania maradhi haya na kuonyesha ukubalifu. Hii ni njia chanya ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano, usemi kama UKIMWI ni mwiba unaonyesha kuwa yeyote anaweza kupata UKIMWI na hivyo kuionya jamii kujihadhari. Kutokana na usemi mbalimbali tunaona jamii ikiwa na hisia tofauti. Kwanza kwa kuunyanyapaisha na kisha baadaye kutumia usemi ulioonyesha mwendikio na ukubalifu wa maradhi ya UKIMWI. Sura itakayofuata itachunguza jinsi maradhi ya UKIMWI yanavyowaathiri wahusika na kuonyesha jinsi maradhi yanavyoweza kutumika kifasihi kuielewa jamii kwa jumla.

SURA YA TATU

ATHARI YA MARADHI YA UKIMWI KWA WAHUSIKA

3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tulichunguza usemi tofauti unaotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Baadhi ya usemi uliotumiwa ulionyesha hatua mbalimbali za maajilio ya maradhi haya, kuenea kwake na hata mwitikio wa wanajamii baada ya muda. Katika sura hii tutachunguza jinsi maradhi ya UKIMWI yanavyowaathiri wahusika. Nadharia itakayoongoza mtafiti katika kutimiza lengo hili ni ile ya Naratolojia. Mhimili utakaoshirikishwa ni ule unaoangalia wahusika kama kipengele muhimu katika masimulizi. Kulingana na nadharia ya Naratolojia, wahusika ni kipengele muhimu cha matini ya kifasihi. Wahusika huchunguzwa kutokana na viashiria mbalimbali. Tunaweza kutoa maelezo ya waziwazi kuwahusu au kuchunguza matendo, maneno, sura, mazingira, mandhari na hali yao kati ya mengine.

Manfred (2005) anasema kuwa, kuna mambo kadha mahakiki anaweza kuangazia anapochunguza wahusika. Anaweza kuchunguza iwapo sifa za wahusika zinaashiriwa kutokana na maneno au kuashiriwa na tabia zao, vilevile anaweza kuchunguza iwapo mhusika huyo anaonyesha sifa zake au anaashiria tabia za wahusika wengine. Sura hii inalenga kuchunguza namna maradhi ya UKIMWI yanavyowaathiri wahusika na kuonyesha jinsi maradhi yanavyoweza kutumiwa kuielewa jamii kwa jumla. Kutokana na maradhi ya UKIMWI tunaona wahusika wakiathirika kwa njia tofauti, kuna wale

wanaoathirika moja kwa moja na kuna wale wanaopata athari ya maradhi haya kupitia kwa wahusika wengine. Sehemu itakayofuata itachunguza athari hizo.

3.1 UNYANYAPAA

Unyanyapaa ni chuki, mitazamo hasi na dhuluma wanayofanyiwa wanaogua maradhi ya UKIMWI. Matokea yake ni kutengwa na familia, wanarika na jamii kwa jumla, kutohudumiwa vyema katika vituo vya afya, mazingira ya shuleni, kunyimwa haki, kuathirika kimawazo mambo yanayochangia pakubwa katika kutinga hatua za matibabu.

Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunamwona Tabu akimkaripia mume wake Ngoma kwa kumuambukiza maradhi ya UKIMWI ambayo kwake yalilingana na kifo kama tunavyoelezwa na mwandishi:

Niambie! Niambie hata siku moja ambayo nilikukosea mpaka sasa nikastahili hukumu hii ya kifo? Kwa yote niliyokutendea malipo ni kifo! (Mkufya, 2005:28).

Kwake Tabu maradhi yale ya UKIMWI yaliweza kulinganishwa na kifo. Grace (dadake Tabu) pia aliona kuwa hakuna kitu kingine ambacho dadake alikuwa akisubiri ila kifo.

Kwa kuambukizwa UKIMWI, Ngoma alikuwa amemhukumu dadake kifo kama anavyosema mwandishi:

Akabaki kuwazia kifo, kifo cha dada yake mpenzi. Kwa nini kifo? Mara nyingi alipokwenda kusali kanisani mchungaji alitamka, “mshahara wa dhambi ni mauti”. Na watu waliamini kauli hiyo. Ni kweli wenye dhambi hufa. Grace akajiuliza; dada yake katenda dhambi gani? Ngoma aliistahili adhabu hiyo ya kifo. Dada yake, je? (Mkufya, 2005:94).

Katika kuona maradhi haya kama kifo ni usemi unaoyanyanyapaisha maradhi haya na kuyafanya kutisha. Waliougua hukata tamaa na kuwafanya kutotafuta matibabu. Hilo

halikutosha, wanajamii pia waliwahukumu waliougua. Katika kuyaita maradhi haya kifo kunafanya jamii kuwaogopa walio na maradhi haya, kuwatenga na kuwadhulumu wanajamii.

Kulingana na Fairclough (1999), lugha inaweza kutumiwa na wanajamii wengine kuwadhibiti wengine kwa kuwa urazini ni hatua ya kwanza katika kujikomboa. Lugha inaweza kutumika kutenda mambo mengi. Baadhi ya mambo haya ni kama kuhukumu, kukemea, kuwaweka wanajamii katika matabaka kati ya mengine. Maradhi ya UKIMWI yameifanya jamii kutumia lugha kujenga unyanyapaa. Unyanyapaa huu unatokana na usemi tofauti unaotumiwa kuyaita maradhi haya kama vile: kifo, laana, uchawi, mdudu kati ya mengine.

Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunaona wanajamii wakiwatenga waliougua na kutotaka kuwahudumia. Kwa mfano, Mamudi ambaye alikuwa mfanyakazi wake Queen alipoona kuwa Queen alikuwa akikohoa na kutoa makohozi aliwaza ifuatavyo:

Haya ni makohozi, je atakapoanza kuharisha na kutapika nitafanyaje?
Aheri niondoke kabla mambo hayajazidi kuharibika (Mkufya, 2005:139)

Mamudi anaona heri awache kazi kwa kuwa hawezi kupenda kumuugua Queen kwa kuwa anajua anaogua UKIMWI. Haya ni baadhi ya mambo wanayofanyiwa wanaogua maradhi ya UKIMWI. Hakuna anayetaka kuwaugua, kwa hiyo mzigo wenyewe unarudia jamaa ya anayeugua. Unyanyapaa huu tunaona unavyowaathiri wahusika wengine. Kwa mfano, Queen anaamua kujiua ili asiteseke na kutengwa au kumtesa

mamake kwa kumuuguza. Mbali na kutengwa, kuna chuki. Wanaougua huchukiwa badala ya kuonyeshwa mapenzi. Kwa mfano wanawe Ngoma walipogundua kuwa mama yao kaambukizwa virusi vya UKIMWI walimchukia baba yao. Grace pia alimchukia Ngoma, Omolo naye alionyesha chuki na kumlaani Ngoma sana. Ngoma alikuwa akijiugua mwenyewe hadi pale alipopelekwa hospitali na Omolo na Grace. Alipoenda hospitali wauguzi hawakutaka kuwahudumia wagonjwa hawa ila tu pale mgonjwa alipoonekana kuwa na pesa za kuwahonga ili wamhudumie.

Kuvunjika kwa ndoa pia kunatokana na unyanyapaa kwa mfano ndoa kati ya Tabu na Ngoma ni mfano wa ndoa inayovunjika katika riwaya ya Mkufya (2005). Kabla kuolewa, Tabu alikuwa Mkristo. Baada ya kupendana na Ngoma ambaye alikuwa muumini wa dini ya Kiislamu, Tabu analazimika kubadili dini yake ili walee watoto wao katika mafundisho ya dini ya Kiislamu kwa kuwa hii ni jamii yenye ubabedume na kwa hivyo ni matakwa yao ndiyo yalifuatwa. Hata hivyo baada ya Ngoma kupata UKIMWI na kumwambukiza Tabu, ndoa ile ilionekana kukosa uaminifu. Baada ya habari kuwa Ngoma amemwambukiza UKIMWI, ndoa ile ilikuwa na mtafaruku. Tabu aliamua kurudia dini yake naye Ngoma alipoona hilo, ikawa vigumu kuishi na mkewe. Mwishowe Ngoma alimtaliki Tabu. Tabu alirudi kwao kama tunavyoona katika kifungu hiki:

Ilikuwa yapata mwaka mmoja na nusu tangu mke wa Ngoma kupewa talaka na kurudi kwa wazazi wake (Mkufya, 2005:213).

Japo kuvunjika kwa ndoa kati ya Ngoma na Tabu kulichangiwa na mambo mengi, sababu kuu ilikuwa maradhi ya UKIMWI.

Katika riwaya ya Omar (2007), Fumbwe alipoanza kuugua tunaona namna familia yake ilivyomtenga. Hapo awali kabla kuugua kwake aliwasaidia sana ndugu zake na wazazi wake. Alikumbuka jinsi alivyomfaa nduguye Kimini. Lakini alipougua na kwenda hospitali tunamwona jinsi alivyokuwa mpweke. Hakuwa na mtu hata wa kwenda kumwona. Anasema:

Mpweke ajabu. Hana mtu! Katelekezwa na kila mtu. Mke aliyekuwa naye ndiye huyo alishakwenda zake kitambo.

“maisha ajabu,” alijiambia huku akisonya. “Mimi huyu hapa wala sina anayenitaka sasa. Si ajabu jamaa wanaomba niondoke mapema ili wapate kurithi. Fadhila fadhili mbuzi binadamu atakuudhi! (Omar, 2007:176).

Fumbwe anatengwa na jamaa yake. Hakuna anayetaka kumkaribia kwa kuwa anaugua maradhi yasiyo na tiba. Wanajamii wake wanangoja afe warithi mali yake. Hivi ndivyo jamii inavyowaambaa wanaougua maradhi ya UKIMWI na kuzidi kukoleza makali yake, wanatengwa na kukosa tumaini, wanahisi hawahitajiki.

Katika kushadidia kauli hii, utafiti uliofanywa na United Nations (2004), ulionyesha kuwa wanawake ndio walioathirika zaidi kutokana na maradhi ya UKIMWI. Kulingana na shirika la UNFPA, yeyote anayewaambia wanawake wajiepushe na kutumia mipira ya kondomu wanapuuzwa ukweli uliopo katika jamii. Kujiepusha na ngono hakumaanishi chochote kwa mwanamke ambaye mumewe si mwaminifu na mipira ya kondomu haisaidii mwanamke chochote hasa anapozingirwa na umaskini na kuwa katika uhusiano wenye dhuluma hasa ikizingatiwa kuwa mifumo ya jamii za Kiafrika ni ya kuumeni. Vilevile, Okoth (2006) anasema kuwa, jinsia iliyoathirika zaidi kutokana na makali ya

UKIMWI ni ya kike: katika shughuli za kiuchumi na kijamii wanawake ndio walioathirika zaidi ikizingatiwa kuwa wao ndio huwauguza waathiriwa. Hii inawafanya kutojihusisha katika shughuli za kilimo, malezi au biashara. Matokeo yake ni ongezeko la umaskini, ukosefu wa chakula, utapia mlo na kuzorota kwa afya pamoja na kuwatoa wasichana shuleni ili kuwalea wengine. Kulingana na AVERT shirika la Uingereza linaloshughulika kutoa habari za UKIMWI nchini Afrika, unyanyapaa na ubaguzi unaotokana na UKIMWI ni kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya UKIMWI hasa inapowahusu wanawake.

Kutokana na maoni haya, unyanyapaa upo zaidi miongoni mwa wanawake ikilinganishwa na wanaume. Hata hivyo katika riwaya hizi, unyanyapaa unawaathiri wahusika wa jinsia zote; Tabu, Fumbwe, Ngoma na Queen. Labda msimulizi anajaribu kudengua mitazamo ambayo imekuwepo tangu jadi kuwa unyanyapaa upo miongoni mwa jinsia ya kike pekee ili kuonyesha kuwa hata mahali wahusika wa kiume wameathirika, unyanyapaa pia upo.

Unyanyapaa umeathiri vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Kuanzia kwa kuwatenga walioathiriwa, kuwaita majina tofauti pamoja na kuyapa maradhi haya majina anuwai na kuwahukumu waathiriwa. Hizi ndizo baadhi ya athari zinazotokana na unyanyapaa ambao unaongeza pingamizi dhidi ya vita vya kuyakabili maradhi ya UKIMWI. Kama anavyoongeza Sontag (1989) kuwa vifo vingi vya wanaouguua maradhi ya UKIMWI vinatokana na usemi unaotumia wala si maradhi yenyewe.

Katika kiwango cha taifa, unyanyapaa unaotokana na UKIMWI unazuia serikali kuchukua hatua zinazofaa na za haraka katika kukabiliana na maradhi haya. Katika kiwango cha mtu binafsi, unyanyapaa unaweza kumzuia kupimwa na kutafuta matibabu.

Unyanyapaa huu unaotokana na sababu kuwa ni maradhi yanayotishia uhai wa binadamu, unahusishwa na mienendo mibaya ya jamii kama uasherati, ushoga matumizi ya dawa za kulevya, ngono ambayo jamii inaona kama utovu wa maadili. Asasi za kidini pia awali ziliona kuwa kuambukizwa UKIMWI kulitokana na mienendo mibaya na kwa hiyo kupata UKIMWI ilikuwa adhabu.

3.2 UYATIMA

Athari nyingine inayokabili wanajamii kutokana na UKIMWI ni uyatima. Kulingana na utafiti uliofanywa na AVERT (2009), idadi ya mayatima katika nchi nyingi za Afrika ni zaidi ya milioni . Katika nchi nyingine, mayatima wanaotokana na maradhi ya UKIMWI wanajumlisha nusu ya mayatima wote au zaidi. Kwa mfano, nchini Kenya idadi ya mayatima wanaotokana na UKIMWI ilikuwa 1,200, 000 mwaka wa 2009, nchini Uganda ilikuwa 1,200, 000 na nchini Tanzania ilikuwa 1,300, 000. Wazazi wengi wanaogua UKIMWI wakifa huwaacha watoto wadogo kufanya majukumu ya watu wazima. Watoto hawa wanapoachwa hulazimika kuacha shule ili kutafuta riziki ya kukidhi mahitaji ya familia iliyoachwa. Watoto wengine hasa wa kike wakati mwingine hujikuta wamejiingiza katika maisha ya ukahaba ili kupata riziki na hivyo kuendeleza athari ya maradhi ya UKIMWI.

Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunaona kuna watoto wengi ambao wanabaki mayatima kutokana na vifo vya wazazi wao. Kwa mfano, Dadii ni mtoto aliyebaki katika familia yao baada ya kufariki kwa baba na mama. Hii ndiyo taswira ambayo inapatikana katika jamii kutokana na athari za UKIMWI. Huyu alikuwa mtoto mdogo ambaye hangeweza kujilea kwa hivyo inabidi wazazi wa waliokufa kuingilia kati ili kusaidia katika ulezi wa watoto hawa. Mamake Queen ndiye aliyebaki kuwajibika kama anavyosema mwandishi:

“Nasikia kakake marehemu pia ameshafariki? Omolo aliuliza.

“Ndiyo, UKIMWI huo huo, na mke wake akamfuata, wakaacha mtoto huyo Dadii (Mkufya, 2005: 182).

Mbali na Dadii, Tabu na Ngoma walipofariki waliwaacha watoto wao. Juma ambaye alikuwa mkubwa alilazimika kukatiza masomo yake ili atafute kibarua asaidie katika kuwalea wadogo zake. Katika riwaya ya Mkufya (2005), Juma ni mfano wa yatima ambaye analazimika kuacha shule na kutafuta ajira ili kuwelea wadogo zake kama invyodhihirika:

Sifa hii ilimfurahisha kwani mwanzoni msimamizi alimlaumu kwa kuajiri kijana mara tu baada ya kumaliza shule ya msingi (Mkufya, 2005: 235).

Juma alilazimika kuacha shule ili amsaidie mamake kutafuta riziki baada ya babake kumtaliki mamake. Umri wake ulikuwa mdogo lakini kulikuwa na haja ya kutafuta riziki ili kumsaidia mamake. Hata hivyo vifo vya wazazi wake wote vilimlazimu kuwa na mzigo mkubwa wa kuilea familia ndipo Omolo anamkumbusha kuwa kulikuwa na haja ya kumrudia babake na kuomba msamaha ili arithi mali ile iwasaidie pamoja na wadogo zake. Anasema:

”Ndiyo. Lakini pia ujue kwamba wadogo zako wanakutegemea wewe baada ya wazazi wako kufariki. Hutakuwa na kipato cha kuweza kugharamia maisha yako, ya kwao, shule mavazi na chakula (Mkufya, 2005: 237).

Juma anatahadharishwa na Omolo kuwa ana jukumu la kulea kwa hiyo kuna haja ya kumwomba babake msamaha ili amrithishe mali ile iwasaidie pamoja na wadogo zake kukidhi mahitaji yao. Kuhusu urithi wa mali ya wazazi waliokufa, tunaona jamii imepiga hatua kwa kuandika wosia. Hivyo wanajamii wenye pupa ya kuwanyang’anya mayatima mali yao wanakosa nafasi. Kwa mfano, Queen anamwandikia Dadii wosia wa kurithi nyumba yake. Labda kwa kuwa Queen alikuwa mwanasheria alijua haja ya kuandika wosia ule. Ngoma naye alipata marafiki wazuri ambao walimpa mawaidha ya kuwarithisha wanawe kwa kuandika wosia. Ngoma alipokuwa akiugua hakuna ndugu zake waliomkaribia. Lakini baada ya kufa tunawaona wakitaka kujua jinsi mali ya marehemu itakavyorithiwa. Kwa mfano:

“Twasikia marehemu alikuachia wosia?” Kassim alimuuliza mara baada ya utambulisho.

“Ndiyo”, Omolo alimjibu.

“Unao hapa? Mashaka aliuliza.

“Hapana”.

“Waweza kuupata kesho baada ya mazishi?” Mashaka aliuliza.

“Maelekezo ya marehemu ni kwamba wosia huo usomwe mahakamani mbele ya shehe Rajabu, Mama Juma, watoto wote na ndugu zake marehemu (Mkufya, 2005:299).

Wajomba zake walijaribu kumlazimisha awape wosia ili wausome pale kabla kwenda mahakamani. Lakini Omolo akasema kuwa hangeenda kinyume cha maelekezo ya marehemu kama inavyobainika:

Kassim akaanza kueleza, “Bwana Omolo, haya masuala ki-ukweli hayakuhusu. Ndugu tulikaa tukajadili suala la huo wosia. Tukaambiwa

wosia umepewa wewe. Sasa tunachotahadharisha ni kuacha ndugu tushughulikie mambo yetu wenyewe! Huo wosia sisi hatuutambui!” (Mkufya, 2005:299).

Wanajamii husubiri vifo vya wanaougua kwa ajili wao huchukua urithi ule wa mayatima na kuwalazimisha watoto hao kuondoka nyumbani na kuanza kujitafutia riziki. Wosia ulioandikwa uliwafaa kina Juma kwa kuwa wangenyang’anywa urithi na wajomba na shangazi zao ambao kifo cha Ngoma kilikuwa harusi kwao kwa kuwa wangechukua mali yake.

Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunaona kuna mradi ambao unaanzishwa kwa ajili ya kutetea mayatima kwa kulinda mali yao. Asha Mmanyema wakiwa na wifw wake Catherine aliyekuwa mdogo wa mume wake kutoka Australia walianzisha mradi wa mayatima ambao wazazi wao walifariki kutokana na maradhi ya UKIMWI. Mradi huu ulifaa kusimamia mali ya mayatima wa UKIMWI na kuwaelekeza jinsi ya kuendesha mali wanayoachiwa na wazazi wao. Hii ni njia chanya ya kuwaopoa mayatima hawa ambao wamezingirwa na jamii yenye uroho na ubinafsi tayari kuwadhulumu. Iwapo jamii inaweza kuiga mfano huu, mayatima hawa wanaweza kusaidiwa ili kuchunga mali wanayoachiwa iwasaidie katika kugharamia mahitaji yao wazazi wao wanapokufa.

Katika kushadidia haya Ghosh na Kalipeni (2004:304) wanasema, idadi kubwa ya watu wanaokufa kutokana na UKIMWI wamo katika umri wa kati ya miaka 15 na 49. Watu hawa wanapokufa huwaacha watoto. Kulingana nao uyatima ni kati ya athari kubwa ya maradhi ya UKIMWI unaokumba bara la Afrika ikizingatiwa kuwa watoto wengi

huwapoteza wazazi wote au mmoja kutokana na maradhi haya. Mayatima hawa hujikuta katika shida mbalimbali ikiwemo; unyanyapaa, utapia mlo, ukosefu wa mwongozo wa wazazi, ukosefu wa elimu na wengine hulazimika kutafuta ajira ili kujikimu. Wakati mwingine watoto hawa hujikuta wamepoteza urithi wao, kufukuzwa nyumbani na hata kujiunga na vikundi vya uhalifu.

Kama anavyoripoti Atieno (2002) jamii ya Afrika imepata wazazi wapya. Kina mama wazee wanawajibika kuwauguza watoto wao na pia kuwalea wajukuu wao kutokana na athari ya maradhi ya UKIMWI. Nafasi ya kulea inachukuliwa na wazee ambao wanachukua muda mwingi katika malezi na kuacha shughuli za kutafuta riziki na hivyo kuendeleza umaskini kama unavyodhihirika na maisha ya mamake Queen.

3.3 UTAMAUSHI

Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunaona jinsi mhusika alivyotamauka. Queen alipotambua kuwa alikuwa na maradhi ya UKIMWI. Queen ambaye alikuwa rafikiye Omolo alipata UKIMWI na kuanza kuugua maradhi nyemelezi. Queen alimkaribisha Omolo kwake baada ya kugundua eti amepata maradhi haya. Omolo alipokwenda kwake alimkuta Queen amedhoofika kiafya. Alionekana mchovu, kama mtu aliyetoka usingizini. Hata jinsi alivyojibwaga kwenye kochi alionekana kama mtu asiyejali tena, mtu aliyekata tamaa. Hata hivyo maoni ya Omolo hayakuwa mbali na ukweli uliokuwepo. Kwa hakika Queen mwenyewe alikuwa amekata tamaa. Hakuona faida ya maisha. Akiwa pamoja na

rafikiye Omolo walishikilia udhanaishi. Kwake yeye kuwepo katika ulimwengu huu hakukuwa na maana kama inavyodhihirika:

‘Uhai umekwisha’, alijisemea kwa sauti. Macho yake yaliangaza sebuleni, kwenye makochi, ukutani kwenye friji, yakasita kwenye picha yake alipotunukiwa shahada ya kwanza ya sheria. Hakika, pale alipendeza! Alikuwa kama ua la alizeti lililochanua kuonyesha nuru, neema na furaha iliyopamba uzuri wake. Sasa ua limenyauka laelekea kukauka. Kwa nini likauke? Kwa nini kwanza lichanue? Ndiyo nini sasa? Maana ya kuwa halafu kutokuwa ni nini? Macho yake yalizidi kuzunguka.

Wa nini mwili ule uliopenda kulishwa, kunyweshwa, kuonjeshwa vitu vizuri; mwili upendao kupapaswa, kukumbatiwa, kufanyiwa mapenzi ... wa nini mwili ule ufao? Oueen alijiuliza maswali hayo katika kutatanika kwake.

Alijitazama, akajichukia. Alichukua fahari yote aliyokuwa nayo huko nyuma, ambayo sasa ilikuwa inaelekea ukingoni (Mkufya, 2005: 66).

Queen alishangaa kwa nini afanye juhudi katika maisha kisha baada ya kufanikiwa afe? Yeye alishindwa kukabiliana na ukweli huu kuwa alikuwa na maradhi ya UKIMWI. Kwake UKIMWI ulikuwa kifo. Hakuona kuwa japo waweza kuwa na UKIMWI kulikuwa na njia ya kuyarefusha maisha labda kwa kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Yeye alikata tamaa; ‘Akakosa sababu ya kuishi. Anasema:

Adhabu gani hii? Alisema mwenyewe huku akila. Kweli aliyaona maisha ni adhabu: kuzaliwa, kuyaonja na kisha kuyanyang’anywa na kifo! Raha zote hazikuwa na maana tena. Zimepotea kwenye kumbukumbu yake. Kilichokuwemo kichwani mwake ni yale mawazo ya kuukaribia mwisho wake (Mkufya, 2005: 68).

Ukweli kuwa alikuwa afe ndio ulitawala maisha yake. Queen anasema kuwa hapo awali alipokuwa mtoto aliamini kwa dhati kuhusu Mungu ambaye sehemu yake iligeuka kuwa Yesu, akaja duniani kwa kuzaliwa na Bikira Mariamu, akafa kwa kusulubishwa

msalabani na baada ya siku tatu akarudi mbinguni. Lakini sasa imani hiyo aliiona kama hadithi nyingine alizosoma. Ila hofu aliyokuwa nayo ni kuwa baada ya kifo chake ingekuwa vipi? Anasema:

Baada ya kufa kwake itakuwaje? Hivi kuna maisha baada ya kifo? Kama yapo yale waliosimulia wakristo, basi ataishia kwenye moto wa milele. Lakini kama hadithi hiyo ya mbinguni na pepo ni uongo, mtu anakwenda wapi akifa? Ni kweli watu wakifa wanaisha na kupotea hivi hivi? Kuna umuhimu gani basi wa kuwepo kwa watu duniani? (Mkufya, 2005: 68).

Hivi ndivyo alivyotamauka na kukata tamaa ya maisha. Kwake alishindwa kukabiliana na unyanyapaa ulioyazingira maradhi ya UKIMWI. Afya ya Queen ilizidi kuwa mbaya. Baada ya miezi mitatu, jeraha waliloita *mkanda wa jeshi* lilipona baada ya matibabu ya muda mrefu hospitalini lakini sasa kifua kikuu ndicho kilichomsumbua. Alikohoa usiku kucha, wakati mwingine akitema makohozi yenye damu.

Mfanyakazi wake Mamudi alipoona Queen anatoa kikohozi cha damu alihofia namna angeishi naye atakapoanza kuharisha. Kwa hiyo, alitoa habari kwa mwajiri wake kuwa alikuwa anakusudia kuacha kazi. Hapo ndipo Queen aliamua kumpigia simu tena Omolo naye akaona heri aende kwa Queen. Ndipo katika mazungumzo yake na Omolo alimdokezea kuwa hakuona haja ya kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa kuwa maradhi aliyogua yalionekana kutokuwa na tiba. Omolo anamwambia:

Mtu hakati tamaa ya kuishi hadi dakika ya mwisho”
Omolo alimpa moyo. “Ah, si ujinga tu! Mimi kusema kweli, mama angeweza kuja nikampa maagizo yote na kumkabidhi nyumba najiondoa siku hiyo hiyo. Ninachosubiri ni yeye tu, aje tuagane”.
“Wewe Queen acha upuuzi? Wataka kujiua? Omolo alionyesha mshangao (Mkufya, 2005: 141).

Kwake hakuona tofauti kati ya kuishi miaka hamsini na miaka mia, au yule anayekufa leo na afaye kesho. Queen alitamauka. Akakosa maana ya maisha. Akaona hakukuwa na tofauti na yule aliyeishi siku chache na siku nyingi. Hatima ilikuwa kufa. Hakuna tofauti ya kuwepo na kutokuwepo. Mamake Queen alipoletwa na Omolo, Queen alimpa wosia wake. Baada ya hapo aliandaa karamu ndogo waliyosherehekea na mamake kisha usiku huo akameza vidonge zaidi vya usingizi akafa. Kama vile alivyokuwa mdhanaishi ndivyo alivyomaliza maisha yake. Wadhanaishi wanashikilia kwamba, mwisho wa mwanadanu ni kifo. Pamoja na haya udhanaishi unajadili hali kama vile fadhaa, mashaka, pekecho na uchovu na jinsi zinavyoathiri maisha ya binadamu. Hiyo ndiyo ilikuwa hatima ya Queen. Alijiua kama alivyoazimia.

3.4 UBADILISHAJI WA MIENENDO YA WAHUSIKA

Waandishi wa tamthilia futuhi kama ilivyo wale wa tanzia huchukulia mambo ya maisha yenye uzito kama vile ajali, ugonjwa, kifo ili kuyatumia kwa ajili ya ucheshi au majonzi katika kazi ya sanaa. Kulingana na Gorman (1993), mwandishi Jane Austen anatumia ugonjwa kuendeleza msuko wa kazi yake, kuwafafanua wahusika na kuwasilisha maudhui kwa wanajamii. Kulingana na Gorman, mwandishi Jane Austen alitumia maradhi katika kazi yake ili kuwabadilisha wahusika. Hawa ni wahusika wenye ubinafsi ambao kabla ya kuugua wanawadhulumu wanajamii wengine. Kwa mfano, anaweza kuwa katili kwa mke wake kwa kumpiga kila anaporudi nyumbani, kutowajibika katika kukidhi mahitaji ya familia yake na hata kuwa mlevi wa kupindukia. Kwa hiyo, mwandishi anaweza kumfanya mhusika huyu kupata maradhi ambayo hayana tiba au

yenye tiba akiwa na lengo la kuona jinsi maradhi haya yanavyoweza kumwathiri mhusika huyu. Kuna wahusika ambao huacha ubinafsi waliokuwa nao wakati wanapogundua kuwa wanaugua. Maradhi yao yanakuwa chanzo cha kuwabadilisha mienendo. Katika kuchunguza namna maradhi yanavyoweza kuwaathiri wahusika, msimulizi katika riwaya ya Mkufya (2005) anaonekana kufuata utaratibu wake Austen wakati maradhi yanamfanya mhusika kubadilisha tabia yake ya awali na kuwa mtu mzuri. Katika riwaya ya Mkufya (2005), mhusika Ngoma anabadilika kutokana na kuambukizwa maradhi ya UKIMWI kama anavyosema mwandishi:

Ngoma alikuwa tajiri. Alimiliki magari manne ya abiria pale kijijini. Kwa siku magari hayo yalimwingizia pesa nyingi. Lakini kila wakati Juma alimsikia mama yake akisema kuwa baba anajitahidi kuweka pesa ili anunue gari lingine. Alijua kwamba baba yake hunywa kuanzia bia sita na kuendelea ndipo aridhike. Bila shaka huwanunulia bia nyingi hao wanawake wa pembeni anaodaiwa kuwa nao. Sasa Juma alijiuliza, “Kama baba yake ana pesa nyingi za kulewa pombe, kwa nini mama yake anaishi maisha ya kimaskini?” (Mkufya, 2005:34).

Japo Ngoma alikuwa na pesa, Tabu na wanawe waliishi maisha ya kifukara. Tabu aliamua kufungua biashara ya genge ili imsaidie katika kukidhi mahitaji ya familia yake kwa kuwa, japo mume wake alikuwa tajiri, utajiri huo haukuwafaidi lolote. Si chakula si mavazi. Lakini punde tu Ngoma alipogundua kuwa Queen alikuwa anaugua maradhi ya UKIMWI alihofia kuwa huenda yeye pia alikuwa ameambukizwa. Ngoma ambaye alikuwa mlevi wa kupindukia, aliyekuwa akifika nyumbani usiku wa manane, alianza kubadilika. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Ngoma alikunywa chupa moja tu ya bia na kuondoka kurudi nyumbani kwake. Hakuwa na hamu ya kwenda popote baada ya habari zile.

Watoto na mke wake walishangaa kumwona baba amerudi mapema. Ngoma akamtuma binti yake, Asha, kwenye baa ya karibu kuleta bia na soda za kutosha wote pale nyumbani.

“Kumetokea nini leo ukarudi mapema?” Mke wake alimwuliza. Nuru, ambaye hakuwa amemzoea baba yake, alimsogelea kwa hadhari, ingawaje udadasi wa utoto ulivutiwa kumgusa mtu Yule (Mkufya, 2005:29)

Ngoma hangepatikana nyumbani kwake mapema. Alizitumia pesa zake kwa wanawake wake mtaani. Hata watoto wake walishangaa kuona baba yao anawanunulia soda na kufika nyumbani mapema. Haya ndiyo yalikuwa mabadiliko ya Ngoma punde aliposikia rafiki yake Queen anaugua maradhi yanayohusishwa na UKIMWI. Baadaye Ngoma aliacha kwenda kwenye baa, ikawa sasa pesa alizokuwa anapata kutoka kwenye biashara zake zinakuwa nyingi. Akajaribu kumwambia Tabu aache biashara yake ya genge kwa kuwa pesa alizokuwa akipata ziliwatosha. Tabu naye akashikilia kuwa alikuwa amezoea na hangewacha aketi bure. Nguo ambazo hakuwa akiwanunulia ila tu wakati wa sherehe sasa akawa yuanunua kila wakati hata wakashindwa kuvaa kwa kuwa walikuwa wamezoea maisha ya kifukara. Ngoma aliuacha ulevi na kushika dini kama inavyodhihirika katika kifungu hiki:

“Hiyo kazi ya genge mimi nimekuambia uiawache sasa, mbona bado umeikazania?” Ngoma alimwuliza mkewe huku na yeye akijihimu kuamka ajiandae kwenda msikitini.

Ngoma akaamua kunyamaza. Akaharakisha kupiga mswaki na kuchukua ndoo ya maji kwenda bafuni kutawadha. Baada ya hapo, akavalia kanzu yake na baraghashia akachukua tasbihi na kuelekea msikitini.

Mavazi yake, tasbihi na makabadhi, vilikuwa bado vipya kwani haukuwa muda mrefu tangu alipoamua kuacha ulevi na kufuatilia mambo ya ibada.

Mageuzi haya ya mume wake yalimkera sana Tabu kwani, kwa ulimbukeni wake wa imani, Ngoma alizua tabia ya kuanza kuwafundisha wenzake maadili mema na kujifanya mcha-Mungu (Mkufya, 2005:106).

anambaka Kibibi na kumpachika mimba baada ya kumlaghai kula tufaha. Kibibi analazimika kurudi kijijini baada ya tukio lile lakini babake anamfukuza. Kibibi anapokosa mahali pa kwenda anaamua kujiua. Kwa bahati nzuri anaokolewa na Ma'Asha. Kibibi anajifungua mtoto wa kiume na anampa jina Kala.

Kibibi anapojaribu kutafuta haki yake, anaambulia patupu pale anapogundua kuwa Fumbwe alikuwa na cheo katika Idara ya Ujasusi. Anajaribu kumpeleka Fumbwe kwa mawakili tofauti lakini Fumbwe anawahonga. Mwishowe Kibibi anaona aachane na Fumbwe – haki yake aliona atalipwa na Mungu. Ndoa ya Fumbwe nayo inavunjika baada ya kuwafumana Inspekta Chongea na Hatima. Baada ya hapo anaingia katika lindi la uasherati. Mwishowe anaanza kuugua maradhi ambayo hakujua iwapo yalikuwa uchawi au laana kama inavyodhihirika:

Alivuta nadhari kukumbuka aliyoyapitia. Watu walisema kwamba maradhi yale kajitakia kwa jinsi alivyoishi. Kwake yeye akiamini kaletewa na mtu. Ama kachomekwa mzizi au laana. Alikisia kuwa laana yenyewe ni ya kiumbe ambacho aliwahi kukibughudhi. Kiumbe ambacho hakikuwa na hatia. Alikumbuka jinsi kiumbe hicho kilivyomlilia kikitaka akinusuru, lakini yeye akajipa hamnazo akacheza alizotaka.

Maneno fulani yalivuma kichwani mwake kama kwamba kaambiwa jana, kauli ambazo zimekuwa donda ndugu moyoni mwake: *Malipo ni papa hapa duniani, Mimi sina uwezo wa kujitetea. Maskini hohe hahe hapa nilipo!* Mwenyewe kuyasema akitokwa na machozi. Umenitoa kwa wazazi wangu bila hiari. Umenipa kuazirika! InshaAllah Rabbi akupe kama haya tu. Nyumba uliyojenga uihame kama nilivyohama mimi (Omar, 2007:174).

Fumbwe bila kujua kuwa maradhi yale yalitokana na mienendo yake tunaona anavyofikiria kuwa ni uchawi au laana. Kinachomla Fumbwe ni kufikiria matendo

aliyomfanyia Kibibi. Kwake, anafikiri kuwa Kibibi alimroga kutokana na yale aliyomtendea. Fumbwe hakumbuki matendo yake ya uasherati. Kwake anaamini kuwa huo ni uchawi. Mhusika huyu hata hivyo anapata adhabu ya matendo yake pale anapoteseka na kufa mpweke kutokana na maradhi yanayonyanyapaishwa na jamii. Huu ni uadilifu wa kifasihi. Hakuna chema ambacho kingemfaa ila kupata adhabu ya tabia yake. Ubaya wake unalipwa kwa adhabu ya maradhi yenye kumfanya kutengwa akidhani kuwa ni kutokana na aliyomtendea Kibibi.

Mhusika mwingine ambaye anapata adhabu ya ubaya wake ni Ngoma katika riwaya ya Mkufya

(2005). Ngoma alikuwa mumewe Tabu. Alikuwa mwenye bidii katika kutafuta mali. Lakini tunaambiwa kuwa japo alikuwa na magari matatu ambayo yalimpa pesa nyingi, alitumia pesa hizo katika kujistarehesha na wanawake kama Queen na Asha na kuitelekeza familia yake kama anavyosema:

Nitamwambia nini Mungu nitakapofikishwa hukumuni? Nitajitetea kwa kushindwa kuilea familia yangu vyema na kumtumikia Mungu? Nitajitetea kwa kumnyima mke wangu matunzo, na badala yake riziki alizonipa Mungu nikazigawa kwa Malaya na kuzilewea pombe? Hivi karibuni nimejaribu kujirekebisha, lakini badala ya kupata shukrani kutoka kwa familia, nimeishia maudhi na karaha. Juma amenikimbia, watoto nikiwanunulia nguo hawazivai; mke wangu kutwa kucha hunililia akinilaumu na kunilaani. Nitamweleza nini Mungu kama mauti yatanifikia kesho au kesho kutwa? (Mkufya, 2005:164).

Ngoma ana majuto mengi kutokana na kuitelekeza familia yake. Tabu alilazimika kufungua biashara ya genge ili kulea aila yake. Mahitaji ya nyumbani yalikuwa nadra kupata kutoka kwa Ngoma, mavazi aliwanunulia wakati wa sherehe. Hata hivyo tunaona

msimulizi akimwadhibu mhusika huyu kwa kupata maradhi ya UKIMWI ambayo anaugua kwa dhiki hadi kufa. Kutokana na ubinafsi wake na kutowajibika, Ngoma anakufa kutokana na maradhi yanayohusishwa na unyanyapaa. Matokeo ni kutengwa na kuhukumiwa na jamii. Mwanawe Juma, anaona kuwa maradhi yale aliyopata babake alistahili kutokana na mienendo yake. Kuwa aliwafanya kuishi maisha ya kifukara na alikuwa na pesa kwa hiyo alistahili. Anasema:

“Boss hujanielewa. Baba kamuua mama yangu kwa kumwambukiza UKIMWI baada ya kumtesa na kumfanya aishi maisha ya dhiki wakati yeye ni tajiri. Hawezi kufuta uovu huo aliofanya kwa kunirithisha mimi mali zake! Nitamkosa mama kwa sababu yake.

“Usiseme hivyo Juma! Hata wewe waweza kupatwa na matatizo ukijakuwa mkubwa.”

“Na niadhibiwe vivyo hivyo! Kama nitafuata mwenendo huo wa baba nitastahili adabu kama hiyo hiyo aipatayo.”(Mkufya, 2007:237).

Watoto wake Ngoma walihisi uchungu mwingi kwa kuwa waliona mama yao aliambukizwa UKIMWI na baba yao na kuona baba yao alistahili adhabu hiyo kutokana na yale aliyokuwa akiwatendea.

Waandishi wa riwaya hizi wamefaulu katika kuipa fasihi nafasi yake ya kuadilisha jamii kwa kuwaadhibu wanaokosa. Hata hivyo mhusika kama Tabu japo si mkosa anajikuta anakufa kutokana na UKIMWI, huenda mwandishi anajaribu kuonyesha kudura ya mhusika huyu. Mhusika mwingine ambaye anaokolewa kutoka kwenye maradhi haya ni Omolo. Omolo alikuwa mhusika mwaminifu na aliwasaidia wengi. Alikuwa na pesa nyingi lakini hakuziharibu kwa wanawake. Alikuwa mwadilifu. Japo Omolo alifanya

mapenzi na Queen na mpira ukachanika aliepuka kuambukizwa. Labda anatumizwa kwa kuopushwa kutokana na wema wake.

3.6 UJASIRI

Maradhi ya UKIMWI yanawaathiri wahusika kwa njia tofauti. Katika riwaya ya Mkufya (2005), mhusika Queen anapogundua kuwa amepata UKIMWI anatamauka na kujiua. Hata hivyo msimulizi kwa upande mwingine anatuonyesha wahusika wengine ambao wanapopata maradhi haya hawafi moyo. Gorman (1993) anasema kuwa matumizi ya maradhi katika kazi ya fasihi huwa na lengo. Lengo hilo laweza kuwa ni kuonyesha hulka ya mhusika. Katika riwaya hii tunaona jinsi maradhi yanavyotumika kuwakuza wahusika wengine na kuonyesha ujasiri wao katika kukabiliana na maradhi.

Kuna wahusika ambao kutokana na nafasi yao katika jamii, wanaogopa kutangaza hali yao, pia hawawezi kunywa dawa zinazopunguza makali ya maradhi haya kwa kuhofia kile ambacho kitasemwa. Hata hivyo, katika riwaya ya Mkufya (2007), mhusika Tabu anaonyesha ukakamavu wake kwa kuchukua hatua ya kwenda kupimwa alipogundua kuwa mume wake alikuwa amemwambukiza UKIMWI. Hatua hii ya kupimiwa na kuwa na mwelekeo chanya inamfanya Tabu kurefusha maisha yake kutokana na mawaidha aliyopewa na Dkt. Hans kuhusu jinsi ya kuishi na maradhi ya UKIMWI ili arefushe maisha yake, awalee wana wake hadi pale atakapokufa.

Tofauti na Ngoma na Queen, Tabu ana mwitikio tofauti. Yeye aliamini kuwa kwa kutumia vidonge, kuacha mawazo na kula vyakula bora angeweza kuishi angalau kwa muda mrefu kutokana na kufuata maelekezo ya daktari. Hii inaonyesha ujasiri wa mhusika katika kukabiliana na hali ambayo wahusika wengine wameshindwa kuikubali. Tabu anaonekana kuvumilia unyanyapaa, aibu na shutuma zinazotokana na maradhi haya. Wakati Queen anajiua, baada ya miezi minne alipogundua ana UKIMWI, Ngoma na Asha wanamfuata Queen baada ya miaka minne lakini inachukua miaka miwili baada ya vifo vyao ndipo Tabu anafuata.

Huenda msimulizi anatumia mhusika Tabu kuonyesha kuwa inategemea mwitikio wetu kwa maradhi haya. Iwapo tutapiga vita unyanyapaa, waathiriwa wa UKIMWI wanaweza kuishi kwa muda mrefu. Tabu anawapa waathiriwa matumaini kuwa, inahitaji ukakamavu ili kuishi na maradhi haya. Dkt. Hans pamoja na mkewe Kristina, Grace, Omolo na jamaa yake Tabu na wanawe walichangia pakubwa katika kumpa Tabu matumaini kwa kuondoa unyanyapaa na kumwonyesha upendo.

3.7 UDHAIFU WA WANAJAMII

Mbali na kutumia ugonjwa kuendeleza msuko, maudhui na kuwakuza wahusika; maradhi yanaweza kutumika kuonyesha udhaifu wa jamii. Katika riwaya ya Mkufya (2005), udhaifu wenyewe unajitokeza kwa njia tofauti katika baadhi ya wahusika. Kama vile: ubinafsi na udaku. Kutokana na maradhi ya UKIMWI mwandishi anatuonyesha tabia za wahusika wengine. Wahusika ambao kwao mhusika anapougua inakuwa ni fursa ya

kuonyesha ubinafsi wao. Udhafu mwingine unaonyeshwa kutokana na miundo ya jamii inayoleta umaskini na kuwafanya wahusika kujikuta katika hali inayofanya maradhi ya UKIMWI kuenea.

Ongezeko la vijana kuhamia mjini kwa ajili ya kutafuta kazi ni njia mojawapo inayochangia kuenea kwa maradhi haya. Katika riwaya ya Mkufya (2005), tunawaona Pendo na Chiku ambao wameenda mjini kutafuta ajira ili kupata riziki. Kutokana na hali ngumu ya kiuchumi vijana hawa wanajikuta wakitafuta kazi katika sehemu za burudani (baa). Matokeo ni kutangamana na wanaume tofauti ili kununuliwa mishikaki, vileo na mwishowe ni kupata maradhi ya UKIMWI yanayowaua. Kwa mfano Chiku alikuwa rafikiye Pendo, walikuwa wakifanya kazi Malaika baa. Wateja wao walikuwa kina Omolo, Ngoma, Asha, Queen kati ya wengine. Omolo anasema:

Furaha aliyokuwa ameizoea *Malaika Bar* ilipungua baada ya kusikia Pendo na Chiku wamesimamishwa kazi baada ya kusababisha shoti kubwa ya pesa za mauzo. Baada ya kuacha kazi Malaika, Chiku aliajiriwa Kanga Moja club na Pendo akapata kazi kwenye baa nyingine iliyoitwa Altwan. Haikupita zaidi ya miezi miwili Chiku akaanza kuugua magonjwa mbalimbali. Hatimaye mwajiri wake akanwachisha kazi. Kulikuwa na tetesi kwamba alikumbwa na UKIMWI. Pendo aliendelea kufanya kazi Altwan.

Omolo hakuwa na habari zozote kama huko nako kaacha au la. Kulikuwa na habari za kuaminika kwamba wiki chache baadaye Chiku alirudishwa kwao Tabora akiwa amedhoofu sana. Omolo alipenda ajue habari zaidi kuhusu watani wake hao, lakini hakupata fursa ya kuwahoji waliozijua (Mkufya, 2005:203).

Wasichana hawa wanalazimika kufanya kazi kwenye baa kutokana na uhitaji. Mapato yale pia hayawatoshi na kuwafanya kuiba na kushiriki katika ukahaba. Matokeo yake ni kupata UKIMWI na mwishowe kufa. Kwa hivyo miundo ya kiuchumi ambayo

inawafanya wengine kuwa matajiri na wengine maskini inachangia pakubwa katika kuenea kwa maradhi ya UKIMWI.

Jambo lingine ambalo linajitokeza kama udhaifu wa jamii ni ubinafsi unaotokana na tamaa ya wanajamii ya kutaka kunufaika au kuhisi vizuri kwa kuwa wengine wamekufa. Hawa ni wahusika kama nduguze Ngoma ambao kifo chake ni nafasi kubwa ya kuchukua mali yake huku wakijidai kuwajali wanawe marehemu. Hili pia linajitokeza katika riwaya ya Omar (2007) ambapo Fumbwe ametelekezwa hospitalini kwa ajili ni mgonjwa na familia yake inangoja afe ili warithi mali yake.

Mbali na hilo, udaku unadhihirisha udhaifu wa jamii. Maradhi ya Queen yanapokelewa kwa furaha na wanawake ambao walimwonea wivu kutokana na cheo, kazi na urembo wake. Kwa mfano katika kifungu hiki:

Queen alikuwa mashuhuri mtaani kwa urembo wake, na pia kwamba alikuwa mwanamke pekee msomi, mwenye cheo kikubwa kazini kwake. Hivyo habari za kuugua kwake zilichukuliwa na wengi hasa wanawake kwa hisia za furaha iliyotokana na wivu na chuki dhidi yake (Mkufya, 2005:29).

Wanajamii hawa walimwonea wivu Queen kwa kuwa alikuwa msomi na mrembo kwa hivyo alipougua walifurahi na kumsema sana. Wanajamii hawa ndio wanaokoleza makali ya maradhi haya kwa kuyanyanyapaisha na kuwafanya walioathiriwa kuhofia kutafuta matibabu. Kwa hivyo, mbali na maradhi kuwaathiri wahusika moja kwa moja yanaweza kutumwia kuimulika jamii ili kujua tabia zao.

3.8 HITIMISHO

Sura hii ililenga kuchunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Unyanyapaa ulionekana kuwaathiri wahusika kwa kiasi kikubwa na kuwa kikwazo kikuu katika hatua za jamii, serikali na wanaoshughulikia UKIMWI katika juhudi za kukabiliana na maradhi haya. Hii inatokana na sababu kuwa maradhi haya yanahusishwa na ngono kwa hivyo walioambukizwa wanaonekana kuwa ni watenda dhambi. Jamii imeendelea kuwahukumu walioathiriwa na hivyo kuwayanyapaisha kiasi cha kukosa kutafuta hatua mwafaka za kukabiliana na maradhi haya. Tatizo lingine ni uyatima uliotokana na vifo vya waathiriwa. Mayatima hawa wameonekana kuwa mzigo mkubwa katika jamii ambayo tayari inakabiliana na hali ngumu za kiuchumi.

Kuna wale ambao wanaona kuwa kuambukizwa maradhi haya ni uadilifu wa kifasihi hasa ikizingatiwa kuwa wanaoathirika wanapata maradhi haya kutokana na mienendo mibaya na ubaya wao kama wahusika binafsi hivyo basi wanahitaji kuadhibiwa. Hawa ni wahusika kama Ngoma na Fumbwe. Pia tunaona kuwa wahusika wanabadilika kutokana na maradhi haya kama Ngoma. Hata hivyo katika kumsawiri Tabu kama mhusika jasiri anayeonekana kukabiliana na maradhi haya kunaonyesha kuwa kuna matumaini ya kukabiliana na UKIMWI. Jamii haijakata tamaa na huu ndio mwikio unaohitajika. Sura itakayofuata inalenga kuchunguza jinsi riwaya hizi zinavyoweza kutumiwa katika kukabiliana na maradhi haya kwa kuwapa matumaini walioathiriwa na kuwaonya wale ambao hawajaambukizwa dhidi ya mienendo inavyoweza kuwafanya kupata maradhi haya.

SURA YA NNE

MATUMIZI YA RIWAYA ZA *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha* KATIKA KUKABILIANA NA MARADHI YA UKIMWI NA CHANGAMOTO ZINAZOTOKEA

4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tulichunguza jinsi maradhi ya UKIMWI yanavyowaathiri wahusika katika riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Baadhi ya athari hizo ni kama unyanyapaa, uyatima, utamaushi na uadilifu wa kifasihi. Vilevile tuliona jinsi maradhi haya yanavyoweza kuwabadilisha wahusika na kuwafanya kuwa na utu pamoja na kuonyesha ujasiri wa wahusika wengine katika kukabiliana nayo. Maradhi ya UKIMWI pia yalitumiwa kuonyesha udhaifu wa wanajamii kwa mfano udaku kama tatizo linalotokana na athari ya maradhi haya.

Katika sura hii, tunachunguza jinsi riwaya hizi zinavyoweza kutumika katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI kwa kuwaonya wahusika dhidi ya mienendo inayoweza kuwafanya kuyapata na kuwahimiza walioambukizwa kwa kuwapa matumaini. Nadharia inayoongoza mtafiti katika kutimiza lengo hili ni ile ya Naratolojia na Matendo ya Usemi. Mhimili wa nadharia ya Naratolojia utakaotumika ni ule wa Mtazamo wa Msimulizi. Msimulizi kwa wakati wote huwa na dhamira au mwelekeo fulani ambao anakusudia msikilizaji au msomaji wake kujishirikisha nao. Katika uhakiki wa matini, Genette (1980) anasema ni vyema kuweza kutambua: ni nani anaona, nani anayewakilisha mtazamo wa msimulizi na nani anayezungumza. Kwa mujibu wa kauli

hii, mtazamo wa msimulizi umetuwezesha kuchunguza kusudi la masimulizi haya kama yenye lengo la kuonya wale ambao hawajapata maradhi haya kuepukana na mienendo inayoweza kuwaingiza katika janga hili, mbali na kupendekeza njia za kufanya mapenzi bila kuambukizwa. Vilevile mtazamo huo umetuwezesha kuona njia za kuwafariji walioathiriwa kwa kuwapa matumaini. Katika nadharia ya Matendo ya Usemi, mhimili uliotuwezesha kufanikisha lengo hili ni ule wa tendo la kusudio ambalo linanua kwamba masimulizi yafasiriwe kama yenye lengo la kuonya wale ambao hawajapata maradhi haya na kuwafariji walioathiriwa. Sehemu inayofuata inachunguza jinsi riwaya hizi zinavyoweza kutumiwa kukabiliana na maradhi ya UKIMWI.

4.1 MATUMIZI YA MIPIRA YA KONDOMU KATIKA RIWAYA YA *Ua la*

***Faraja* (2005)**

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) tunaona msimulizi akiangazia matumizi ya mipira ya kondomu kama njia nzuri ya kuepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Kama tunavyoambiwa na mwandishi kuwa Jose alikuwa anafanya kazi ya kuhamasisha watu kuhusu matumizi ya kondomu ndio maana aliitwa soksi. Kilichomshangaza Omolo ni kwamba Jose alikazania tatizo la UKIMWI kama kwamba lilimhusu sana yeye binafsi. Hili linajidhihirisha kutokana na bidii ya Jose katika kunadi mipira ya kondomu pale *Malaika Bar* kila jioni kwa kupaza sauti akisema:

“Mambo kwa soksi! Mambo kwa soksi! Maji uyavalie nguo ndipo uyakoge! Ulapo ndizi usiimenye ila ivishe ganda! Jando la Raha Leo ni kuvishana magozi!” (Mkufya, 2005:12).

Jose alikuwa anasisistiza matumizi ya mipira ya kondomu katika kufanya ngono. Kulingana na Jose, dhana ya kuvishana mipira inafaaa kuwa jukumu la watu wote iwapo wanajamii wangetaka kufaulu katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Yeye anaona kuwa ngono inaweza kufurahiwa bila wasiwasi za maambukizi iwapo watu watatumia mipira hii. Hata hivyo wengi hawakupendezwa na biashara ya Jose. Kwa mfano, Chiku alipomwona Jose, alimsogelea na kumwonyesha njia atoke. Jose alikashifiwa na Chiku lakini hakujali. Alisimama katikati ya ukumbi na kurudia maneno yake. Hakuna mteja aliyenunua mipira ile ila mhudumu mmoja Yakobo ambaye alinunua pakiti kumi kwa ajili ya wateja wake ambao walizinunua usiku kwa bei nzuri baada ya maduka yote kufungwa. Hii inaonyesha kuwa wanajamii wanajua kuwa mipira inaweza kuwazuia kutokana na kuambukizwa maradhi ya UKIMWI ila wanapuuza maoni haya. Yakobo naye anajua kuna watu wachache ambao hutumia mipira, labda watu hawa huogopa kununua mipira ya kondomu hadharani kutoka kwa muuzaji lakini wanapoipata wanaitumia.

Chiku ambaye alikuwa akimkashifu Jose alipokuwa akinadi mipira ya kondomu pale *Malaika Bar*, alikuwa akifanya kazi ya kuwahudumia wateja. Baada ya muda wakiwa na rafikiye Pendo waliwachishwa kazi. Alienda kutafuta kazi kwenye baa nyingine (Alwatan). Lakini baada ya muda alipelekwa nyumbani kwao kutokana na kuugua maradhi ya UKIMWI. Mhusika huyu ambaye aliona kazi ya Jose ya kunadi mipira kama isiyostahili, anaugua maradhi yale yale aliyokuwa akitahadharishwa. Chiku anawakilisha wanajamii ambao hupuuza mawaidha hata iwapo ni ya kuwafaa. Chiku alimpuuzilia

mbali Jose na kumkashifu kama kwamba hakuwa akifanya mapenzi. Iwapo angemsikiza Jose, hangepata maradhi yale kwa kuwa mipira hii inazuia maambukizi.

Mhusika mwingine ambaye alishangazwa na Jose ni Omolo. Kwake, alishangaa kwa kuwa Jose alichukua tatizo la maradhi yale kama tatizo lake binafsi. Hata hivyo Omolo alijua kuwa ilikuwa muhimu kutumia mipira wakati wa kufanya ngono. Omolo alikuwa rafiki yake Queen ambaye walikuwa wamejuana katika shughuli za kazi. Hata hivyo Queen na Omolo walikuwa wamefanya mapenzi kwa kutumia mipira ya kondomu. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Kama Mima siku ile, Queen alishitushwa na kutotahiriwa kwa Omolo. Lakini yeye akawa mstaarabu. Hakucheka wala hakughairi. Ila alikwenda kabatini, akatoa mpira wa kiume, akamrushia Omolo akauchukua na kuvaa. Na siku ile ikawa ya kwanza kwa Omolo kulifurahia tendo lile akiwa katika utu uzima wake. Mipira miwili ilitumiwa na siku ile aliporudi nyumbani kwake ilikuwa usiku. Alichoka sana. Hakuwa na hamu ya kwenda *Malaika Bar* (Mkufya, 2005: 52).

Omolo alifurahia tendo lile bila wasiwasi wowote wa maambukizi. Hii inaonyesha kuwa iwapo wanajamii watumia mipira watafurahia tendo lile la kujamiiana bila woga wowote. Hata hivyo, mhusika Queen anatoa mipira ya kiume wala si ya kike, hii inaonyesha kuwa huenda jamii imewatenga wanawake katika kukabiliana na maradhi haya. Iwapo mipira ya kike itakuwepo, wanawake wanaweza kuwa na nafasi nzuri ya kujikinga wala si kusubiri wanaume kuamua hatima yao. Japo Queen alitumia mipira, hakuwa akifurahia. Anamwambia Omolo aende akakamilishe tohara. Hii inaonyesha kuwa bado wanajamii hawatilii maanani matumizi ya mipira ya kondomu katika

kukabiliana na maambukizi ya maradhi haya. Kwao, matumizi ya mipira inawafanya kukosa kufurahia ngono.

Katika kushadidia maoni haya, Kobia (2008:62) anasema, katika jamii ya Luhya, kuna usemi unaotumiwa na wanajamii kuwa hakuna utamu wowote katika kula peremende iliyofungwa kwa karatasi. Hili linaonyesha kuwa wanajamii hawafurahii ngono wanapotumia mipira ya kondomu. Hata hivyo, wanaonywa kujitahadharisha na maradhi ya UKIMWI kwa kuambiwa kuwa iwapo wanakula 'ndizi' hasa vijana walio na marafiki wengi ni vizuri kula na maganda yake. Ikiwa na maana kuwa kuna haja ya kutumia mipira wanaposhiriki ngono. Mara nyingine Queen alifaulu tena kumhadaa Omolo. Mara hii mipira ulichanika. Omolo hakurudia tendo hilo na alikimbia bafuni akaoga kama anavyosema:

Kama siku ile ya kwanza, walitumia mipira. Queen akamwambia, "Bwana nenda ukakamilishe tohara. Kila siku kutumia mipira haipendezi." Omolo akaitikia, lakini moyoni alisema, "Pumbavu! Huu ndio mwisho". Waliendelea safari ya pili na ya tatu. Lakini safari ya tatu mipira ulichanika. Omolo akachomoka upesi na kukimbilia bafuni. Akaoga na kusafisha sehemu zilizohusika mara nyingi kama mtu anayejitakasa (Mkufya, 2005:53).

Omolo anaepuka maradhi haya kwa kutumia mipira ya kondomu. Japo Omolo hakupendezwa na kazi yake Jose, alijua kuwa mipira ya kondomu ilikuwa muhimu katika kuepuka maambukizi. Kwa Omolo kukimbia bafuni na kuoga ni udanganyifu unaoweza kupotosha jamii kuwa unaweza kuepuka maambukizi ya maradhi haya kwa kuoga. Kauli hii inashadidiwa na wanaharakati wanaokabiliana na maradhi ya UKIMWI nchini Afrika Kusini waliomkashifu Jacob Zuma mwaka wa 2006 kwa kusema kuwa alioga baada ya

kushiriki ngono na mwanamke aliyekuwa akiugua maradhi ya UKIMWI kama njia ya kuepuka maambukizi. Kulingana na wanaharakati hawa, usemi huo unaweza kuharibu juhudi zao za miaka mingi za kukabiliana na maradhi haya kwa kuwahadaa wanajamii kuwa unapooga baada ya kushiriki ngono na aliyeathiriwa na maradhi haya utaepuka maambukizi. Kwa kukiri kuwa hakutumia mipira japo alijua kuwa mwanamke huyo alikuwa na maradhi ya UKIMWI liliwafanya wanaharakati hawa kuhami hasa ikizingatiwa kuwa nchini Afrika Kusini kuna watu milioni tano wanaougua maradhi ya UKIMWI na njia kuu inayoeneza maradhi haya ni kushiriki ngono bila kinga (BBC, 2006).

Ngoma pia alikuwa rafiki yake Queen lakini hawakutumia mipira ya kondomu ndio maana alimwambukiza UKIMWI. Tofauti na Omolo, Ngoma anatumia mipira na mkewe wakati tayari amepata maradhi haya kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Ngoma alifanya kazi kubwa kumlaghai mke wake mpaka akamwamini. Hivyo, siku ile walifanya tendo la ndoa kwa kutumia mipira. Lakini tendo lile lilikuwa geni kwao. Hakuna aliyelifurahia. Walijiona kama wanacheza, kama watoto wadogo wanaoigiza mchezo wa ndoa vichakani, maana, umuhimu na heshima ya tendo lile vikapaushwa na kuweko kwa ukuta wa mpira uliotenganisha miili na damu zao; ukuta ambao haukuwa na sababu kama kila mmoja wao angekuwa mwaminifu; ukuta ambao, katika hisia za Tabu ulikuwa mwanzo wa kutenganisha miili na nafsi zilizounda unyumba wao (Mkufya, 2005:31).

Kwa mhusika Tabu, matumizi ya mipira katika ndoa yanafanya tendo lile la ngono lisifurahishe, kwake mipira inaleta utengano. Kama vile Queen, Tabu ni mhusika ambaye matumizi ya mipira haifurahishi lakini hata hivyo msimulizi anatuonyesha kuwa iwapo tutatumia mipira tutaepuka maambukizi. Ngoma alitumia mipira wakati tayari alikuwa

amepata maradhi yale na kumwambukiza mke wake. Lakini iwapo angetumia mipira mara ya kwanza na rafiki yake Queen, hagemwambukiza mke wake.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa mhimili wa mtazamo wa msimulizi tunaona msimulizi anasisitiza kuwa tunaweza kuepuka maradhi haya iwapo wanajamii watazingatia matumizi ya mipira ya kondomu. Iwapo wahusika wale waliokuwa *Malaika Bar* wangemsikiza Jose, hawangepata maradhi haya ya UKIMWI.

Japo matumizi ya mipira ya kondomu yameonekana kuwa njia bora ya kuzuia kuenea kwa maradhi ya UKIMWI, jambo hili limepata pingamizi kutoka kwa asasi za kidini. Kwa mfano, kulingana na Thavis (2009), kanisa la Katoliki lilipinga matumizi ya mipira ya kondomu katika ndoa na kuisitiza elimu ya kujamiina kuegemea katika uaminifu. Viongozi hawa wa kidini wanasema kuwa, kutegemea mipira ya kondomu katika kuzuia maambukizi ya maradhi ya UKIMWI kutawadanganya wanajamii kwa sababu wakati mwingine mipira hii hupasuka na kuvunja. Kuhimiza matumizi ya mipira kutafanya wanajamii kushiriki katika ngono za kiholela na uasherati. Kwa hiyo, serikali na wanajamii wanafaa kuisitiza uaminifu katika uhusiano wala si matumizi ya mipira ya kondomu (Katheya, 2002).

4.2 KUACHA UASHERATI

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), msimulizi anaonya wanajamii dhidi ya uasherati kama njia inayoeneza maradhi ya UKIMWI. Msimulizi anawatahadharisha wanaume

dhidi ya wanawake malaya. Kwa mfano Queen alikuwa mwanamke mashuhuri mtaani kwa urembo wake, mwanamke pekee msomi na mwenye cheo kikubwa kazini kwake. Hata hivyo, mwanamke huyu hakujiheshimu kwa kuwa alifanya mapenzi na wanaume wengi kama vile Ngoma na Omolo. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

“Queen!” Jina hili lilivuma akilini mwake kwa nguvu kama upepo wa kimbunga. Ni kweli kwamba mwanamke yule malaya amewajeruhi watu aliowapenda kiasi kile? Kama amemdhuru Ngoma, basi hata dada yake amedhurika. Na kama hao wamedhurika, Omolo je, atakuwa amepona? Asubuhi ya siku ile, Queen ndiye aliyepiga simu na kumwambia ana jambo la muhimu kumwambia Omolo. Pengine jambo lenyewe ni hizo habari za UKIMWI! Wazo la Omolo kuweza kufanya mapenzi na malaya huyo lilimchefua moyo. Hakupenda kulifikiria. Akalirushia pembeni. Akamtazama dada yake. Alishindwa kummaliza (Mkufya, 2005:59).

Japo Queen alikuwa mashuhuri, aliharibu umaarufu ule kwa kushiriki katika umalaya. Yeye anafanya mapenzi na wanaume wengi kwa mfano Ngoma na Omolo na kuchangia katika kueneza maradhi ya UKIMWI. Hii inaonyesha kuwa ni vyema kuwa na mpenzi mmoja. Iwapo Queen angekuwa na mpenzi mmoja, Tabu hangeambukizwa maradhi ya UKIMWI.

Mhusika mwingine ambaye alikuwa malaya pale Tandika ni Asha. Asha Mmanyema alikuwa na rafiki Mzungu aliyetitwa Hastings kama tunavyoambiwa:

Uingiapo kwenye hoteli ya Victoria, ukiangaza macho juu ya kaunta, ukutani, utakutana uso kwa uso na picha kubwa ya Mzungu huyo, akiwa amesimama na Asha enzi hizo walipoishi kama mtu na hawara wake (Mkufya, 2005:83).

Kabla ya kifo chake, Hastings alimjengea nyumba nzuri ya ghorofa na kumwachia pesa nyingi. Lakini hata hivyo baada ya kifo chake Asha hakutaka kuolewa na kwa sababu

alikuwa na mali aliona kuwa hakutaka kujifunga katika ndoa. Alitaka uhuru na kutokana na uhuru huo alikuwa na uhusiano na wanaume wengi kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Kilichothibitisha ile kauli kwamba Msafiri kaolewa ni ule uhuru wa Asha kuwa na marafiki wengine bila kuogopa kwamba, kwa uhuru huo angeathiri uhusiano wake na Msafiri. Mmoja wa marafiki wa kiume aliowapata wakati 'mume' wake akiwa safarini alikuwa Ngoma (Mkufya, 2005:82).

Kwake Asha pesa zinamfanya kuwa na uhuru wa kuwanunua wanaume. Yeye hakuwa mhitaji na kwa hivyo aliweza kuchagua kufanya mapenzi na mwanaume aliyependa. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Asha akacheka sana akasema, "Sinunuliwi. Nitakununua wewe kwa senti hamsini na busu moja shavuni." Msafiri akanyanyuka kwa nguvu na kutaka kumwendea pale alipo. Macho yake yalikuwa mekundu kwa shauku. Asha akacheka, akanyanyuka na kujifanya anataka kukimbia. Mwili wake ulikuwa mzito. Msafiri akamwendea (Mkufya, 2005: 81).

Kutokana na uhuru wa Asha, anajihusisha kimapenzi na Ngoma. Katika uhusiano huu Asha anapata UKIMWI kwa kuwa Ngoma alikuwa rafikiye Queen. Kutokana na tabia ya Asha tunaona maradhi haya yakiingia katika ndoa ya Msafiri. Kwa hivyo msimulizi anatahadharisha dhidi ya kushirikiana na wanawake malaya kama Queen na Asha. Iwapo wanaume watajihusisha na wanawake hawa ni vyema kutumia mipira ya kondomu kwa mfano Omolo alilala na Queen lakini akatumia mipira na kuepuka kuambukizwa maradhi haya.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007) mhusika Fumbwe anashiriki uasherati baada ya kutengana na mke wake Hatima na hatimaye kupata maradhi ya UKIMWI. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Hayo ajua Mungu ila hizo tetesi zilimfanya Fumbwe kumbadilikia mama na mwana. Hapo ndipo alipoanza mbio zake. Akawa ni mtu asopisha rinda. Maji yalizidi unga pale alipowakuta Chongea na Hatima katika mambo yao (Omar, 2007:177).

Fumbwe anapomfumania Hatima anajiingiza katika ulevi pamoja na kufanya mapenzi na wanawake wengi na mwishowe kupata ndwele isiyotibika. Jambo hili linajidhihirisha kutokana na tabia zake Fumbwe ambaye anafanya mapenzi na wasichana wadogo hata ofisini. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Baada ya muda mfupi, alitoka ndani msichana. Alivaa nguo zilizoonya zaidi ya kusitiri. Harufu ya manukato ilimfuata alipopita. Alielekea walikokuwa wamekaa watu, akasimama karibu na Tufaha. Yule bwana aliingia ndani.

'Mpaka kesho,' alisema.

'Haya kwaheri,' akaitikia mhazili.

Simu ililia na yule msichana akarudi tena ofisini. Yaonekana mkutano wake na mwenye afisi ulikuwa muhimu sana. Kikao chenyewe kilidumu kwa muda wa saa tatu. Msichana wa watu alipotoka mle ofisini alionekana kuchoka. Kibeti chake kwapani alifululiza mlangoni huku nyuma akiacha harufu kali ya marashi. Hakutaka kuwatizama waliokuwa ukumbini (Omar, 2007: 119).

Tabia ya Fumbwe ya kujiingiza katika uasherati inadhihirika katika kifungu hiki.

Jambo ambalo hakujua kuwa litaweza kuyahatarisha maisha yake. Mwishowe anapata maradhi yanayomtatiza hadi kufa. Kwa kuangazia tabia ya Fumbwe, msimulizi anawatahadharisha wanawake kutojikusisha na wanaume wenye wapenzi wengi kwa kuwa hilo laweza kuwafanya kupata maradhi ya UKIMWI.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Matendo ya Usemi, msimulizi anaonya dhidi ya uasherati kama njia mojawapo ya kujiepusha na maradhi ya UKIMWI. Ni wazi kuwa wahusika wengi wanaoambukizwa maradhi haya katika riwaya hizi na mwishowe kufa, wanashiriki katika uasherati hasa ikizingatiwa kuwa uasherati ndiyo njia kuu ya kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Kama tunavyoambiwa na Zulu na wengine (2004:167) kuwa, nchini Uganda, ufanisi wao katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI ulitokana na kuwahimiza wanajamii kutoshiriki ngono na wepenzi wengi.

4.3 UAMINIFU KATIKA NDOA

Jambo lingine linaloweza kufanya maradhi ya UKIMWI kudhibitiwa ni kuwa mwaminifu katika ndoa kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005). Wahusika Ngoma na Msafiri wanawaambukiza wake zao UKIMWI kwa kuwa hawakuwa waaminifu katika ndoa. Ngoma alikuwa mumewe Tabu na alikuwa akifanya mapenzi na Queen. Ngoma alipata maradhi haya na kumwambukiza Tabu. Ngoma pia alifanya mapenzi na Asha na kumfanya Msafiri kuambukizwa. Omolo alijua haya na alipokuwa *Malaika Bar* aliwaona Ngoma na Asha wakizozana akauliza:

Ngoma na Asha walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Pia, Omolo alikwishawahi kumfumania Ngoma nyumbani kwa Queen. Alikuwa anajua tabia ya uzinzi ya jirani yake. Ikiwa Queen alikuwa mgonjwa, bila shaka amemwambukiza Ngoma kama hawakutumia mipira. Je, mzozo ule unahusiana na yale aliyokuta kwa Queen siku ile? (Mkufya, 2005:71).

Ni wazi kuwa japo Ngoma alikuwa ameo hakuwa mwaminifu na ndio sababu ilimfanya kumwambukiza mke wake UKIMWI. Alifanya mapenzi na Queen na Asha bila kutumia mipira.

Mhusika mwingine ambaye alikuwa ameo na hakuwa mwaminifu katika ndoa ni Msafiri kama tunavyoambiwa:

Asha aliketi pale kwenye kaunta ya hoteli yake akimwazia mpenzi wake, Msafiri. Hofu ilimzidi alipofikiria kwamba, kama Ngoma amemwambukiza UKIMWI, hata yeye atakuwa amemwambukiza Msafiri (Mkufya, 2005:83).

Msafiri anayapata maradhi haya na kumwambukiza mke wake kutokana na kutokuwa mwaminifu. Msafiri alikuwa rafiki yake Asha na kwa kuwa alikuwa akija baada ya muda hangejua Asha alikuwa msherati. Angaliepuka maradhi yale iwapo angalikuwa mwaminifu.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007) mhusika Fumbwe anapata UKIMWI kutokana na kutokuwa mwaminifu. Hatima (mkewe) pia hakuwa mwaminifu. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Siku zote huzuni imemtawala Fumbwe asione raha ya kuishi. Mke aliyemtwa akiwa hana chochote. Akamshughulikia kimasomo hadi yake kupata stashahada ya elimujamii. Malipo yake kumla kivuli, tena nyumbani kwake. Ndiyo na yeye pia alikuwamo na jicho lake la nje. Lakini mengi akiyafanyia nje. Pengine mara moja tu aliwahi kujisahau akayafanya nyumbani (Omar, 2007:176).

Ni wazi kuwa ndoa kati ya Hatima na Fumbwe inavunjika kwa sababu wote hawakuwa waaminifu. Fumbwe anambaka Kibibi na kumpachika mimba Habibi anapokwenda kuzuru wazazi wake kule kijijini. Fumbwe naye anamfumania Hatima wakiwa na

Chongea alipomhadaa Hatima kuwa alikuwa ameenda kuwazuru wazee wake kijijini. Jambo ambalo linamfanya Fumbwe kuachana na Hatima na kuingia katika ulevi na uasherati na mwishowe kupata maradhi ya UKIMWI.

Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Matendo ya Usemi, msimulizi anaangazia ndoa hizi kwa lengo la kuwaonya wanajamii dhidi ya uzinzi. Katika kufanya hivyo anahimiza uaminifu katika ndoa kama njia ya kuepuka kupata maradhi ya UKIMWI katika ndoa. Kwa mfano ndoa kati ya Dkt. Hans na mkewe Kristina katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) ni kielelezo cha kufuatwa na wanajamii. Iwapo uaminifu utakuwa katika ndoa UKIMWI utadhibitiwa.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), ndoa kati ya Kibibi na Salala ni mfano mzuri wa kuigwa. Hata iwapo Salala anafariki na kumuacha Kibibi mjane, tunaona kuwa anakufa kutokana na ajali barabarani wala si maradhi ya UKIMWI. Ndoa nyingine ni kati ya Mwalimu Selemani na mkewe Habiba. Wahusika hawa wanakuwa waaminifu katika ndoa yao hadi pale Mwalimu Selemani anapokufa baada ya kukumbwa na kiharusi.

Katika kushadidia haya, wanaharakati wote wanawanaoshughulika katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI wanasisitiza uaminifu katika ndoa. Hili pia limeungwa mkono na asasi za kidini ambazo zinasisitiza uaminifu katika ndoa kama njia bora ya kudhibiti kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano, Baba Mtakatifu wa kanisa Katoliki

aliorodhesha njia za kudhibiti kuenea kwa maradhi haya. Njia hizo kulingana naye ni kama: kutozini, kuwa waaminifu katika ndoa na kukabiliana na umaskini (B. B.C, 2005).

4.4 UBABE-DUME

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) msimulizi anakashifu ubabe-dume kama njia inayofanya maradhi ya UKIMWI kuenea. Kwa mfano, Ngoma anamdunisha mke wake kiasi cha kumwambukiza maradhi haya. Ngoma alikuwa tajiri kutokana na biashara zake kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Zamani alipopata pesa alidhani furaha ya maisha iko kwenye anasa hata kama akimkirihi mke wake. Sasa anasa zimemwegesha katikati ya miiba. Kila alipogusa akakuta panachoma (Mkufya, 2005:138).

Ngoma alipata pesa nyingi kutokana na biashara zake. Lakini pesa hizi alizitumia katika anasa. Alikuwa akinywa pombe na wanawake kama vile Queen na Asha. Ngoma alikuwa akifika kwake usiku wa manane bila kumwogopa mke wake Tabu. Kutokana na utajiri huu, Ngoma alimdharau mke wake kwa kuwa hakuwa na mapato yakilinganishwa na aliyopata katika biashara zake. Tunaona Ngoma akijistarehesha na wanawake (Queen na Asha) na marafiki zake Mpemba, Zito na kuitelekeza familia yake. Ngoma alimdharau mke wake kiasi cha kufanya mapenzi na wanawake na kurudi nyumbani akiwa amelewa na kunukia marashi ya wanawake wengine.

Hata katika kufanya maamuzi, tunaona Ngoma ndiye anayeamua. Kwa mfano, yeye ndiye anayemfanya Tabu kuwacha dini yake ya Kikristo na kujiunga na Uislamu. Vilevile katika kufanya mapenzi, yeye ndiye anayeamua kutumia mipira. Tabu hana

uamuzi wowote. Lake ni kufuata uamuzi wa Ngoma. Hii inajidhihirisha pale Ngoma anapomlaghai Tabu kuwa watu, hata wanandoa hutumia mipira anaposikia fununu kuwa Queen anaugua. Mwandishi anasema;

Kesho yake pia Ngoma alirudi nyumbani mapema, ila alikuwa amelewa sana. Tabu alikataa kunywa pombe siku ile. Baada ya chakula cha jioni, walipokwenda kulala, Ngoma alimpa mke wake pakti mbili za mipira ya kiume akamwambia, “Ma’Juma, siku hizi magonjwa ni mengi. Hujui sisi wanaume tunakopita. Mimi naona tunapotaka kukutana tutumie hii mipira.” (Mkufya, 2005:138).

Ngoma ndiye anayefanya maamuzi jambo linalomfanya Tabu kupata maradhi yale. Japo Tabu alijua mume wake hakuwa mwaminifu, hangemwambia atumie mipira kwa sababu mume wake hangekubali.

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), ubabe dume wa Fumbwe unamfanya kushiriki katika uasherati jambo ambalo tunaona linamfanya kuambukizwa maradhi ya UKIMWI. Yeye anaona fahari kuwa baada ya kumfumania Hatima wanaachana, lakini hata hivyo yeye anapata maradhi ya UKIMWI.

Katika kushadidia maoni haya, Onyango (2007) anaunga mkono wazo kuwa ubabe dume ni kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Anashikilia kuwa itikadi na nguvu za kijamii zinaelekea kuwapendelea wanaume na katika hali hii wanawake ndio walioathirika sana kuhusu maambukizi ya UKIMWI. Hii inatokana na misingi inayowapendelea wanaume na kuwadhalilisha wanawake. Kwa mujibu wa nadharia ya Matendo ya Usemi, msimulizi anakashifu ubabe dume kama njia inayochangia kuenea

kwa maradhi ya UKIMWI. Iwapo wanawake hawatadhalilishwa, wanaweza kufanya maamuzi na kuepuka maambukizi.

4.5 VIPINGAMIZI VYA KIJAMII

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), msimulizi anakashifu vipingamizi vya kijamii kama vile ndoa kama mojawapo ya chanzo cha kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano, Tabu alizoea kujiuliza kama kulikuwa na umuhimu wa ndoa yao. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Tabu alijiuliza maswali mengi lakini mara nyingi hakupata jibu. Ila alitoa kisingizio kwamba baba na mama yake na ndugu zake watamlaumu kwa kuvunja ndoa iwapo ataamua kuachana na Ngoma. Pia aliogopa kwamba jamii itamcheka kwa kuwaachia malaya wamchukue mume wake na kuacha watoto wao wapate shida kutokana na wazazi wao kufarakana. Aidha aliogopa Mungu atamlaani kwa kuvunja kiapo cha ndoa alichopa pale walipofunga ndoa hii. Visingizio hivi ndivyo vilivyomfanya avumilie na kubeba mzigo mzito wa ndoa ile. Lakini siku alipogundua kwamba kuvumilia kwake kumemletea baa kubwa zaidi, alilia sana. Alijuta, alishindwa kujisamehe kwa ujinga wake. Alilaani vipingamizi vya kijamii vilivyomfanya asite kumkimbia mwanamume yule. Zaidi ya hapo, alilaani utumwa, uonevu na usaliti uliofichama katika jambo lile la kijamii lililoitwa ndoa (Mkufya, 2005:112).

Kulingana na msimulizi, asasi ya ndoa ambayo imeundwa na jamii inawafanya wahusika wengine kupata UKIMWI. Kwa mfano ni kutokana na kuiogopa jamii ndipo Tabu anapata maradhi haya. Msimulizi anakashifu vipingamizi vya kijamii vinavyowafanya watu watumwa na kuogopa kijikomboa na mwishowe kupata maradhi haya. Wahusika kama Tabu na mkewe Msafiri wanapata maradhi haya kwa ajili ya ndoa. Kwa mujibu wa mhimili wa mtazamo wa msimulizi, msimulizi anawahimiza wanawake kujikomboa kutokana na vipingamizi kama ndoa hasa wanapojua kuwa wanaume wao si waaminifu.

Hawafai kuogopa kile jamii itasema. Iwapo wanawake watajikomboa, maradhi ya UKIMWI yatadhibitiwa

Katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), tunaona Hatima ambaye alikuwa mkewe Fumbwe akiepuka maradhi kwa sababu ya kuvunjika kwa ndoa yao. Tofauti na Tabu, Hatima alikuwa kiruka njia kama mume wake. Lakini anapofumaniwa wakiwa na Chongea, anaamua kutoka kwenye ndoa hiyo jambo linalochangia katika kumwepusha na maradhi ya UKIMWI.

Katika kushadidia maoni haya, utafiti ulifanywa na UN (2004) ulionyesha kuwa maradhi ya UKIMWI yalionekana kuwaathiri sana wanawake. Utafiti huo ulionyesha kwamba, wanawake wengi ambao wako kwenye ndoa wanakumbwa na maradhi haya ya UKIMWI kwa kuwa hawana uwezo wa kutoa maoni yao hasa kuhusu maswala ya kujamiiana na kawahimiza wanaume wao kutumia mipira ya kondomu. Naye Philips (2004: 164) anasema, wanawake ndio walioathirika sana katika maambukizi haya kwa sababu ya nafasi yao katika miundo ya jamii na uwezo duni katika kufanya mashauri kuhusu kinga katika maswala ya kujamiiana na hasa wanawake walio kwenye ndoa. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwahusisha wanawake katika maswala haya na kuwaona kama wenye nafasi sawa na wanaume katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI.

4.6 KUWAWEZESHA WANAWAKE KIUCHUMI

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) msimulizi anaangazia umaskini kama chanzo cha kuambukizwa na kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Kwa mfano, Tabu ni mwanamke ambaye anapata maradhi haya kutokana na hali yake ya kiuchumi. Tabu (mkewe Ngoma) hakuwa akifanya kazi yoyote. Kazi yake ilikuwa kuwalea wanawe. Mumewe (Ngoma) alikuwa mfanyabiashara aliyemiliki magari. Japo Ngoma alikuwa na pesa, alizitumia pesa hizo katika anasa na kuitelekeza familia yake. Jambo hili linamlazimu Tabu kuanzisha biashara ya genge ambayo inamsaidia katika kukidhi mahitaji yake na wanawe. Kama anavyosema mwandishi:

Juma alimchukia sana baba yake. Aliichukia tabia yake ya ulevi, kuvuta sigara na mizozo ya mara kwa mara na mama yake. Pia, Juma alimchukia baba yake kwa kutomjali mama yake na kumsababisha ajishughulishe na biashara za kupika vitumbua na chapati; na kuuza genge la mboga ili apate pesa za kujinunulia mahitaji yake.

Ngoma alikuwa tajiri. Alimiliki magari manne ya abiria pale kijijini. Kwa siku magari hayo yalimwingizia pesa nyingi. Lakini kila wakati Juma alimsikia mama yake akisema kuwa baba anajitahiki kuweka pesa ili anunue gari lingine. Alijua baba yake anatumia pesa alipokwenda kulewa. Pesa za kununulia bia mbili tu, zililingana na faida ya mapato yote aliyoyapata mama yake kwa siku kwenye genge (Mkufya, 2007:34).

Ni wazi kuwa Ngoma alikuwa na mapato mazuri kuliko mkewe na kwa sababu hii alimdharau mkewe. Mali ile anaitumia katika anasa na mwishowe anapata maradhi ya UKIMWI. Mapato ya Tabu yalikuwa kidogo ikilinganishwa na Ngoma. Tofauti hii inampa Ngoma kiburi na kumfanya kumdhulumu mke wake na watoto kwa kuwatelekeza. Tabu naye anavumilia katika ile ndoa akijua mume wake ni asherati kwa sababu ya mapato duni kutokana na biashara yake ya genge na kuhofia kuwaacha

wanawe. Kutokana na ufakiri wake anavumilia katika ndoa ile na mwishowe anapata maradhi ya UKIMWI.

Mhusika mwingine ambaye anaathirika kutokana na hali yake duni ya kiuchumi ni Chiku. Chiku alikuwa rafikiye Pendo na walikuwa wakifanya kazi *Malaika Bar*. Wasichana hawa wanafanya kazi hii ya kuwahudumia wateja kwenye baa kwa ajili ya uhitaji. Mshahara ambao wanapata ni mdogo ukilinganishwa na mahitaji yao, jambo ambalo linawafanya kuomba kununuliwa mishikaki, vileo na hata kushiriki katika ngono ili kukidhi mahitaji yao. Kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Muza nyama alipita karibu yake, akamuuliza, “Mzee tuchome mingapi leo? Omolo alimtazama, akatingisha kichwa kwa kukataa na kusema, “Nimeshakula chakula nyumbani.” Pendo na Chiku walicheka. Sasa wakawa wamepata pa kuanzia. Wakamwambia, “Tununulie sisi. Toka asubuhi hatujala kitu.”

“... Mwataka mingapi?”

Wakamjibu kwa pamoja, “Kiasi chochote utakachonunua. Mfuko wako tu”. Sauti zao zilijaa mzaha na ukorofi wa kike kwa mwanaume. Macho yao yalimtazama huku kope zikipepesa kwa ishara za kumshawishi.

...mchoma nyama akaanza kuondoka. Omolo akaagiza “Yakobo, hebu wapatie mishikati mitano kila mmoja. Alipomaliza kusema, akageukia kaunta.

“Asante kaka yetu!” walimshukuru. Sauti zao za pamoja zilikuwa na mkwaruzo kidogo na wororo wenye kuamsha hisia za kiume (Mkufya, 2005:34).

Ni wazi kuwa wahusika hawa wameajiriwa. Lakini ujira wao hautoshelezi mahitaji yao.

Jambo hili linawasukuma kuwaomba wateja (wanaume) na hata kushiriki katika anasa

kama tunavyoambiwa na Omolo:

Furaha aliyokuwa ameizoea *Malaika Bar* ilipungua baada ya kusikia Pendo na Chiku wamesimamishwa kazi baada ya kusababisha shoti kubwa ya pesa za mauzo. Baada ya kuacha kazi *Malaika*, Chiku aliajiriwa *Kanga*

Moja Club na Pendo akapata kazi kwenye baa nyingine iliyoitwa Alwatan. Haikupita zaidi ya miezi miwili, Chiku akaanza kuugua magonjwa mbalimbali. Hatimaye, mwajiri wake akamwachisha kazi. Kulikuwa na tetesi kwamba alikumbwa na UKIMWI. Pendo aliendelea kufanya kazi Alwatan. Omolo hakuwa na habari zozote kama huko nako kaacha au la. Kulikuwa na habari za kuaminika kwamba wiki chache baadaye, Chiku alirudishwa kwao Tabora akiwa amedhoofu sana (Mkufya, 2005:203).

Chiku anapata maradhi haya kutokana na hali yake ya kiuchumi. Mbali na kuombaomba wanaume ama kuwanunulia pombe au mishikaki, wanawake kama hawa hulazimika kulala na wanaume bila kinga yoyote na mwishowe kupata maradhi ya UKIMWI. Kwa mujibu wa mhimili wa mtazamo wa msimulizi, kuna haja ya kupiga vita umaskini kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kuwasaidia kuepuka maradhi ya UKIMWI. Iwapo Chiku na Tabu wangukuwa na uwezo kiuchumi, wangukuwa katika nafasi nzuri ya kuepuka maradhi haya.

Hata hivyo, katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), mhusika Hatima anaepuka maradhi haya kutokana na kutengana na Fumbwe. Yeye alikuwa amesoma na alikuwa ameajiriwa, kwa hiyo aliweza kujikimu hata baada ya kutengana na Fumbwe. Uwezo wake kiuchumi unamsaidia katika kutoka kwenye nyumba ya Fumbwe jambo ambalo linamwepusha kutokana na maradhi ya UKIMWI.

Vilevile, katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), tunapata mhusika Kibibi ambaye alisoma hadi katika darasa la nane na kukosa kuendelea na masomo ya sekondari. Kibibi alibakwa na Fumbwe na kupachikwa mimba. Aliporudi kwao (kwa Mwalimu Selemani), wazazi wake walimfukuza kwa kuwa hawangeweza kustahimili aibu ile. Hata hivyo, tunaona

tofauti na Chiku katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), Kibibi anajikomboa kwa kuanzisha biashara ndogo ambayo inamsaidia katika kukidhi mahitaji yake kama tunavyoambiwa na mwandishi:

TUFAHA alikuwa ameamua kujisabilia kukilea kitoto chake. Alitaka kumlea Kala kwa tunu na tamasha. Wala hakujali gharama na dhiki alizopambana nazo katika hali ya kumkidhia mwanawe haja zote. Hakuwa na jingine ila kufanya hivyo viashara vya kijungu jiko mekoni, apatacho wakitumie na akikosa ajishukurie. Alikusudia kuhakikisha kwamba mwanawe amepata elimu, nuru ya maisha ambayo yeye alihiniwa kwa kuwa kazaliwa mwanamke.

Biashara hii inamsaidia katika kukidhi mahitaji yake, Ma'Asha na Kala. Vilevile anamsomesha Kala mpaka anahiti na kuwa daktari. Biashara hii inamwepusha na kujiingiza katika uasherati kama njia ya kupata mapato. Mwishowe biashara yake inanawiri katika jambo ambalo linamfanya kujisimamia kiuchumi na kumwepusha Kibibi kutokana na kushiriki katika uasherati kama njia ya kujipa mapato na kuambukizwa maradhi ya UKIMWI.

Katika kushadidia haya, Akuffo (1987) anasema kuwa, ili kukabiliana na maradhi ya UKIMWI kuna haja ya kutilia maanani umaskini ambao unaendelea kuongezeka katika jamii hasa katika miji. Umaskini uliokithiri, mzigo wa maradhi, ukosefu wa ajira katika jamii unaonekana kuchangia kuwafanya wanajamii kuwa na wapenzi wengi na kujiingiza katika uasherati ili kukidhi mahitaji yao. Kwa hiyo, iwapo jamii inataka kukabiliana na (maradhi haya kuna haja ya kuwapa wanajamii ajira ili kuwafanya kutoshiriki katika tabia ambazo zinachangia kuenea kwa maradhi ya UKIMWI.

4.7 KUPIGA VITA UNYANYAPAA NA KUWAPA WAATHIRIWA MATUMAINI

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005) msimulizi anaangazia vita dhidi ya unyanyapaa kama njia ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Njia moja ni kwa kutumia usemi usioyafanya maradhi haya kutisha. Kama tulivyojadili katika sura iliyotangulia, uvumbuzi wa maradhi ya UKIMWI uliititiza jamii kabla kudhibitiwa na kueleweka kama maradhi yanayofanya mwili kupunguza kinga ya maradhi. Wakati huo kulikuwa na usemi ulioyafanya kutisha. Mara uliitwa uchawi, kifo, laana, ugonjwa mpya usio na tiba. Katika kuyatambua maradhi haya kwa kutumia usemi huu, walioathirika walinyanyapaishwa. Hata hivyo, baada ya utafiti wa kina kufanywa, wanajamii walipata ufahamu wa kutosha. Mwishowe kukawa na mwikio chanya kuyahusu. Usemi uliokuwa ukitumiwa awali ukabadilika. Wanajamii hawa wakaanza kuyatania kwa kuyaita mwiba, mdudu, kudura na katika kufanya hivyo inaonyesha mwikio chanya wa wanajamii kuhusu maradhi haya.

Njia nyingine ya kuondoa unyanyapaa ni kuwaonyesha upendo walioathriwa. Kwa mfano Tabu alipogundua kuwa ameambukizwa maradhi ya UKIMWI alilia sana kama anavyosema msimulizi:

Tabu alilia sana katika mwezi ule wa kwanza aliposhuku kwamba kaambukizwa UKIMWI, hakutaka kufanya shughuli zozote hapo nyumbani. Aliketi ameduwaa, akiwaza toka asubuhi hadi jioni. Watoto; Juma, Aisha na Abu walijua hali ya kusoneka kwa mama yao. Hivyo, walimsaidia kwa kila hali. Aisha alipika, Juma aliosha vyombo na Abu alikuwa tayari kutoa msaada kila alipohitajiwa. Familia yote ikawa kama imemwelekea mama yao. Naye Tabu alifarajika sana. Wakati mwingine matani ya Abu kwa Aisha yalimfanya asahau matatizo yake, akatabasamu au kuchangia utani. Hivyo, polepole, bila kujua, watoto walifanikiwa kumrudisha mama yao katika hali ya kawaida. Grace pia alichangia kwa

kumpa moyo dada yake asiwe na shaka, abaki na imani na asubiri kwenda kupima iwapo alikuwa ameambukizwa (Mkufya, 2005:113).

Ni wazi kuwa upendo unachangia kumrudisha Tabu katika hali yake na kumfanya asahau kuwa ameambukizwa. Kwa hivyo, msimulizi anasisitiza kuwa ni bora kuwaonyesha upendo walioathiriwa. Kwa kuwachukia na kuwatenga mfano Ngoma katika riwaya hii na Fumbwe katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), kunawafanya wahusika hawa kufa haraka kutokana na upweke. Kwa hivyo msimulizi anakashifu chuki dhidi ya waliougua na kuhimiza upendo pamoja na kuwafurahia kama njia ya kupiga vita unyanyapaa.

Njia nyingine ya kupiga vita unyanyapaa ni kuwahudumia vyema wanaougua hasa wakiwa wamelazwa hospitalini. Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), tunaona Dkt. Hans anavyomwonyesha Tabu upendo na kumpa tumaini la kukabiliana na maradhi haya. Dkt Hans anamwambia Tabu:

“Vizuri, lakini kuna mengine. Ukipima ukajua mapema kwamba una virusi, utajitahidi kuutunza mwili wako ili uweze kuishi zaidi ingawa una virusi. Utatumia maelekezo ya lishe, matibabu ya maradhi ya kawaida na pia kutumia dawa za kupunguza kasi ya kuongezeka kwa virusi. Ukizitumia dawa hizo vizuri zitaongeza muda wako wa kuishi ...”

“Sasa kwani kuishi kuna kipimo maalum? Kwani wewe unajua mimi nitakufa kesho au kesho kutwa au miaka saba ijayo?” “Sijui, lakini wewe hufi kwa UKIMWI.”

“Hata kama pengine sina virusi kama unavyodhani, lakini kufa ni kule kule. Nitakufa siku fulani ijayo. Yaweza kuwa leo au kesho. Siyo ajabu kwamba wewe mwenye virusi ukarefusha maisha yako kwa miaka kumi, kama ukifuata masharti yetu. Na mimi nisiye na virusi nikafa mapema zaidi kwa malaria kali mwaka huu au kwa kugongwa na gari mwaka kesho (Mkufya, 2005:186-187).

Daktari Hans anampa Tabu matumaini kuwa hata akipima na kupata kuwa ana virusi anaweza kuyarefusha maisha yake. Iwapo mwathiriwa atafuata masharti ya daktari, si lazima afe haraka. Anaweza kuishi zaidi ili awalee wanawe na kuwapa miongozo ya maisha. Bali na kumpa matumaini, Tabu anapopimwa na kupatikana ana virusi, Dkt.

Hans anamwonyesha Upendo. Kama tunavyoambiwa:

“Hans, kufa kwa UKIMWI ni aibu, ndugu yangu!”

“Naelewa dada. Ni aibu kwa watu wajinga. Lakini kwa jinsi ulivyonieleza kuhusu maisha yako, huna sababu ya kuona aibu. Dkt. Hans akachukua kanga ya Tabu iliyokuwa inataka kudondoka chini, akamfuta machozi nayo. Tabu akasimama, akiwa anamtazama kwa macho yenye shukrani, ingawa uso ulikuwa na huzuni. “Asante Hansi, asante ndugu yangu. Umenionyesha upendo, asante. Hata nikiugua nitakumbuka yote uliyosema na wewe nitakukumbuka”.

“Hutaugulia mbali, tutakuwa pamoja. Nitakuorodhesha katika wagonjwa wangu. Nitakuuguza, tutaugua sote, mimi na wewe ...” Tabu akamtazama tena. Akatabasamu na machozi yakaanza tena kutoka Hans akayafuta. “Sasa usilie tena. Jiandae kuishi na virusi, ukiwalea watoto wako mpaka hapo tutakapofika mwisho (Mkufya, 2005:194).

Vilevile katika riwaya ya *Kala Tufaha* (2007), Fumbwe alipolazwa hospitalini, Daktari

Kala alimhudumia Fumbwe vizuri kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Maskini Fumbwe! Ndwele zimemtoa nyumbani akaja piga kambi hospitalini. Mafao yake ya kustaafu yote huenda kwa matibabu. Bahati yake kukumbana na daktari kijana mchangamfu, Daktari Kala Tufaha. “Kijana mzuri sana huyu, Mungu amuweke,” husema Fumbwe. “Hatuna nasaba naye na muone jinsi anavyonishughulikia. Wala si mtu wa kitu kidogo.” Daktari Kala hakosi kila siku kumpitia mgonjwa wake kumjulia hali. Awe kazini hayupo kazini atapata wasaa wa kumpitia Fumbwe. Ikitokea asafiri, huwapigia wenziwe simu hapo hospitalini kujulia hali ya mgonjwa wake (Omar, 2007:170).

Msimulizi anahimiza huduma bora kutoka kwa madaktari na wauguzi kama njia ya kupiga vita unyanyapaa. Kama vile Kala anavyomshughulikia Fumbwe, madaktari

wanafaa kuwashughulikia wagonjwa na kuwaonyesha upendo. Kwa njia hii unyanyapaa utapigwa vita na tunaweza kukabiliana na maradhi ya UKIMWI.

Kwa mujibu wa mhimili wa mtazamo wa msimulizi, msimulizi anahimiza wanajamii kuwaonyesha waathiriwa mapenzi. Hakika Dkt. Hans anatimiza ahadi yake kwa kumuuguza Tabu hadi mwisho, Kama tulivyosema awali kuwa ni vyema kumtuliza mwathiriwa kwa njia ya kimaadili, tunaona madaktari hawa: Dkt. Hans na Kala wakijiweka katika tajriba ya wahusika, wanawazia maisha ya wagonjwa hawa, wanaweka fikra na hisia zao pamoja nao na kuanza kuandika sura mpya ya maisha ambayo msuko wake umetibuliwa na maradhi haya. Tunaona madaktari hawa wakiwapa matumaini na kuwasaidia kukadiria thamani ya maisha, mipango ya maisha, mirathi na vilevile kuwa nao katika upeo huu wa mgogoro wa nafsi, mwili na akili. Kwa hivyo, riwaya hizi zimeonyesha kuwa kuna haja ya madaktari kuwauguza waathiriwa bali sio tu kuwapa dawa. Madaktari wanafaa kujiweka katika hali ya waathiriwa hawa na kuwauguza katika upendo na kuwapa tumaini kama wanavyofanya Dkt. Hans na Dkt. Kala. Hii ni hatua chanya katika kukabiliana na maradhi haya. Kwa njia hii tunaweza kupiga vita unyanyapaa na kuyarefusha maisha ya waathiriwa.

4.8 KUPIMA DAMU KABLA NDOA KATIKA RIWAYA YA *Ua La Faraja* (2005).

Katika riwaya ya *Ua la Faraja* (2005), msimulizi anaangazia utamaduni mpya wa kupima damu kwa wanandoa kabla kuoana ili kuthibitisha kuwa hawana virusi vya

UKIMWI. Mhusika Queen anapofariki, anaandika wosia. Katika wosia huo anamwandikia Omolo akisema:

Mwisho: Nakuaga rafiki na mpenzi wangu. Yalikuwa mapenzi ya muda mfupi, lakini niliyathamini kushinda yote niliyowahi kupata. Nina uhakika sijakuambukiza huu ugonjwa, tulitumia mipira. Tafadhali, nenda ukahakikishe. Kapime damu kisha, nakusihi, tafuta mpenzi, naye akapime damu, muoane. Uwe mwaminifu na yeye awe mwaminifu kwako. Ngono za holela ni jambo la kipuuzi. Nimegundua ngono haina starehe yoyote zaidi ya majuto baada ya kuifanya. Wewe ni hodari sana wa ukweli huu lakini uoe uzae. Mke wako akikubali, kama ni mtoto wa kike mwite Tumaini, jina la mama yangu. Maisha yakikosa matumaini yamekosa maana, yanaishia fadhaa (Mkufya, 2005:178).

Kwa mujibu wa mhimili wa mtazamo wa msimulizi, msimulizi anahimiza wanajamii kuwa kuna haja ya kupima damu kabla ya ndoa ili kuhakikisha kuwa jamii inapata kizazi kipya kisicho na maradhi haya kama njia ya kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Iwapo tutazingatia mawaidha ya Queen, tunaona kuwa kuna matumaini katika kukabiliana na UKIMWI. Kilele cha riwaya hii ni Grace kuwa mjamzito na kujifungua mtoto wa kike na kumpa jina Tumaini kama tunavyoambiwa na mwandishi:

Omolo na Grace walikaa kimya, kila mmoja akitafakari. Ndipo baada ya kimya kirefu, Dkt. Hans aliifungua ile chupa ya *champagne*. Kizibo kikaruka juu, povu likafoka na wote wakasherehekea ujauzito wa Grace. “Utamwita nani akizaliwa wa kiume?” Dkt. Hans aliuliza. “Tumaini,” Grace alijibu. Omolo akashangaa. “Hutamwita Faraja?” Dkt. Hans aliuliza. “Yote ni sawa lakini mimi napenda Tumaini,” Grace alijibu. “Mimi naona mtoto huyu atakuwa faraja kwako na familia yako kubwa uliyokabidhiwa na dada”. “Ndiyo, lakini tukimwita Faraja tutakuwa kama bado tunayasononekea mauti. Naona Tumaini ni jina lenye nguvu zaidi.” “Je, akizaliwa wa kike, utamwita nani?” Dkt. Hans alizidi kuuliza. “Nitamwita hilo hilo Tumaini,” Grace alijibu.

Omolo akazidi kushangaa. Miaka saba iliyopita Queen alimsihi Omolo kwamba akizaa mtoto wa kike amwite Tumaini. Lakini Omolo aliubakisha huo mshangao wake moyoni. Ikawa siri ambayo aliogopa akiisema itamuudhi mkewe (Mkufya, 2005:378).

Inadhihirika wazi kuwa wanajamii wana matumaini. Iwapo tutajiepusha na uasherati, tupime damu kujua hali zetu kiafya, wanandoa wawe waaminifu, tutapata kizazi kipya kisichokuwa na maradhi ya UKIMWI. Kwa hiyo, msimulizi hafi moyo, si mtamaushi. Ana matumaini kuwa tutaweza kukabiliana na maradhi haya.

Maoni haya yanashadidiwa na Mutembei (2011) ambaye anasema kuwa, maradhi ya UKIMWI yameleta utamaduni mpya wa kupima damu ili kuthibitisha hali ya wanaohusika kabla ndoa. Nchini Tanzania, makanisa yana sheria kuwa sharti wanandoa kupima damu kabla ya kufunga ndoa. Jambo hili ni zuri kwa kuwa wanajamii wanaweza kudhibiti kuenea kwa maradhi ya UKIMWI iwapo watapimwa na kuwa waaminifu.

4.9 HITIMISHO

Sura hii ililenga kuchunguza jinsi riwaya zilizoteuliwa zinavyoweza kutumiwa katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI na changamoto zake. Baadhi ya njia zilizopendekezwa na waandishi hawa ni kama; kuepuka uasherati. Ngono za kiholela zilionekana kama njia ya kueneza maradhi haya. Matumizi ya mipira ya kondomu pia yalionekana kama njia ya kujiepusha kupata haya maradhi na kutowaambukiza wanajamii wengine. Hata hivyo, kuna wanajamii kama Ngoma ambao wanatumia mipira baada ya maambukizi jambo ambalo linaenda kinyume na vita dhidi ya maradhi haya. Katika ndoa, uaminifu ulionekana kuwa njia bora ya kufuatwa na wanandoa ili kuepuka maradhi haya. Umaskini ulionekana kuwa chanzo cha kuambukizwa na kuenea kwa

maradhi haya. Hata hivyo msimulizi anapendekeza kupiga vita umaskini na kuwawezesha wanawake kiuchumi kama njia mwafaka ya kuyakabili.

Ubabe-dume vilevile ulionekana kuwa kikwazo kikubwa katika vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Katika kushughulikia suala hilo, kulikuwa na haja ya kudengua ubabe-dume na kuwaona wanawake kama nguzo muhimu katika vita dhidi ya UKIMWI. Kwa hivyo, si bora kuwadhalilisha na kuwapuuza. Msimulizi anakashifu vipingamizi vya kijamii kama ndoa kama njia mojawapo inayochangia kuenea kwa maradhi haya. Wanajamii walionekana kuwa na mwikio chanya kwa kujaribu kupiga vita unyanyapaa na kuwaonyesha waathiriwa mapenzi. Mwisho, ilionekana kuwa hata katika vuguvugu hili kuna matumaini. Kuzaliwa kwa Tumaini ni ishara kuwa waathiriwa wakizingatia lishe bora na kufuata maagizo ya daktari wanaweza kuishi kwa muda mrefu. Kwa wale ambao hawajaambukizwa, kuna haja ya kuambaa uasherati. Wanajamii wanapotaka kuoia ni vizuri kupima damu ili kujua hali yao na kisha kuwa waaminifu katika ndoa. Iwapo wanajamii watafanya hivyo, kuna uwezekano wa kuwa na kizazi kipya kisicho na maradhi ya UKIMWI.

Japo njia hizo zote zinaonekana kuchangia katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI, katika riwaya ya Mkufya (2005: 13), mhusika Omolo anamwambia Jose kuwa yeye anaona ni busara zaidi katika kupiga vita tabia ya watu kushabikia ngono. Kwenye sinema, kwenye muziki wote wa Kiafrika na kila mahali. Kulingana naye, kuna haja ya kupiga vita ushabiki na sanaa za kushabikia ngono. Yeye anaona wanajamii wanafaa

HITIMISHO

5.0 UTANGULIZI

Katika sura ya nne, tulieleza jinsi riwaya zilizoteuliwa zilivyoweza kutumiwa katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Njia zilizopendekezwa ni kama; matumizi ya mipira ya kondomu, kuepuka uasherati, kuwa waaminifu katika ndoa, kuacha ubabe dume, kuwawezesha wanawake kiuchumi, kutupilia mbali vikwazo vya kijamii vinavyowafanya wanajamii wengine kulazimika kuambukizwa UKIMWI, kupiga vita unyanyapaa na kuwaonyesha upendo waathiriwa pamoja na kuwapa matumaini. Katika sura hii, tutahtimisha tasnifu na kutoa mapendekezo kwa utafiti zaidi.

5.1 MUHTASARI WA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi suala la UKIMWI lilivyosawiriwa katika riwaya za Kiswahili: *Ua la Faraja* [2005] na *Kala Tufaha* [2007]. Utafiti ulilenga kuchunguza usemi mbalimbali uliotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Pia utafiti ulilenga kuchunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Vilevile utafiti ulidhamiria kuonyesha jinsi riwaya hizi zilivyotumiwa kukabiliana na maradhi ya UKIMWI na changamoto zake. Katika kuyafikia malengo ya utafiti huu, jumla ya riwaya mbili ziliteuliwa; *Ua la Faraja* na *Kala Tufaha*. Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu kusudio, ambayo iliwezesha kuafiki malengo ya utafiti.

Matumizi ya nadharia zilizoteuliwa ilitokana na sababu kwamba zote mbili zilitarajiwa kuhimili kazi hii. Nadharia ya kwanza ilikuwa Naratolojia. Mihimili iliyoongoza kazi hii

ni ile ya kuona usemi kama kipengele kikuu cha nadharia hii. Mhimili huu ulionekana kuwa muhimu katika kumsaidia mtafiti kuchunguza usemi mbalimbali uliotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Mhimili wa pili uliona wahusika kama sehemu kuu ya masimulizi. Mhimili huu ulimwezesha mtafiti kuchunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Mhimili wa watu ulikuwa mtazamo wa msimulizi ambao ulimwezesha mtafiti kuona masimulizi haya kama yenye lengo la kuwaonya watu dhidi ya njia zinazoweza kuwafanya kuepuka maradhi haya, na kuwafariji waathiriwa kwa kuwapa matumaini. Nadharia nyingine iliyoongoza utafiti huu ni ile ya Matendo ya Usemi. Kulingana na nadharia hiyo, lugha hutumiwa kutenda, baadhi ya matendo hayo ni kama kuonya, kukashifu, kuhimiza kati ya mengine. Mhimili iliyoongoza utafiti huu ni ile ya tendo la usemi na tendo la kusudio. Tendo la usemi lililenga kuona masimulizi haya kama usemi wenye maana fulani; kuonya ambao hawajapata maradhi haya dhidi ya mienendo inayoweza kuwafanya kuyapata na kuhimiza waathiriwa kwa kuwapa matumaini. Tendo la kusudio lililolenga kuyaona masimulizi haya kama yenye kusudi fulani kusudi hilo likiwa kuwafariji waathiriwa kwa kuwapa matumaini na kuwaonya wanajamii dhidi ya mienendo inayoweza kuwafanya kuambukizwa maradhi ya UKIMWI.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti; maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilichunguza usemi mbalimbali uliotumiwa kuyaashiria maradhi ya UKIMWI. Baadhi ya usemi uliotumiwa ni kama: UKIMWI ni uchawi, laana, kifo, maradhi mapya, mwiba, janga, kudra na mdudu. Japo semi hizi zilitumiwa katika kuyanyanyapaisha maradhi haya, tunaona jamii inapata mwamko mpya pale inapoanza kuyakubali maradhi haya na kuyazungumzia bila aibu.

Sura ya tatu ilichunguza athari ya maradhi ya UKIMWI kwa wahusika. Athari hizo ni kama unyanyapaa, uyatima, uadilifu wa kifasihi, kubadilisha wahusika, utamaushi pamoja na kuonyesha vile riwaya hizi zinavyoweza kutumiwa kujua jamii. Hii ni kama kuonyesha ujasiri, na udhaifu wa wanajamii.

Sura ya nne ilichunguza jinsi riwaya hizi zinavyoweza kutumiwa kukabiliana na maradhi ya UKIMWI na changamoto zake. Kulikuwa na njia za kuwafariji walioathiriwa pamoja na njia za kuepuka kuambukizwa maradhi haya.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu. Hitimisho hilo limetoa utangulizi na muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye sura hii imeeleza matokeo, na mapendekezo ya tafiti ambazo zinaweza kufanywa katika siku za baadaye.

5.2 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi suala la UKIMWI lilivyosawiriwa katika riwaya za *Ua la Faraja* (2005) na *Kala Tufaha* (2007). Uchanganuzi wa riwaya zilizoteuliwa umeonyesha kuwa, tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI, jamii imepitia hatua mbalimbali. Kwanza kwa kuyapa maradhi haya majina ya kutisha na baadaye kubadili mielekeo yao kuyahusu. Usemi wenyewe ni kama UKIMWI ni uchawi, laana, kifo, janga. Katika kuyatambua kwa majina haya tunaona unyanyapaa unavyoingizwa katika jamii na kuwahukumu waathiriwa, jambo linalokuwa kikwazo katika kukabiliana nayo. Hata hivyo baada ya kupata ufahamu kuyahusu tunaona wanajamii wakibadilika na kuanza kupinga vita unyanyapaa. Kwa njia hii tunaona mwitikio chanya wa wanajamii wanapoanza kutaniana kuhusu maradhi haya. Usemi kama UKIMWI ni mwiba au mdudu unaanza kutumiwa. Kutokana na ufahamu huu tunaona mabadiliko chanya yanayochangia katika kukabiliana na maradhi haya.

Lengo la pili lilihusu kuchunguza athari ya maradhi haya kwa wahusika. Baadhi ya athari hizo ni kama unyanyapaa. Unyanyapaa ulionekana kutokea katika sehemu tofauti. Kwa mfano kutokana na unyanyapaa ndoa zinavunjika, waathiriwa wengine wanashindwa kukabiliana na maradhi haya na mwishowe kujiua, wahusika wengine wanachukiwa na kutengwa na jamii, jambo ambalo linawafanya kutotafuta matibabu katika vituo vya afya.

Athari nyingine ya maradhi haya ni uyatima. Waathiriwa wanapougua na kufa, wanaacha watoto mayatima ambao wanalazimika kuwa wazazi na kuanza kuwalea wenzao kabla ya

umri. Wengine wanaacha shule na kutafuta kazi kwa ajili ya kuwalea wenzao. Mayatima hawa wanakuwa mzigo katika jamii pamoja na serikali kwa sababu serikali haina uwezo wa kuwachunga vilivyo pamoja na kutoa matibabu kwa waathiriwa. Hata hivyo utafiti umeonyesha mchango wa wanajamii wengine katika kuwasaidia mayatima hawa. Kwa mfano, kuna mradi wa kuwasaidia mayatima katika kuwapa mafunzo ya kutunza mali wanayoachiwa na wazazi wao. Hii ni njia nzuri ya kuwasaidia mayatima dhidi ya wanajamii walafi wanaongoja ndugu zao (wazazi wa mayatima hawa) kufa ili kurithi mali ile na kuwahini mayatima hawa.

Jambo lingine lililodhihirika kutokana na utafiti huu ni kuwa wahusika wanayapokea maradhi haya kwa njia tofauti. Wengine wanatamauka na mwishowe kujiua, wengine wanaogopa kutafuta matibabu na kuugua kwa uchungu na wengine wanakuwa na ujasiri wa kutafuta njia za kuishi na maradhi haya. Kwa wengine inakuwa chanzo cha kuwasimanga wengine hasa wale wasio na maradhi haya.

Kifasihi tunaona maradhi yanaweza kutumiwa kuwabadilisha wahusika. Tunaona wahusika wenye ubinafsi wakibadilika kutokana na kuambukizwa maradhi haya. Kwao, inakuwa ni mwanzo wa kuacha kuwadhulumu wanajamii wengine na kuwa na utu wa kuweza kuona ubaya wao na kuwathamini watu wengine kama binadamu. Vilevile tunaona maradhi yakitumiwa kuonyesha uadilifu wa kifasihi. Wahusika wenye maadili wanafunzwa kwa kuepushwa na maradhi haya na wale wabinafsi na wadhalimu

wanayapata. Mwishowe wanaogua kwa uchungu na kufa. Kwa njia hii fasihi inachukua nafasi yake inayostahili: ya kuwatuza waadilifu na kuwaadhibu wanaokosa.

Lengo la tatu lilikuwa kuchunguza nafasi ya riwaya hizi, katika kukabiliana na maradhi ya UKIMWI na changamoto zake. Kutokana na utafiti, ilibainika kuwa matumizi ya mipira ya kondomu ni njia bora ya kuepuka kuambukizwa maradhi haya. Hata hivyo kuna wanajamii kama vile Ngoma ambao wanatumia mipira baada ya kuwaambukiza wengine na basi kutofaidi chochote katika matumizi yale. Njia nyingine iliyojitokeza ni kuepuka uasherati. Kwa wanandoa, uaminifu ni njia nzuri ya kuepuka kuambukizwa. Vipingamizi vya kijamii kama vile asasi ya ndoa ilionekana kuchangia katika kuwadhalilisha wanawake. Kwa kuogopa jamii wanawake walilazimika kuvumilia katika ndoa dhalimu na mwishowe kuambukizwa maradhi haya. Vilevile ubabe-dume pamoja na umaskini ulichangia pakubwa katika kufanya maradhi haya kuenea. Kutokana na utafiti kuna haja ya kupiga vita ubabe-dume pamoja na kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kupunguza kuenea kwa maradhi haya. Unyanyapaa pia ulionekana kuwa kikwazo lakini tunaona baada ya muda jamii inabadilika. Usemi wenye kuyanyanyapaisha maradhi haya unafifia. Utambuzi wa wanajamii unawapa nafasi nzuri ya kuelewa kuwa unaweza kuwa na maradhi haya na ukaishi kwa muda mrefu iwapo utafuata maelekezo ya daktari. Matokeo yake ni kuanza kuyatania maradhi haya jambo ambalo linakuwa njia chanya ya kukabiliana nayo.

Vilevile tunaona mielekeo ya wanajamii ikibadilika. Waathiriwa wanaonyeshwa mapenzi, na kupewa tumaini kutoka kwa wanajamii wote wakiwemo madaktari. Kilele cha utafiti huu ni kuzaliwa kwa Tumaini. Ishara kuwa tunaweza kupata kizazi kipya kisicho na maradhi ya UKIMWI iwapo tutapima damu kabla ya ndoa na kuwa waaminifu baada ya ndoa. Kwa walioathiriwa ni vizuri kufuata maagizo ya daktari jambo ambalo litafanya waathiriwa kuyarefusha maisha.

5.3 MCHANGO WA UTAFITI

Kutokana na utafiti huu, imebainika kwamba fasihi, hususan riwaya (masimulizi), inaweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe kuhusu maswala ibuka yanayokumba jamii. Utafiti umeonyesha kuwa mbali na sayansi, fasihi (riwaya) inaweza kutumiwa kukabiliana na maradhi ya UKIMWI. Tofauti na kuburudisha wanajamii, ujumbe muhimu unaweza kupitishwa katika riwaya. Ujumbe unaweza kuwasaidia wanajamii kuepuka kuambukizwa maradhi ya UKIMWI pamoja na kuwapa matumaini na kuwafariji walioathiriwa.

Utafiti pia umeshirikisha nadharia mbili: ile ya Naratolojia pamoja na Matendo ya Usemi. Kutokana na usaidizi wa nadharia hizi mbili, utafiti huu umebainisha kuwa mbali na kuburudisha, masimulizi yanaweza kutumiwa kupitisha ujumbe katika jamii. Ujumbe wenyewe ukiwa unalenga masuala yanayoikabili jamii. Kwa kusoma masimulizi haya, wanajamii wanaweza kupata ujumbe utakaowawezesha kukabiliana na hali zinazowazingira. Katika muktadha huu, masuala ya UKIMWI ambayo yameitatiza jamii

kwa miongo mitatu yanaweza kutatuliwa. Vilevile masimulizi haya yanawapa wanajamii matumaini kuwa suluhisho litapatikana.

5.4 MAPENDEKEZO

Utafiti ulishughulikia suala la UKIMWI katika riwaya za Kiswahili. Tulionyesha usemi mbalimbali uliotumiwa na wanajamii tangu kugunduliwa kwa maradhi ya UKIMWI. Vilevile tulionyesha mabadiliko ya usemi baada ya wanajamii kupata ufahamu kuhusu maradhi haya. Pamoja na hayo tuliangalia jinsi wahusika wanavyoathirika na maradhi haya. Mbali na kuangalia jinsi riwaya hizi zinavyoweza kutumiwa kukabiliana na maradhi haya. Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha jinsi UKIMWI ulivyoshughulikiwa katika fasihi simulizi. Utafiti unaweza kufanywa katika jamii tofauti kwa kuwa fasihi simulizi ni tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kuchunguza jinsi nyimbo pendwa zilivyoshughulikia suala la UKIMWI. Nyimbo hizi zinaweza kuangaliwa kwa kuchunguza ujumbe uliopitishwa tangu kugunduliwa kwa maradhi haya hadi sasa.

Vilevile kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika tamthilia ya Kiswahili ili kujua jinsi suala la UKIMWI lilivyoshughulikiwa. Ni muhimu pia kuchunguza viwango vya athari ya maradhi haya kutegemea jinsia. Ni jinsia ipi iliyoathirika zaidi na mchango wa kila jinsia katika kukabiliana na maradhi haya kwa kuzingatia nadharia zinginezo. Utafiti huu

utakuwa na mchango katika kuonyesha kuwa hakika tanzu zote za fasihi zina nafasi kubwa katika kukabiliana na masuala ibuka hususan UKIMWI.

Alim, M. (2003). 'The Relevance of Formal and Vocational Training to Girls' Employment Opportunities in Education and Development in West Africa' *Journal of Education* 22 (3) 625-644.

Aronson, E. (2003). *The Construction of the African Perceptions on Death Through Oral Tradition*. University of Helsinki.

<http://www.kuoliopainotus.fi/kuoliopainotus/kuoliopainotus.html>

Arthur, W. F. (1995). *The Wounded Storyteller: Body Illness and Ethics*. Chicago: University of Chicago Press.

Cherry, G. (2002). 'African Novelists Mothers' *East African Standard*. *Mid Week Magazine* 10. 8th November

Greene, J. L. C. (1963). *How to Do Things With Words*. Chicago: Clarendon Press.

H.R.C. (2004). 'Pope rejects condoms for Africa' <http://www.kenya.com/kenya/040127k.htm/7102911>

Introduction to the Structure/Analysis of Narrative Discourse

MAREJELEO

Akuffo, F. (1987). 'Teenage Pregnancies and School Drop-outs: The Relevance of Family Life Education and Vocational Training to Girls' Employment Opportunities' in *Sex Roles, Population, and Development in West Africa*. 22 (3) :625-644.

Alembi, E. (2002). *The Construction of the Abanyole Perceptions on Death Through Oral Funeral Poetry*. University of Helsinki.
<http://ethesis.helsinki.fi/julkaisut/hum/kultt/vk/alembi>.

Arthur, W. F. (1995). *The Wounded Storyteller: Body Illness and Ethics*. Chicago: University of Chicago Press.

Atieno, D. (2002). 'Africa Newest Mothers' *East African Standard: Mid Week Magazine*. Nairobi: 6th November.

Austin, J. L. C. (1962). *How to Do Things With Words*. Chicago: Clarendon Press.

B.B.C. (2005) 'Pope rejects condoms for Africa'.
<http://news.bbc.co.uk/2/hi/europe/4081276.stm> 7/10/2011

Barthes, R. (1975). *An Introduction to the Structural Analysis of Narrative Discourse*. Oxford: Blackwell.

Bertoncini, E.Z. (2005). William, E. Mkufya's Latest Novel *Ua la Faraja*: A commitment to the Fight Against HIV/AIDS. *Swahili Forum* 12. 3-13.

Biblia, (1997). *Maandiko Matakatifu*. Dodoma: Bible Society of Tanzania

Bor, R. & Elford, J. (1998). *The Family & HIV Today*. London: Cassell.

Butt, R. (2009). "Pope claims condoms could make African Aids crisis worse." *The Guardian*. 7/10/2011.

Chatman, S. (1990). *Coming to Terms: The Rhetoric of Narrative in Fiction and Film*. Ithaca: Cornell UP.

Cienki, A. (2005). Researching Conceptual Metaphors that (may) Underlink Political Discourse www.eis.bris.ac.uk/potfc/Granada/papers/Genki.pdf, Accessed on 20th March 2011.

Cleland, J. & Ferry, B. (1995). *Sexual Behaviour and AIDS in the Developing World*. London: World Health Organization/ Taylor & Francis.

Cuddon, J. A. A. (1997). *A Dictionary of Literary Terms*. (4th Edition). New York: Penguin.

Dolezel, L. (1973). *Narrative modes in Czech Literature*. Toronto: University of Toronto

Easthope, A. & McGowan, K. (ed) (1992). *A critical & Cultural Theory Reader*.
Buckingham. Open University Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. England: Person Education Limited.

Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social change*. Cambridge: MA: Blackwell.

Fairclough, N. L. & Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis. In: *Discourse Studies A Multidisciplinary introduction*. Van Dijk (ed) Vol. 2 pp 258-284 London: Sage Publications.

Fairclough, N.L. (1992). 'Discourse and Text: Linguistic and Intertextual Analysis within Discourse Analysis. In: *Discourse and Society*. 3: 193-217.

Fairclough, N.L. (1995). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of Language*. London: Longman.

Gachara, M. (2005). *A Pragmatic Analysis of The Language Used to Campaign Against HIV/AIDS: A Case Study of Kikuyu Speakers in Nairobi and Nyeri*. Unpublished M. A. Thesis, Kenyatta University.

Genette, G. (1980). *Narratives Discourse*. New York: Cornell University Press.

Ghosh, J. & Kalipeni, E. (2004). 'Rising Tides of AIDS in Southern African in *HIV & AIDS in Africa: Beyond Epidemiology*. Kalipeni E. et al Malden: Massachusetts: Blackwell Publishing Ltd. pp 304-315.

Gikandi, S. (1987). *Reading the African Novel*. London: James Currey.

Gorman, A. G. (1993). *The Body in Illness and Health: Themes and Images in Jane Austen*. New York: Peter Lang Publishers.

Harman, W. & Holman, C. (2006). *A Handbook to Literature* (10th Edition) Dorling Kindersley. India.

Hawthorn, J. (2001). *Studying the Novel (4th edition)*. London: Oxford University Press.

<http://www.avert.org/hiv-aids-stigma.htm>. Accessed on 27. 04. 2011.

<http://www.bbc.co.uk/mediaselector/check/player/noi/newsid-6900000/newsid-6903100.6/11/2011>.

<http://www.ifeas.uni-mainz.de/swafo/sf12/Bertoncini.pdf> Accessed on 11.12.2010.

Ileri, A. (1981). *The African Experience in Literature and Ideology*. London: Heinemann.

Iribemwangi, P. I. (mhariri) (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Isichei, E. (2004). *Voices of The Poor in Africa: Moral Economy and The Popular Imagination*. Rochester: University of Rochester Press.

Juma, L. (2001). "Ongeri's Appeal to Clerics on Condoms" *Kenya times*. Nairobi Saturday, 10th August.

Katheya, E. (2002). 'Use Condom at Your Own Spiritual Physical Peril. *East African Standard*. Nairobi: 7 March.

Kebasso, G. na wengine (2005) "Call For Government to Protect AIDS Victims" *Kenya Times* .Nairobi. Thursday, 1st December.

Kimani, H. W. (2006). *Uwiano wa Picha na Matini Katika Mabango ya Matangazo ya UKIMWI: Mtazamo wa Kisemiotiki*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Kingei, K. na Kobia, J. (wahariri) (2007). *Likizo ya Mauti na Hadithi Nyingine* . Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kleinman, A. (1988). *The Illness Narratives: Suffering Healing and the Human Condition*. New York: Basic Books.

Kobia J. M. (2008). 'Metaphors on HIV/AIDS Discourse Among Oluluyia Speakers of Western Kenya'. in *Critical Approaches to Discourse Analysis Across Disciplines*. <http://cadaad.org/ejournal>. Vol 2(2): 48-66.

Kristen, M. (1991). *The Linguistics Encyclopedia*. London: Routledge.

Lyons, M. (2004). 'Mobile Populations and HIV/AIDS in East Africa' in *HIV & AIDS in Africa: Beyond Epidemiology*. Kalipeni, E. et al. Malden: Massachusetts: Blackwell Publishing Ltd. pp 175-190.

Manfred, J. (2005). *Narratology: A Guide to the Theory of Narrative*. Cologne: University of Cologne.

Mark, J. L. (1987). *The body of the mind: The Bodily Basics of Meaning, Imagination and Reason*. Chicago: University of Chicago.

Mkufya, W. E. (2005). *Ua la Faraja*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Muiruri, B. (2010). "Living Positively" *Daily Nation*. Nairobi. Saturday, 29th May.

Muriungi, A. (2004). "Healthy Bodies Versus Diseased Bodies: Romance as a Trope of Social Order in Kenyan HIV/AIDS Fiction" *Social Dynamics, Volume 30, Issue 2* (2004).

Muriungi, A. (2006): *Romance, Love and Gender in Times of Crisis: HIV/AIDS in Kenyan Popular Fiction*. Ph.D. Thesis. University of Witwatersrand. Johannesburg. Unpublished.

Muriungi, A. (2007). "Chira and HIV/AIDS: The (RE) Construction of Sexual Moralities in Kenyan Popular Fiction" in *Urban Legends, Colonial Myths: Popular Culture and Literature in East Africa*. Eritrea: Africa world press, Inc. pp 281-305.

Mutembei, A. K (2011). 'A Comparative Study of Plays on AIDS From Tanzania and The USA' in Makokha, J. K. et al. *East African Literature: Essays on Written and Oral Traditions* Berlin: Logos Verlag pp 415-435.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili 1982-2009*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Mwita, J. M. (1993). "Tamthilia Mbili za Ebrahim Hussein: 'Arusi na Kwenye Ukingo wa Thim'". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Haikuchapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

NACC (2005). National HIV/AIDS Monitoring and Evaluation Framework. Nairobi: NACC.

Nation Correspondent, (2006). 'Church Says sorry to Aids Patients'. *Daily Nation*. Nairobi. 16th March.

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel*. Nairobi: Heinemann.

Ngoyani, D. S. (2006). Lexical Innovation in Tanzania's Political Discourse. In: *KISWAHILI*. Vol. 69. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Odhiambo, K. na Oduma, R. (2008). "Some Reflections on The Performance of The Court Interpreter in Kenya" *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press. 343-351.

Ogude, J. & Nyairo, J. (2007) *Urban Legends, Colonial Myths: Popular Culture and Literature in East Africa*. Eritrea: Africa world press, Inc.

Okoth, D. (2006). 'Women Still bear the brunt of AIDS in Africa'. *East African Standard*. Nairobi: 29th November.

Omar, B. (2005). *Kala Tufaha*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Onyango, J. O. (2007). *Discursive Masculinities and the War Against AIDS: Kenyan Experience*. Commission for Development for Studies at the Austrian Academy of Sciences. (KEF). 26/09/2011. (www.oeaw.ac.at/kef)

Ouko, J. (2000). "AIDS Campaign Kicks Off" *Daily Nation*: Nairobi. Thursday, 23rd March.

Parkin, D. (1978). *The Cultural Definition of Political Response: Lineal Destiny Among the Luo*. London: Academic.

Philips, O. (2004). 'The Invisible Presence of Homosexuality: Implications for HIV/AIDS and Rights in South Africa' *HIV/AIDS in Africa: Beyond Epidemiology*. Kalipeni, E. et al. Malden: Massachusetts: Blackwell Publishing Ltd. pp. 155-166.

Prince, G. (1973). *A Grammar of Stories*. The Hague: Mouton.

Raglan, L. (1956). *The Hero: A Study in Tradition Myth and Drama*. New York: Vintage Books.

Rimmon-Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Metuenen.

Schoepf, B. G. (2004). "AIDS, History and Struggles Over Meaning" in *Africa: Beyond Epidemiology*. Kalipeni E. et al Malden: Massachusetts: Blackwell Publishing Ltd. pp1-28.

Schoepf, B. G. et.al. (1988). 'Women, AIDS and Economic Crisis in Central Africa.' in *Canadian Journal of African Studies*. Oppong, C. (ed). Portsmouth: Heinemann. pp 154-164.

Schoepf, B.G. et al (1991). 'Gender, Power and Risks of Aids in Central Africa'. In *Women and Health in Africa*. M. Turshen, (ed) Trenton, N J: Africa World Press. pp. 187-203.

Serwadda, D. (1985). "Slim Disease: A New Disease in Uganda and its Association with HTLV-III Infection. *The Lancet*. October 19; 2. 849-852.

Sontag, S. (1989). *Illness as Metaphor and AIDS and its Metaphors*. Fawar: Strauss and Giroux.

Thavis, J. (2009). "Pope's condom comments latest chapter in sensitive church discussion". <http://www.catholicnews.com/data/stories/cns/0901232.htm>. 7/10/2011.

Thomas, F. (2008). "Indigeneous Narratives of HIV/AIDS: Morality and Blame in Time of Changes" *Medical Anthropology Volume 27. Issue 3, July*

Todoli, J. (2007). Disease Metaphor in Urban Planning. In: *Critical Approaches to Discourse Analysis Across Disciplines* 1(2): 51-60.

Ullman, S. (1972). *The Language of Jane Austen*. Oxford: Basil Blackwell.

UNAIDS, (2011). *UNAIDS World AIDS Day Report 2011*. <http://www.avert.org/Africa>.

United Nation, (2004). 'Worst Hit by Disease are Women' *Standard*: Nairobi. 16th July.

Vladimr, P. (1968). *Morphology of the Folk-Tale*. Trans Lawrence Scott. Austin: University of Texas Publishers.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (1991). *A Dictionary of Stylistics*. New York: London Group UK. Limited.

Wamitila, W. K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Wamitila, W. K. (2004). *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wellek, R. & Warren, A. (1973). *Theory of Literature*. Penguin Books Limited. Harmondsworth.

Zulu, M. E. et al (2004). *Urbanization, Poverty, and Sex: Roots of Risky Sexual Behaviours in Slum Settlements in Nairobi, Kenya in HIV/AIDS in Africa: Beyond*

Epidemiology. Kalipeni, E. et al. Malden: Masschusetts: Blackwell Publishing Ltd. pp.
167-174.

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY